ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	**-**	**SPIKA**
1.Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/

		Jimbo la Kiembesamaki
		11. Mhe. Riziki Pembe Juma - MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
		12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali - MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais
19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya

		Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga wa Nchi, Makamu wa pili wa Zanzibar/ la Mwera	-	Naibu Waziri Ofisi ya wa Rais Jimbo
22. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni
23. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
26. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Naibu Waziri wa Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake
28. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Juma Makungu Juma Waziri wa Ardhi, Nishati na	-	Naibu Maji,

	Mazingira/ Jimbo la Kijini	
30. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
31. Mhe. Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
32. Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil	-	Uteuzi wa Rais
33. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
34. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
35. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
36. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
37. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
38. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa
39. Mhe. Bahati Khamis Kombo	-	Jimbo la Chambani
40. Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-	Nafasi za Wanawake
41. Mhe. Hamad Abdalla Rashid	-	Jimbo la Wawi
42. Mhe. Hamida Abdalla Issa	-	Nafasi za Wanawake
43. Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Jimbo la Shaurimoyo
44. Mhe. Hassan Khamis Hafidh	-	Jimbo la Welezo
45. Mhe. Hidaya Ali Makame	-	Nafasi za Wanawake
46. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)	-	Jimbo la Mtoni
47. Mhe. Jaku Hashim Ayoub	-	Jimbo la Paje
48. Mhe. Khadija Omar Kibano	-	Jimbo la Mtambwe
49. Mhe. Machano Othman Said	-	Jimbo la Mfenesini
50. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti	-	Jimbo la Mtopepo
51. Mhe. Makame Said Juma	-	Jimbo la Kojani
52. Mhe. Maryam Thani Juma	-	Jimbo la Gando
53. Mhe. Masoud Abrahman Masoud	-	Jimbo la Bububu
54. Mhe. Miraji Khamis Mussa	-	Jimbo la Chumbuni
55. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha	-	Jimbo la Mtambile
56. Mhe. Mohamed Said Mohamed	-	Jimbo la Mpendae
57. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali	-	Jimbo la Uzini
58. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf	-	Jimbo la Bumbwini
59. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame	-	Nafasi za Wanawake
60. Mhe. Mussa Ali Mussa	-	Jimbo la Ole
61. Mhe. Mussa Foum Mussa	-	Jimbo la Kiwani
62. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	-	Nafasi za Wanawake
63. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis	-	Nafasi za Wanawake
64. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini	-	Jimbo la Dimani
65. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy	-	Jimbo la Chaani
66. Mhe. Nassor Salim Ali	-	Jimbo la Kikwajuni
67. Mhe. Omar Seif Abeid	-	Jimbo la Konde

68. Mhe. Panya Ali Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
69. Mhe. Rashid Makame Shamsi	-	Jimbo la Magomeni
70. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa	-	Nafasi za Wanawake
71. Mhe. Said Omar Said	-	Jimbo la Wingwi
72. Mhe. Said Hassan Said	-	Mwanasheria Mkuu
73. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma	-	Nafasi za Wanawake
74. Mhe. Salma Mussa Bilal	-	Nafasi za Wanawake
75. Mhe. Shaib Said Ali	-	Jimbo la Chonga
76. Mhe. Simai Mohammed Said	-	Jimbo la Tunguu
77. Mhe. Sira Ubwa Mamboya	-	Uteuzi wa Rais
78. Mhe. Suleiman Makame Ali	-	Jimbo la Ziwani
79. Mhe. Suleiman Sarahan Said	-	Jimbo la Chakechake
80. Mhe. Tatu Mohamed Ussi	-	Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Jimbo la Mkwajuni
82. Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
83. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Jimbo la Fuoni
85. Mhe. Zaina Abdalla Salum	-	Nafasi za Wanawake
86. Mhe. Zulfa Mmaka Omar	-	Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem	-	Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Nne - Tarehe 12 Februari, 2018

(Kikao Kilianza Saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Mwanaasha Khamis Juma) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha Mezani Mswada wa Kufuta Sheria ya Mwenendo wa Jinai Nam. 7 ya Mwaka 2004 na Kutunga Sheria ya Mwenendo wa Jinai na Kuweka Utaratibu Bora wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai na Usikilizaji wa Kesi za Jinai na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum: Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha Mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum kuhusu Mswada wa Kufuta Sheria ya Mwenendo wa Jinai Nam. 7 ya Mwaka 2004 na Kutunga Sheria Mpya ya Mwenendo wa Jinai na Kuweka Utaratibu Bora wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai na Usikilizaji wa Kesi za Jinai na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 21

Kutoshirikishwa Kwa Serikali Katika Miradi Ya Maendeleo

Mhe. Nassor Salim Ali (kny. Mhe. Suleiman Sarahan Said) - Aliuliza:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inastahiki pongezi katika jitihada zake za kuleta maendeleo kupitia miradi midogo na mikubwa ili kukuza uchumi wetu. Lakini kuna mambo ambayo hujitokeza katika baadhi ya maeneo katika kutekeleza miradi mikubwa ya ufadhili ambayo yanaleta usumbufu kwa wahusika kwa vile walengwa wa baadhi ya miradi hawashirikishwi katika miradi hiyo kikamilifu.

(a) Je, Serikali inalijua suala hili la baadhi ya mikataba katika ujenzi fulani kutokushirikishwa kikamilifu kwa sekta husika ya Serikali.

(b) Ni vikwazo gani au masharti gani yanayofanya kwa misaada, wafadhili au mikopo hiyo katika kufanya miradi hiyo bila kuwashirikisha wahusika wenye sekta husika.

(c) Je, Serikali inachukuwa hatua gani katika kuliondosha tatizo hilo kwani hupelekea kutokea changamoto mbali mbali zinazoifanya Serikali kupoteza fedha na kutokamilika kwa miradi hiyo na pia kutokukidhi baadhi ya madhumuni husika.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti naomba kujibu swali Nam. 21 la Mhe. Suleimain Sarahan Said, lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:

Kabla ya kujibu swali hili naomba kutowa maelezo mafupi ya utangulizi.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina utaratibu shirikishi wa kuandaa, kutekeleza na kufanya ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo inayoianzisha hapa nchini. Kupitia Tume ya Mipango ya Zanzibar, Serikali imetayarisha muongozo shirikishi wa utayarishaji na utafutaji wa fedha za ufadhili wa miradi ambapo sekta zote zinapaswa kufuata. Sekta za Serikali mara nyingi ndizo zinazoibua dhana za miradi na kwa kushirikiana na Tume ya Mipango huandaa andiko la mradi husika na hatimae kuwasilishwa Wizara ya Fedha na Mipango kupitia Idara ya Fedha za Nje kwa ajili ya ufadhili kwa ile miradi inayohitaji msaada au mkopo kutoka kwa wafadhili. Aidha, miradi inayoanzishwa na wafadhili pia hushirikisha wadau wote zikiwemo sekta husika katika hatua zote za mazungumzo na washirika husika.

Mhe. Mwenyekiti, suala la Serikali kuingia mkataba kati yake na chombo kingine linafanywa kwa umahiri na umakini mkubwa. Kwa sasa mikataba yote ya Serikali inapaswa kuwasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kupitiwa na kupata ushauri wa Kisheria. Hatua hii imesaidia sana kuondosha migogoro ya Kisheria baada ya mikataba hiyo kuwekwa saini na Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango au sekta zake.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ya utangulizi sasa naomba nijibu swali la Mhe. Suleiman Sarahan Said kama ifuatavyo:-

(a) Katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ikiwemo ujenzi inayofadhiliwa na washirikia wa Maendeleo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inawashirikisha kikamilifu sekta husika katika mikataba na utekelezaji wa miradi hiyo.

(b) Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika utekelezaji wa miradi mikubwa inayofadhiliwa na Washirika wa Maendeleo iwe

kwa njia ya Mikopo au Ruzuku haijawahi kupokea masharti au vikwazo vyovyote vinavyopelekea kutowashirikisha wahusika wa utekelezaji wa miradi hiyo. Aidha, miradi yote mikubwa inafuatiliwa na Wizara husika zikishirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango.

(c) Serikali imeweka Sheria na miongozo ya kufuatwa ili Serikali isipoteze fedha au kuepuka kutokamilika kwa Miradi au kutokukidhi madhumuni ya kutekelezwa miradi hiyo. Sheria hizo ni pamoja na sheria ya Fedha ya 2016, Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Serikali 2016, pamoja na miongozo yake, hizo zote zinafanya katika kuondoa changamoto ziliopo katika kuibua na kutekeleza miradi katika sekta mbali mbali.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, na nashukuru sana kwa majibu yake mazuri Mhe. Waziri, lakini kuna swala (a) na (b) ambalo namuongezea kumuulizia, namuulizia Mhe. Waziri

a) Pamoja na majibu yake kwamba Mikataba inapitiwa na inawekwa katika sehemu ambazo ni salama lakini inatokeaje baada ya Mikataba kufeli hatua gani ambazo zinachukuliwa kwa upande wa wale watendaji wa Serikali ambao ndio wanaisimamia ile Serikali

b) Kwa sababu Mikataba ile inakuwa imesimamiwa kisawa sawa inatokezeaje tokezeaje mpaka ikafeli katika mazingira yaliyokuwa ya utatanishi.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mhe. Suleiman Sarahani Said lenye vifungu (a) na (b) lakini kama nimemuelewa sawa sawa ni swali moja, kwa nini Mikataba inafeli. Kwa sababu swali hili amelizungumza kuijumla sijafahamu hasa ni mkataba gani anao-

refer kama umefeli kwa sababu kwa kumbukumbu nilizonazo Mikataba yote ya Miradi haijafeli inatekelezwa kikamilifu, na Miradi iliyoibuliwa inatekelezwa kikamilifu na inaleta tija kwa nchi na kwa umma sasa kama ana Mradi *Specific* au ana Mkataba maalum ambao anahisi mkataba huo umefeli mimi ningeomba atueleze Mkataba huo.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza namshukuru sana Mhe. Waziri wa Fedha kwa kujibu swali hili kwa umakini na ufanisi, lakini pili napenda kuishukuru Serikali kwa kufanya maendeleo ya nchi yetu kwa wananchi wetu kila uchao. Mhe. Mwenyekiti, swali langu ni kwamba naamini miradi mingi inafanyika lakini utaratibu gani Serikali inatumia katika kufanya *analysis* kabla huo mradi haujafanyika nitatoa mfano, Mhe. Mwenyekiti, barabara ya Jendele - Cheju ime-*cost* karibu billioni mbili. Lakini barabara ya Makaburini Kituoni cha Polisi- Fuoni ime-*cost* karibu *10.9 billion* sasa nataka kujua utaratibu uliotumika na Makaburini Fuoni ni Kilomita sita lakini Jendele- Cheju ni kilomita 11 Mhe. Mwenyekiti naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mhe. Hassan Khamis Hafidh kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, Miradi yote inayoibuliwa, na kwanza miradi mingi inaibuliwa na sekta husika na inawashirikisha wataalamu wa sekta hizo kikamilifu na kwa miradi ambayo inapata mikopo au misaada miradi hiyo haiwekwi saini na Wizara ya Fedha kwa maana ya mkopo *loan agreement* mpaka pale sekta zinapoweka saini *technical agreement* kwa maana ya mkataba wa kiufundi. Sasa tofauti aliyoileza ya gharama ya barabara ya Jendele - Fuoni hii inatokana na mazingira ya barabara hizo kwa sababu gharama

haitokani na ukubwa tu au *distance* ya hiyo barabara lakini pia inatokana na mazingira ya eneo husika.

Kwa hivyo mimi naamini kwamba uchambuzi ulifanywa yakinifu na kutokana na uchambuzi huo, gharama hizo zilikubalika na sekta zinahusika kwa maana ya timu ya wataalam lakini baadaye serikali imeikubali gharama hiyo kutokana na mazingira ya barabara yenyewe. Kwa hivyo si sahihi kutumia kigezo cha masafa ikawa hiyo sasa ndio kigezo cha kusema kwamba barabara hii imejengwa ghali na hii nyengine imejengwa kwa unafuu. Ni mazingira ya barabara husika zipo barabara zinahitaji kifusi kijazwe kwa wingi zaidi lakini kuna mazingira mengine ambayo pengine kuna maji katika eneo hilo, kwa hiyo kunahitajika umakini zaidi katika ujenzi wa barabara kwa hivyo hayo ni mazingira ambayo yanapelekea kuwepo na tofauti ya gharama baina ya barabara na barabara.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza, lakini Mhe. Mwenyekiti nichukuwe fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri na niipongeze Serikali yetu chini ya Dr. Ali Mohamed Shein katika kutekeleza vyema na kusimamia vyema ilani ya Chama cha Mapinduzi katika kuendesha miradi mbali mbali mikubwa na kuleta maendeleo katika nchi yetu.

Lakini kwa kutumia sheria hii ya mwaka 2016 lakini katika majibu yake amesema pamoja na miongozo na kuondoa changamoto na utekelezaji mbovu wa miradi hiyo swali langu ni kwamba:

Je serikali ina kauli gani kwa wale ambao wamekuwa wakitumiya njia mbaya katika kukwamisha miradi mikubwa ya kimaendeo na kutokuwafanyisha wananchi wao kufaidika na miradi hiyo. Je

serikali ina kauli gani kwa wale ambao wanaikwamisha miradi hiyo mikubwa katika kuleta maendeleo katika nchi yetu.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mhe. Nassor Salim Ali kama ifuatavyo:-

Kwanza kama alivyosema, sheria zipo, kanuni zipo, miongozo ipo kuna Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Serikali na Kanuni zake, kuna Sheria ya Fedha na Kanuni zake, na watendaji wote wanapaswa kuzingatia sheria hizo, lakini nilisema hapa kabla ya mradi kutelezwa na kabla ya mkataba haujafungwa mikataba yote inapitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na yote hayo yanafanywa kwa umakini mkubwa ili kuhakikisha kwamba hakutotokea na ubadhilifu wowote lakini vile vile utekelezaji isioridhisha wa miradi.

Sasa kwa wale ambao watakwenda kinyume na sheria hizo basi sheria hizo pia zimeweka jinsi gani watu hao wanatavyoshughulikiwa. Lakini wajibu wetu kama sisi wasimamizi wa shughuli zinazofanywa za serikali na sisi pia ni wajibu wetu wa kuwakumbusha watendaji wetu wanaosimamia miradi hiyo mikubwa kuwa makini katika kuibua lakini pia katika kutekeza miradi na pale wale watakaokwenda kinyume basi hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

Nam. 11

Changamoto Za Mtoto wa Miaka Saba Kubadilishwa Mazingira ya Malezi

Mhe. Suleiman Sarahan Said - Aliuliza:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inastahili pongezi katika jitihada zake za kuwalinda raia na haki zao. Hata hivyo, katika suala la watoto ambao wazazi wao wametengana, baada ya miaka saba sheria humruhusu mtoto huyo achukuliwe na baba na kumpeleka kwa wazazi wa mume au kwa mama wa kambo ambapo watoto wa aina hiyo wengi wao hupata matatizo mengi ya kila aina.

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kubadilisha umri huo kwani wakati huo bado mtoto huwa hajajitambua.

(b) Je, ni kigezo gani kinachotumika kuona umri wa miaka saba ni muafaka kwa mtoto kuwa anajitambua na kwenda katika mazingira mapya.

(c) Kutokana na matatizo hayo ya watoto na umri wa miaka saba kuwa bado mdogo, Je, Serikali inachukua hatua gani kusitisha sheria hiyo mpaka utafiti mwengine ufanyike.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto -Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote kwanza naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema ambae ameweza kutupa pumzi zake na asubuhi hii tukakutana hapa tukiwa wenye afya na hali nzuri. Baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu sasa Mhe. Mwenyekiti kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 11 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, Seriakli kupitia Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto hushugulikia watoto wote kama wanavyotambulika na Sheria bila ya kuangalia

kigezo cha umri walionao kwa wakati huo. Wizara inaposhughulikia masuala ya watoto mara zote huangalia kwanza maslahi bora kwa mtoto husika bila ya kujali umri wake hivyo hoja ya kubadilisha umri haipo kwani Serikali haijaweka kigezo hicho katika miongozo, Sera na Sheria zake.

Aidha, Serikali imeweka misingi hiyo kwa kuzingatia mila na desturi na jamii tulonayo sambamba na mikataba na miongozo ya Kimataifa kuhusiana na haki za watoto ambapo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kama sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeridhia na inatekeleza.

(b) Mhe. Mwenyekiti, naomba kueleza kwamba umri wa miaka saba sio kigezo ambacho Wizara yangu inakitumia katika kuamua masuala yote yanayohusu ustawi pamoja na maslahi bora ya mtoto.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kurejea tena hapa naomba kueleza kwamba umri wa miaka saba sio kigezo ambacho Wizara yangu inakitumia katika kuamua masuala yote yanayohusu ustawi pamoja na maslahi bora ya mtoto nikimaanisha jambo lolote lile ikiwa ni suala la ulezi, matunzo, ukaazi au vyenginevyo. Kama nilivyoeleza hapo awali Wizara kwa kuzingatia misingi iliyowekwa na Sheria hulazimika moja kwa moja kuweka kipaumbele juu ya maslahi bora ya mtoto husika kabla ya kuamua wapi mtoto huyo anaweza kupata stahiki iliyokusudiwa ambayo haitaathiri kwa namna yoyote ile ustawi wake katika maisha yake.

(c) Mhe. Mwenyekiti, Sheria ya Mtoto Namba 6 ya mwaka 2011, haikuweka umri wa miaka saba. Kwa mujibu wa Sheria hiyo, utaratibu uliowekwa katika kushughulikia masuala ya mtoto ni kwa kuzingatia maslahi bora ya mtoto husika na sio kwa kutizama umri wake, hivyo kigezo kinachotumika katika kushughulikia masuala ya watoto kama nilivyoeleza awali Wizara

hushughulikia masuala hayo kwa kuzingatia maslahi bora kwa watoto hao kwa mujibu wa Sheria bila kusahau silka mila na desturi zinazowiana na Sheria zilizopo ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, na mimi nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri pamoja na hayo kauli kubwa sana ambayo iko mitaani au katika familia ni kwamba, kigezo cha baba akitaka mtoto kwa aliyekuwa mke wake au kwa familiya nyengine ambayo inahusiana na mke wake tunazungumzia sana kwamba mpaka afike miaka saba, lakini Waziri hapa ameniambia kwamba miaka saba hakuna sheria hiyo wala sio kigezo. Sasa kauli hii ya miaka saba ambayo maeneo mengine tunakwenda kwenye maeneo ya sheria unaambiwa mpaka afike miaka saba ndio upewe mtoto wako, hii ni kauli tu au inatoka wapi kauli kama hii ambayo mara nyingi inaamuliwa kwamba mtoto afike miaka saba.

b) Ni kwa sababu waziri ana dhamana ya watoto na mambo mengine, kuna watoto wa mitaani wanakuwa hawana huduma, lakini kuna watoto wanakataliwa na baba au mama katika misingi ya kuvutana, hivyo wizara inachukua hatua gani kuwalea watoto hawa.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

a) Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema kwenye jibu langu mama kwamba mtoto anapopatwa na kadhia ile hatuangalii ule umri, bali tunaangalia stahiki nzuri ya mtoto ambapo anaweza kupata matunzo, haijalishi kwamba kuna sheria hayo ni maneno tu. Lakini hakuna sheria inayosema kwamba mtoto akifika miaka

saba achukulie na baba, sisi tunaangalia maslahi ya mtoto wapi anaweza kuyapata ikiwa kwa baba au ikiwa kwa mama.

b) Mhe. Mwenyekiti, kuhusu watoto wanaozurura mitaani anaozungumzia Mhe. Mwakilishi kwamba wanazurura wanakosa mapenzi au malezi ya pande zote mbili, wizara inafanyaje. Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba watoto wale wizara tunawachukua na kuwahifadhi na taratibu za kuwatafuta wazee wao kwa njia moja au nyengine zinafuata na tunapowaona wazee wao basi watoto wale tunahakikisha tunawakabidhi katika mikono ya familia zao. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Bihindi Hamad Khamis: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuweza kumuuliza Mhe. Naibu Waziri maswali mawili ya nyongeza. Kwanza kabisa nianze kumpongeza Mhe. Naibu Waziri kwa kuweza kujibu maswali yake kwa ufasaha na utulivu.

a) Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2017 wizara imepokea kesi ngapi zinazohusu malalamiko na mivutano ya watoto.

b) Katika kesi hizo watoto wangapi walirudishwa kwa mama zao baada ya suluhu.

Mhe. Naibu Waziri Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye (a) na (b).

a) Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Kazi kupitia Idara ya Wazee na Ustawi wa Jamii kupitia Kitengo cha Hifadhi ya Mtoto kimeweza kupokea malalamiko 120, na katika malalamiko hayo 41 yameweza kufanyiwa kazi.

b) Ni watoto 19 ambao waliweza kurudishwa kwa mama zao baada ya suluhu ya kesi hizi kupatikana. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Shaib Said Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza swali moja lenye kifungu (a) na (b).

a) Kwa kuwa kwa sheria hiyo hivi sasa inampa mama uwezo wa kumchukua mtoto huyo, lakini mama huyo huyo au kuna baadhi ya wanawake huwatelekeza watoto hao katika maeneo mbali mbali na tunawaona. Je, wizara yako mpaka hivi sasa ina watoto wangapi waliotelekezwa na wanawake hao kwa Unguja na Pemba.

b) Wanawake hao wanaopatikana ni hatua gani inayochukuliwa ili kuwarudishia watoto hawa. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, kwanza niungane na yeye Mhe. Mwakilishi kwamba ni kweli sasa hivi kumetokea wimbi la akina mama ambao wameshajifungua wanatekeleza watoto wao kwa namna moja au nyengine. Lakini ninachotaka kumwambia kwamba wizara hivi sasa tuna watoto watano ambao wametelekezwa na mama zao, wawili ni kutoka Unguja na watatu kutoka Pemba. Lakini amesema je mama yule anayetelekeza watoto kama nimemfahamu vizuri ni taratibu zipi zinazochukuliwa na kurejeshewa mtoto wake au sio.

Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto inapopata kesi kama ile kwamba kwanza inaanza kufatilia utaratibu kwa kesi ile, na tukishaigundua basi kwanza kesi ile inapelekwa kwenye vyombo vya sheria ikiwa hapa pana polisi na Mahakama.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba nieleze kwa ufupi kwanza tunaambiwa kuna sheria inayomgusa mama anapojifungua, kuanzia siku moja mpaka mwaka mmoja hawezi kushtakiwa kwa kosa hilo kwamba ametelekeza mtoto kwa sababu anasema akili yake haiko vizuri. Lakini nichukue nafasi hii kuwaomba Waheshimiwa Wawakilishi hivi sasa tumo katika kurekebisha sheria mbali mbali, basi na hii naomba sana tuitupie macho ili tuweze kuwachukulia hatua na adhabu wale kina mama ambao wanatelekeza watoto wao baada ya kujifungua, kwani wimbi hili hapa Zanzibar sasa hivi limekuwa linaongezeka siku hadi siku.

Mhe. Mwenyekiti, lakini ametaka kujua Mhe. Mwakilishi kwamba mtoto yule ikisha anarudishwa vipi kwa mama yake. Naomba kwanza nimueleze Mhe. Mwakilishi kwamba baada ya taratibu za sheria hizi nilizozitaja awali mtoto yule kwanza tunakaa nae katika nyumba yetu ya kuhifadhia watoto Mazizini na huku utaratibu wa sheria ukiendelea. Ikiwa mama yule anaonekana anastahiki kupewa mtoto wake basi hatuna kipingamizi cha kumpa mtoto wake, na akiona hana sifa ya kupewa mtoto basi serikali haiko tayari kumrudishia mtoto yule na tunakaa nae sisi katika nyumba yetu ya Mazizini. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Nam. 12

Skuli Binafsi Kutopatiwa Misaada Kutoka Serikalini

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Aliuliza:

Serikali inastahiki pongezi kwa kuhakikisha watoto wanasoma bila ya malipo kwa lengo la kusoma na kufikia kidato cha nne. Pamoja na mipango mizuri ya serikali, idadi ya watoto ni kubwa na hii inawapa fursa watu binafsi kufungua skuli na kuipunguzia mzigo serikali.

(a) Je, kwa vile wanafunzi wa skuli za serikali na skuli za binafsi ni watoto wetu, wizara inawafikiaje watoto wanaosoma katika skuli binafsi wakati wanapopata misaada inayoletwa serikalini.

(b) Kwa vile watoto wanaosoma katika skuli za watu binafsi nao pia huwa wanastahiki kupewa misaada, serikali haioni kwamba watoto hao kutokupewa misaada hiyo kunawanyima haki yao kama watoto wengine.

(c) Kwa vile watoto wanaosomeshwa skuli za watu binafsi wanapomaliza wanaitumikia serikali hii, kutokuwapa vile vinavyoletwa kwa watoto wote si mnawatia unyonge watoto wetu kwa kujiona wanabaguliwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 12 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Kwanza napenda katoa maelezo ya utangalizi. Napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru na kuwapongeza wamiliki wa skuli za binafsi na skuli za jamii kwa mchango mkubwa wanaotoa katika kuongeza upatikanaji wa nafasi za kusomea na kuchangia katika kuinua kiwango cha elimu. Pia, napenda kuchukua fursa hii kuwahakikishia Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kuwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ina mashirikiano na

wamiliki wa skuli binafsi na skuli za jamii. Wizara inawaalika wamiliki wa skuli binafsi katika vikao mikutano ya walimu wakuu, walimu na kamati za skuli ili kuweza kuchangia mawazo na ushauri katika kuimarisha elimu yetu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli kuwa wizara inapokea misaada katoka kwa wahisani wa ndani na nje ya nchi kwa lengo la kuimarisha maendeleo ya elimu yetu. Baadhi ya misaada hiyo inakusudiwa kwa matumizi ya wanafunzi na walimu wa skuli za serikai tu na baadhi inakuwa kwa skuli zote. Misaada hiyo inapogaiwa inafuata mahitaji yaliyokusudiwa.

(b) Wizara inazipatia skuli za binafsi baadhi ya misaada kutegemea na lengo la msaada huo lilivyokusidiwa. Baadhi ya misaada iliyotolewa kwa skuli binafsi na skuli za jamii ni kama hii ifuatavyo:-

- Katika mwaka 2014/2015 skuli 11 za maandalizi za jamii zimefungiwa pembea za watoto wadogo. Skuli hizo ni Skuli za Bweleo, Chwaka, Mangapwani, Mombasa, Unguja Ukuu na Donge Mtambile kwa Unguja. Kwa upande wa Pemba ni Alsadik, Jeshini, Istiqama Konde, Istiqama Mkanjuni na Istiqama Mkoani.

- Skuli za binafsi pia hupewa msaada wa nakala tano tano za vitabu kwa kila somo, mihutasari na miongozo mbali mbali ikiwa ni mchango wa serikali katika kukuza taaluma katika skuli hizo. Walimu wa skuli za binafsi pia hushirikishwa katika mafunzo kupitia baadhi ya miradi kama vile mafunzo ya ukusanyaji wa takwimu, mitaala na viwango vya kujifunzia.

- Skuli za binafsi pia huruhusiwa kujiunga na Vituo vya Ualimu na kufaidika na mafunzo mbali mbali yanayoendeshwa kwa walimu kupitia vituo hivyo. Jumla ya skuli 33 za binafsi, Unguja (29) na Pemba (4) ni wanachama wa Vituo vya Ualimu.

- Kampuni ya "CHARA" hutoa misaada ya viatu kwa wanafunzi wa skuli za msingi za serikali na baadhi ya wanafunzi wa skuli za binafsi.

- Skuli za binafsi zinashirikishwa kikamilifu katika shughuli zote za kitaifa zikiwemo mashidano ya michezo ya Tamasha la Elimu Bila ya Malipo.

(c) Wanafunzi wa skuli binafsi hawabaguliwi na baadhi yao wanaruhusiwa kujiunga na skuli za serikali pindipo wazazi wao wanaposhindwa kuwalipia ada. Pia, ieleweke kuwa skuli za serikali ndio skuli zenye idadi kubwa ya wanafunzi na mahitaji makubwa ya vifaa na nyenzo mbali mbali za kufundishia ukilinganisha na skuli za binafsi ambazo baadhi yake zina idadi ndogo ya wanafunzi. Ahsante.

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii kuuliza swali la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

a) Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2016/2017 ni skuli ngapi za binafsi mlizozipatia msaada kwa upande wa Unguja na Pemba.

b) Mhe. Naibu Waziri kutokana na ongezeko kubwa la idadi ya wanafunzi waliofaulu hapa Zanzibar ni sababu zipi zilizopelekea serikali kushindwa kutotangaza matokeo ya wanafunzi waliofaulu katika skuli binafsi kwani na wao ni sehemu ya taifa hili.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye (a) na (b) kama hivi ifuatavy:-

a) Ni kwamba tumesema hii misaada iko katika sura nyingi. Kuna sura ya kupatia vitabu, kuna sura ya ukaguzi, kuna sura ya kupitia mafunzo ya vituo vya ualimu. Sasa misaada ya namna hii ni misaada endelevu na inaendelea kila mwaka kupitia vituo vya walimu.

b) Ni kwamba matokeo ya mtihani ya kitaifa ya kidato cha pili na *standard four*, haya yote yanatangazwa siku hizi kupitia kwenye mitandao, ukipitia kwenye mitandao utaona matokeo ya kila skuli. Ahsante.

c)

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa na mimi nafasi ya kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza. Lakini kwanza nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake fasaha ya swali mama la Mhe. Mwanaidi. Mhe. Mwenyekiti, swali langu liko katika kifungu (a) na (b)

a) Mhe. Naibu Waziri amekiri kwamba skuli binafsi wanazipatia nakla za vitabu vya kufundishia na kujifunzia kwa kila skuli nakla tano tano. Lakini kutokana na uhaba huo baadhi ya skuli hulazimika kutoa *photocopy* vitabu hivyo hususan vya wanafunzi hali ambayo inaondosha uhalisia na hususan kwa watoto wa madarasa ya chini. Je, Mhe. Naibu Waziri ni lini wizara inafikiria kuweza kuwaongezea nakla skuli hizi binafsi ambazo zinafanya mitihani ya taifa ili na wao wanafunzi waweze kuneemeka na matunda ya elimu Zanzibar.

b) Kama vile wizara haiwezi kukidhi kutoa kopi za kutosha, basi ni lini itaweza sasa kuwaruhusu skuli za binafsi kuweza

kununua kopi hizo kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ili wanafunzi wanaosoma katika skuli hizo waneemeke. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali tayari tumeshazungumza na wamiliki na walimu wa skuli binafsi kwamba itatoa nakala za vitabu wenyewe ili wachapishe kwa ajili ya matumizi ya skuli zao, tumeshazungumza nao na tumeshakaa nao. Sasa ni wao wenyewe kuamua lini watakuja wizara tuwapatie ili wachapishe, lakini kutoa *photocopy* hiyo hairuhusiki.

Kuhusu suala la pili, ninafikiri lishajibika kwa pamoja kwamba tayari tumeshawaruhusu kuja wizarani kuwapa kopi kwa ajili ya kwenda kwa mchapishaji kuchapisha vitabu kiasi wanavyotaka wenyewe. Ahsante.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa fursa hii niweze kuuliza swali la nyongeza lenye (a) na (b). Pia nimpongeze kwa majibu yake mwanana ambayo ameyatoa kwa wajumbe.

a) Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa skuli za watu binafsi unakiri kwamba zinasaidia sana mzigo wa serikali katika kuwapatia haki ya elimu watoto wetu nchini. Je, serikali inatambua kuwa baadhi ya skuli binafsi kama vile *Al-Haramain Internation* wameanza mtindo wa kuwachunja wanafunzi wao ambao wale mahodari sana wanafanya mitihani katika ile ile na wale ambao wamepungukiwa na sifa kidogo wameanza kuwapangia skuli

nyengine kufanya mitihani hiyo, kitu ambacho kinaleta usumbufu kwa wazee na watoto hao.

b) Je, serikali kama haitambui ina mpango gani wa kulichunguza hili na kulikemia kuona kwamba mtindo huo hauwezi kuendelea, kwani watoto hao wameanza tokea skuli ya maandalizi na leo kuwaondoa hapo. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba tayari Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imeshatoa kauli rasmi kwamba ni mitihani ya taifa inayofanywa na Serikali ya Zanzibar ndio iwe kigezo cha kuwachuja wanafunzi, si mtihani mwengine wowote. Kauli hii tayari tumeshaitoa kama kuna skuli inafanya hivyo basi tutaichukulia hatua mara moja, hiyo ni kauli ambayo imetolewa rasmi na Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali. Ahsante sana.

Nam. 3

Ada ya Maji Serikalini kwa Wanaochimba Visima Ndani ya Nyumba Zao

Mhe. Tatu Mohamed Ussi - Aliuliza:

Kwa kuwa siku hizi wananchi wengi wanaojenga nyumba wanachimba visima ndani ya nyumba hizo kwa ajili ya kujipunguzia tatizo la maji.

(a) Je, wizara inalijua hilo na kama inajua wananchi hao wanaochimba visima hivyo hawapaswi kulipa ada ya maji serikalini.

(b) Je, wizara ina mpango gani wa kuwapitia wananchi hao ili kuwapa elimu ya kuchimba visima hivyo kwa kuepuka kuchimba karibu na mashimo ya vyoo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 3 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji inafahamu uwepo wa wimbi kubwa la uchimbaji visima binafsi na inaendelea na zoezi la utambuzi wa visima binafsi, wananchi wanaomiliki visima hivyo wanatakiwa kuvisajili visima hivyo na kulipa ada ya TZS. 50,000 kwa mwaka.

(b) Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka ya Maji inaendelea na utoaji wa taaluma kwa wananchi kupitia vyombo vya habari, mikutano ya wananchi na matangazo juu ya usajili. Vile vile kuwataka wananchi wenye visima binafsi kuja Mamlaka ya Maji kupatiwa dawa ya kutibu maji pamoja na kutoa ushauri na maelekezo kwa visima vinavyotaka kuchimbwa au vilivyochimbwa kinyume cha utaratibu ili kuepuka kuchimba visima katika maeneo ambayo hayako salama. Ahsante sana.

Mhe. Tatu Mohammed Ussi: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, namshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri naomba nimuulize swali dogo la nyongeza lenye kipengele (a) na (b).

a) Ni visima vingapi ambavyo vimesajiliwa hadi Januari, 2018.

b) Je, wizara yake inajua kwamba visima hivyo vinavyochimbwa majumbani ndivyo vinavyosaidia jamii kwa kiwango kikubwa, wizara yake ina mpango gani wa kusaidia visima hivyo katika kusafishwa. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye vipengele (a) na (b). Nikianza na (b) ni kwamba:

(b) Wizara inafahamu visima hivi vina msaada mkubwa kwa jamii na ndio maana wakati mwengine hata kama taratibu ilikosekana tunakuwa tunavivumilia kwa ajili ya msaada huu. Lakini vyenginevyo, kama ingekuwa tayari tumetengamaa kiupatikanaji wa maji kama tulivyokuwa tunatamani Unguja na Pemba visima vyengine vingekuwa tayari tumevifunga. Kwa hiyo, tunavithamini sana, tunajua mchango wake. Lakini visima ambavyo vimesajiliwa tulivyonavyo ni 1,325. Ahsante sana.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: *Bismillahi Rahmani Rahiim*. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa ruhusa kumuuliza swali la nyongeza Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji Nishati na Mazingira Swali langu ni kwamba, kwa kuwa siku nyingi jimboni kwangu Chaani, Kandwi mashine ya maji imeharibika na wananchi wangu wameshaanza kupatwa na maradhi ya kuharisha. Ni lini wizara yake itaweza kwenda kupeleka mashine ile ili kuondosha usumbufu wa maji kuanzia wananchi mpaka mahotelini.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Wizara inafahamu kwamba *pump* pale imeharibika na tupo katika jitihada

ya kutafuta nyengine, lakini kama yupo tayari kushikana mkono na wizara basi tunamkaribisha kusudi kuharakisha upatikanaji wa *pump* hiyo. Ahsante sana.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipatia na mimi nafasi kuuliza swali dogo la nyongeza lenye kifungu (a) na (b). Kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa majibu yake lakini ningependa nimuulize swali dogo tu.

Mhe. Naibu Waziri kwa vile tunafahamu mtu anapotaka kuchimba kisima sio wengi wanaofuata hizo taratibu za kuja wizarani na kujua hapa pangu pako salama au hapako salama.

(a) Je, kama wizara huwa wanachukua jitihada gani ndani ya mashehia kuweka hawa wataalamu ambao wanahusika na suala hili ili suala la uchimbaji wa visima vilivyo salama lizingatiwe zaidi na kutokufuata yale maelekezo ambayo sio na kuchimba visima visivyo salama.

(b) Je, hizi dawa ambazo wizara inatoa mpaka mtu anapokuja huko wizarani hawaoni kwamba kuna haja ya kuweka hizi dawa ndani ya mashehia au wilaya, ili ziweze kupatikana kila baada ya muda kwa kutumia ndani ya visima hivi ambavyo vinatumika.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:

Jitihada ambazo tunafanya ya kwanza kila wilaya kuna maafisa toshelezi wa mamlaka ya maji, kusudi kupeleka huduma karibu kwa jamii. Kama itakuwa bado ni tatizo niombe sasa wananchi ambao wanataka kuchimba kisima waende kwa sheha na sheha atawaelekeza hapo wilaya husika.

Kwenye suala la dawa, ni vyema kwanza visima vyote tukavisajili, kusudi kama hajaja sisi tunaweza tukashirikiana na masheha tukajua kisima gani bado hakijachukuliwa dawa zake kuliko kuvipeleka kule. Kwa sababu unaweza ukaziweka kule zikatumika vyengine tofauti na ilivyokusudiwa kwa ajili ya kuhimiza. Dawa ni dawa, ni vyema dawa inapochukuliwa ikatumika katika eneo husika. Ushauri wake ni mzuri na tutajaribu zaidi kuangalia namna gani tutafikia hilo lengo alilolikusudia. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Ali Suleiman Ali kwa swali la nyongeza la upendeleo. (*Makofi*)

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa imani kubwa uliyonipa hasa tukizingatia kwamba tatizo la maji katika nchi yetu ndio kilio kikubwa.

Mhe. Mwenyekiti, katika swali mama lililoulizwa jinsi ya visima mbali mbali vinavyochimbwa vya wananchi ndani ya majumba yao pamoja na nje, ambapo wananchi wengi wamejitolea kuchimba visima hivyo kutokana na adha kubwa tunayopata katika nchi yetu ya ukosefu wa maji. Swali langu liko hapa.

Kwa kuwa serikali tuliahidiwa kuna bilioni 200 au dola 92 milioni hadi leo kimya mwaka wa pili huu. Je, serikali inatoa tamko gani juu ya suala hilo. Fedha hizo zipo au hazipo, ili wananchi wetu waelewe kwamba suala hilo limeshindikana na sisi tujitayarishe kwa vyengine.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Ule ni mkopo na tunaendelea na taratibu za kuutekeleza. Lakini kwa kufahamu

tatizo la maji tulilonalo hatukuutegemea mradi ule tu au mkopo ule, tunatekeleza na miradi mengine lakini kwa ufupi niseme ule ni mkopo na tunaendelea na utaratibu. Ahsante sana.

Nam. 57

Kupatikana Mashine za Kilimo za Bei Nafuu

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza:

Kwa kuwa hivi karibuni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imetoa fedha kwa ajili ya ununuzi wa matrekta mapya 20, kwa ajili ya kuendeleza azma yake kwa wananchi kuweza kuzalisha zaidi na kujitosheleza kwa chakula, na kwa sababu yapo mabonde ya mpunga ambayo hayawezi kulimwa kwa trekta kutokana na kutokuwepo kwa miundombinu mizuri ya barabara za kuyafikia mabonde hayo, jambo ambalo linasababishwa na hali halisi ya jiografia iliyosimama na mabonde yenye mavuli ambayo hayakauki maji kwa muda wote, jambo ambalo linaweza kusababisha trekta kuzama ardhini. Lakini zipo mashine za kilimo za bei nafuu ambazo hutumika kwa kutayarishia shamba za mpunga kupandia, kuchimbia mashimo ya migomba na kadhalika ambazo hupatikana kwa bei nafuu na kuwakopesha wakulima.

(a) Je, serikali ina mpango gani wa kununua mashine za kilimo za bei nafuu ambazo hutumika kwa kutayarishia shamba la mpunga, kupandia, kuchimba mashimo ya migomba na kadhalika, ambazo hupatikana kwa bei nafuu na kuwakopesha wakulima.

(b) Je, wizara ina mpango wa makusudi wa kuwataka na kuwapatia wakulima wetu wote mbegu ya mpunga iliyotolewa na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi ambayo kwa mwaka wa kilimo uliopita ulitoa mpunga mwingi zaidi kuliko zile za asili.

(c) Je, thamani ya mashine hizo za kupandia, kupalilia na kuvunia mpunga na mahindi hapa kwetu zimeshaanza kutumiwa na wakulima wetu na bei yake ni kiasi gani na zimepatikana wapi.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 57 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi imekuwa ikishajihisha wakulima utumiaji wa mashine ndogo ndogo za kilimo hasa *"power tillers"* kwenye mabonde ya mpunga ambayo hayawezi kulimwa kwa trekta, kutokana na kutokuwepo kwa miundombinu ya barabara za kuyafikia mabonde hayo. Hata hivyo, mnamo mwaka 2012, serikali imegawa jumla ya *"power tillers"* 50 kwa Jumuiya za Wakulima. Aidha, watu binafsi wamekuwa wakiviagiza vifaa hivyo na wanaendelea kuvitumia kwa Unguja na Pemba. Kwa muda huu Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo inafanya utafiti wa upatikanaji wa mashine ndogo ndogo ambazo zitaweza kutumika kwenye maeneo hayo.

(b) Mhe. Mwenyekiti, katika msimu wa kilimo cha mpunga, Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi imeshanunua tani 350 za mbegu ya mpunga. Mbegu hizo zilizonunuliwa ni za aina ile ile iliyonunuliwa na kusambazwa msimu uliopita ambazo ni: *“Super India”, “TXD”* "88" na *“SARO”.* Mbegu hizi zimegawiwa kusambazwa kwa wakulima wote wa mpunga. Kazi ya usambazaji kwa wakulima hao ambao tayari wameshatayarisha konde zao kwa ajili ya upandaji imeshaanza.

(c) Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwajulisha Waheshimiwa Wajumbe kwamba, kwa muda huu Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo inafanya utafiti wa upatikanaji wa mashine ndogo ndogo za kupandia, kupalilia na kuvunia mpunga na mahindi, ukiondoa *"power tillers"* ambazo bei yake ni TZS. 5,000,000 - 6,000,000. Taarifa juu ya mashine nyengine zitatolewa baada ya utafiti kukamilika.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri lakini nina maswali lenye kipengele (a) na (b) ambalo nataka kuuliza.

(a) Kwa kuwa wizara inaendelea na utafiti na msimu wa kilimo umeshafika, sasa ningependa nijue tu kwa maslahi yangu na wakulima wenzangu. Je, ni lini utafiti huu ulianza na lini utakamilika ili wakulima wetu ambao wana uwezo wa hapa ambao hawajui huko nje zinakopatikana wakaweza kupata taarifa ya upatikanaji wake wakaweza kuzinunua na kuzitumia na kuzalisha mazao mengi zaidi wakapata maslahi wakaongeza kipato chao.

(b) Je, wizara haioni kwamba kuna tatizo la ufuatiliaji ukitilia maanani kwamba watu binafsi wameshaanza kuzigundua na wameshaanza kuzileta. Lakini wizara mpaka leo bado wanaendelea na utafiti. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mheshimiwa swali lake la nyongeza lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:

(a) Utafiti huu ulianza mwishoni mwa mwaka 2017 na tunaendelea nao na utakapokamilika ndipo tutakapotoa taarifa

kamili kwa wananchi mashine hizi zitapatikana wapi na wataweza kuzinunua wapi. Mashine hizi tunategemea tutakapowakilisha katika kampuni hii utafiti wetu basi hawa wakulima wote watakuja katika Wizara ya Kilimo, Maliasili Mifugo na Uvuvi na hawatokuwa wakisafiri kwenda kuzinunua nje ya nchi. Vile vile kama kuna watu ambao wana uwezo wa kwenda kununua nje ya nchi, basi pia na wao wanaruhusiwa wanaweza kwenda kununua nje ya nchi.

(b) Tatizo la ufuatiliaji si tatizo hili, kwa sababu tunafuatilia ili tuwaletee wananchi wetu vifaa bora na vifaa ambavyo vitakuwa vinakaa kwa muda mrefu, hatutaki kuja kukaribisha malalamiko kwa siku za mbele baadae na wakasema kwamba tumeleta vifaa ambavyo si sahihi. Nashukuru sana.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii kumuuliza swali la nyongeza Mhe. Naibu Waziri kama ifuatavyo. Katika uvunaji wa mpunga kwa msimu uliopita Mhe. Waziri wa Kilimo alikwenda mabonde ya Mwachealale na akazindua uvunaji wa mpunga kwa kikundi cha ushirika cha watu wa Mwachealale. Bahati nzuri walipata mpunga mwingi na waziri alifurahi sana. Lakini Mhe. Waziri aliahidi kununua mbegu, lakini hadi leo hakwenda tena kununua mbegu hizo.

(a) Je, anawaambia nini wananchi wale wa Mwachealale ambao wameingia hasara kutokana na waziri kutotekeleza ahadi yake.

(b) Wananchi wa Bumbwisudi eneo la Kirununda wana eneo la umwagiliaji na limekubaliwa na serikali kuwa skuli za umwagiliani. Lakini tatizo lililokuwepo ni kwamba serikali hiyo

hiyo kupitia Wizara ya Kilimo imetoa kazi za uchimbaji wa mitaro katika eneo lile kwamtu kutoka nje ya eneo lile. Je,

waziri haoni kwamba hakuwatendea haki wananchi wa Bumbwisudi hasa wa eneo la Kirununda kwamba kazi ile wanaiweza na wangelipewa ingelikuwa kazi nzuri zaidi.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo. Mhe. Mwenyekiti, kikundi cha Mwachealale kuhusiana na mbegu zao kuwa hazikununuliwa siwezi kujua mimi sijakuwepo, lakini niseme labda wangewasiliana na wanunuaji wa mbegu halafu baadae tukajua nini kinaendelea.

Swali lake la (b), labda nimwambie Mhe. Mwakilishi hao watu aliosema ambao hawakutendewa haki katika kuchimba huu mtaro. Je, waliomba? Kwa sababu huwezi ukapewa kazi tu bila ya kuandika barua ama kuomba katika suala hili. Vile vile tunapopenda kuwapa kazi kwa wananchi wetu tunaangalia wananchi kwanza kabla ya kumpa mtu wa nje. Sasa labda nimwambie Mhe. Mwakilishi ikiwa wananchi wake wako tayari kwa kazi hizi basi wao watangulize maombi kabla. Ahsante sana.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipatia na mimi nafasi kuweza kuulisa swali dogo la nyongeza lenye kipengele (a) na (b). Kwanza nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri kwa ufuatiliaji wake mzuri na kuwaimarisha wakulima wetu na kilimo katika nchi yetu pia.

(a) Mhe. Naibu Waziri ametwambia katika jibu lake mama kwamba kuna hizi *power tillers* 50 ambazo zimetolewa kwa jumuiya za wakulima. Sasa tungependa tufahamu hizi jumuiya wa wakulima ambazo zimepewa *power tillers* ni zipi.

(b) Je, kama wizara tayari imeshatoa *power tillers* 50 kuna taratibu gani za ufuatiliaji wa hizo *power tillers* ambazo

zimeshatolewa kwa hizo jumuiya ili ziendelee kufanya kazi na kufanya mzunguko kwa wakulima wengine ndani ya mashamba yetu. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye kipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:

(a) Mhe. Mwakilishi nimuombe kwamba jumuiya hizi nimletee kwa maandishi ili niwe nazo zote kwa ujumla na niwe na uhakika wa jibu hili.

(b) Utaratibu wa ufuatiliaji unaendelea lakini niseme kwamba, baada ya kuwapa vikundi hivi sasa hivi kutoka mwaka 2012 mpaka sasa hivi hizi zilikuwa ni jukumu lao na zilikuwa ni katika mikono yao. Kwa hivyo, kuna wengine ambao tayari zimeshalala na kuna nyengine bado zinaendelea kufanya kazi. Nashukuru.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kuhusu utaratibu.

Mhe. Mwenyekiti: Nimekuona kuhusu utaratibu lakini mimi nimeshasimama. Waheshimiwa Wajumbe maswali yetu yalioko katika *order paper* yetu ya leo yamemalizika, lakini kabla sijampisha Naibu Spika naomba nitoe matangazo mawili.

Tangazo la kwanza Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii (Mhe. Ali Suleiman Ali) anawatangazia Wajumbe wa Kamati hiyo wakutane katika kikao kifupi hapo chumba Nam. 2.

La pili, kuhusiana na wageni wetu wa leo. Wageni hawa ni wageni wa Mhe. Nassor Salim Ali, Mwakilishi wa Jimbo la Kikwajuni, jumla yao ni 20. Hawa ni viongozi na wachezaji wa

Timu ya Taifa ya Mchezo wa Nage Zanzibar. Timu hii imechukua ubingwa katika mashindano ya sherehe za miaka 21 ya kuzaliwa kwa CCM jijini Dar es Salaam hivi karibuni. Wageni hao wanaongozwa na Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Mjini Ndugu Talib Ali Talib, naomba wote kwa pamoja tusimame wakiongozwa na Mwenyekiti. Karibuni sana. *(Makofi)*

Viongozi wengine Ndugu Haji Sultani Pembe, Rais wa Mchezo wa Nage Zanzibar; Ndugu Mbarouk Abdalla Hanga, Diwani wa Rahaleo; Ndugu Ibrahim Khamis Fataki Diwani wa Kikwajuni, Ndugu Machano Ali Machano, Diwani wa Kuteuliwa. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wajumbe timu hii ya nage inaundwa na wachezaji kutoka Miembeni, Mwera, Welezo na Chumbuni. Ahsanteni sana karibuni. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mhe. Jaku Hashim Ayoub wa Jimbo la Paje. Wageni wenyewe ni Ndugu Haji Khatib Haji kutoka Daraja Bovu, Ndugu Rehema Makame Hamad kutoka Daraja Bovu na Ndugu Khamis Muhidin Khamis kutoka Umoja wa Watu wenye Ulemavu Zanzibar. Karibuni sana.

Sasa naomba nimpishe Mhe. Naibu Spika ili aendelee na shughuli zinazofuata.

(Hapa Mhe. Naibu Spika, alikalia kiti)

Utaratibu

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi nikushukuru nimesimama kwenye kanuni ya 42. Sijui kama utaniruhusu niisome au itakuwa imetosha.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Jaku Hashim Ayoub naomba urudie unachokizungumza.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, nimesimama katika kanuni ya 42(3)

Mhe. Naibu Spika: Naam endelea.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Niisome!

Mhe. Naibu Spika: Inatosha kuitaja hiyo kanuni endelea na hoja yako.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, kumetokea jambo la dharura na nimeomba Baraza tulijadili. Kuna mtoto katika wageni wangu waliokuja anaitwa Khatib Haji Khatib aliepekekwa alipelekwa katika Hospitali ya Rufaa ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Naibu Spika: Sawa nimekuelewa kaa kwanza kuna hoja nyengine imetoka. Halafu nitatoa maamuzi. Mhe. Nadir Abdul-Latif Yussuf.

Mhe. Nadir Abdul- Latif Yussuf Al-Wardy: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi nitainuka na hiyo hiyo kanuni ya 42 ili jambo la dharua lijadiliwe kuhusiana na Profesa Kabudi. Niendelee Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Spika: Hapana usiendelee kaa kwanza. Tunaanza na hoja ya mwazo ya Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Waheshimiwa Wajumbe Kanuni yetu inatwambiwa kwamba hoja ambayo inaweza kuletwa kwa siku moja ni hoja moja ya dharura. Lakini kwa nafasi yangu naweza kutoa hoja mbili ambazo kwa kuwa tunaweza kuzigawa tutakuwa tuna saa moja tu ya hoja za dharura.

Kwa hiyo, kila hoja itatumia nusu saa. Kwa hiyo, naanza na Mhe. Jaku Hashim Ayoub ambaye atazungumza hoja yake na kwa kuna Waheshimiwa Wajumbe ambao watachangia katika hoja hiyo kama muda utaruhusu basi Wajumbe naweza kuwapa dakika zisizozidi dakika kumi. Mhe. Jaku Hashim Ayoub.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, nikushukuru kwa dhati kabisa kutoka ndani ya sakafu ya moyo wangu. Mhe. Naibu Spika, kipindi kilichopita nilikaa kimya kikao kizima na hichi nilikusudia hivyo hivyo. Lakini kuna mambo itakuwa ni "*masuula*" kwa mbele ya haki kwa Mwenyezi Mungu na nitoe hadithi tu inayosema.

"Manran Minkum Mathlan faliyakhiruh biyadihi famansyastatuyn falisabihi wamanyalstatihu tabiiyn wadhalika bikalbih"

Hadithi hii Mhe. Naibu Spika, ukaona jambo ovu utumie ulimi wako wa pili mkono wako, la tatu ni imani dhaifu ulichukue. Kuna kitendo ambacho kimetokea Hospitali ya Mnanzi Mmoja ambayo ni Hospital ya Rufaa kwa mtoto Hatib Haji Hatibu alikwenda na mtoto wenyewe mlemavu, alikwenda hospitali kwenda matibabu mzizi wake ukawa hauonekani akafungwa mpira kama huu hapa huu.

Nafikiri kama sikosei niujaribu kuufunga hapa basi nitapata habari na kakaa nao kama siku mbili au tatu, mtoto analia machozi yanamtoka na mama yake nafikiri itakuwa elimu yake ndogo kama mimi yeye akaona ndio dawa, mtoto analia machozi yanamtoka. Mama mtu akenda kwa jirani yake akamhadithia akamwambia nenda hospitali haraka kufika hiospitali yule mama akagombwa sana na daktari huo si uzembe. "Sasa ng'ombe wa mbele hataki kwenda unampiga ng'ombe wa nyuma?" .

Uzembe waliofanya hospitali mkono umevimba umeoza damu hatimae ikabidi waitwe watu ule mkono ukatwe mtoto huyu hapa huu ni uzembe huu mpira tuangalie siku tatu,nne ukafungwa huu hapa wa *drip,* mtoto miaka mitatu na nusu ambaye anaitwa Khatib Haji Khatib mtoto wenyewe ni mlemavu na hili si la kwanza si la pili si la tatu *wallah* inatia huruma kabisa kabisa tumepiga kelele mpaka tunachoka *yailah*. Huu ni unyonge na imani dhaifu kabisa.

Kenda mtu kutafuta matibabu leo anampata haya tunalia kwa uchungu, leo Dr. Ali Mohammed Shein kazi yote anayoifanya katika Hospitali ya Mnazi Mmoja ni haki kweli hii. Kweli tunamsaidia Mhe. Rais, leo mtu mlemavu anaengezwa ulemavu *"Inna llillah waina ilayh rajiun"*.

Mtoto nikikuonesha utalia yoyote atalia, miaka mitatu na nusu mtoto wenyewe ni mlemavu wa miguu leo anaongezwa ulemavu, kuna mmoja akaonesha jino jengine anangolewa jino jengine. Rais jitihada zote alizozifanya hatuzioni kweli sisi *"Inna llillah waina ilayhi rajiun"*. Leo mtoto familia yake watamlea saa ngapi yule haifai mambo mengine *yakhe* jitihada zote anazochukuwa Mhe. Rais hatuzioni kweli kila wanapolalamika Wizara ya Fedha wanaongezwa bajeti.

Mhe. Naibu Spika, kama itawezekana bora nisome mapendekezo yangu kwa Serikali lakini naiomba serikali kuzingatia:-

(1) Baraza hili likanye na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kufanya uhakiki wa taarifa wafanyakazi wote wa Hospitali ya Mnazi Mmoja kuangalia kama watendaji hao wana sifa za kitaalamu kufanya kazi wanazozifanya.

(2) Serikali mbali na Taasisi za Kisheria kuhusiana na nidhamu zilizimo katika sheria mbali mbali iandae kanuni maalum kwa ajili ya madaktari kuchukua hatua za kinidhamu kwa

madaktari hao. Serikali iwachukulie hatua za kisheria zinazofaa kwa uzembe huo.

(3) Serikali ifikirie kulipa fidia kwa familia hiyo na mtoto huyo kupata elimu.

(4) Iwe fundisho jambo hili lisitokezee tena au na mambo mengine yanayofanana na kama haya.

Mhe. Naibu Spika, jitihada zote mimi nasikitika na Mhe. Rais anavyochukuwa jitihada nasema mimi hata saa tisa za usiku nikiamshwa kama sikumshukuru Mhe. Rais Dr. Shein nitapata dhambi hakika, unalomwambia Rais yule msikivu, saa tisa za usiku ndio usingizi mkali nikaamshwa, Mhe. Ali Hassan Mwinyi anasema kila kitabu na zama zake, kama kuna kitabu cha Mhe. Dr. Ali Mohammed Shein ni hichi cha Wizara ya Afya jitihada anazochukua.

Leo tuangalie Hospitali iliyojengwa Mkoani kule milioni kumi na sita dola, leo *CT Scan* hakuna duniani kote nafikiri ya ukapate bure leo kipimo hichi cha laki mbili na nusu kinafanyika bure. Sasa jitihada gani, maneno yake alisema kama sikosei.

Mhe. Rais, kaunda wizara ili iwasaidie wananchi na sio yeye Mhe. Rais katika majumuisho aliyoyafanya siku ya tarehe 17 katika majumuisho ya Mkoa wa Kusini, Mhe. Haji Omar Kheir alikuwa shahidi kaunda wizara ili ziwasaidie wananchi sio maneno yangu haya namnukuu Mhe. Rais katika majumuisho yake, uzalendo ni muhimu.

Siku hizi mtu anataka apate yeye nyumba tano, wananchi wa Kitogani walitoa nyumba tano pale fidia lakini kiongozi anataka kumiliki nyumba tano sasa hivi haya si maneno yangu namnukuu

Mhe. Rais. Kaunda wizara zisaidie wananchi, leo mawaziri ndio tunawasaidia wananchi kweli hivi.

Mhe. Naibu Spika, naomba hoja hii ijadiliwe hivi sasa ili wananchi wapate kusikia. Natoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Jaku Hashim Ayoub tunakushukuru kwa hoja yako na imeungwa mkono na Wajumbe wengi wa Baraza. Kwa hiyo, sasa tutaanza kuchangia na mchangiaji wetu wa mwanzo atakuwa ni Mhe. Hassan Khamis Hafidh. Mhe. Hassan Khamis Hafidh hukuniambia unataka kuchangia nini? Mheshimiwa isizidi zaidi ya dakika kumi. Samahani nimeambiwa kuwa ni dakika tano.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Naibu Spika, kwanza napenda sana kuchukua fursa hii ya kukushukuru wewe kwa kunipa fursa hii ya kuchangia hoja madhubuti muhimu iliyowasilishwa hapa na Mhe. Jaku Hashim Ayoub Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Paje. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, lakini pili napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa jitihada zake za dhati kabisa ambazo kila mwananchi wa Zanzibar anazielewa katika kutaka kuimairisha Sekta ya Afya Zanzibar. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Rais tunamshukuru jitihada zake tunaziona, tunazitambua. Lakini Mhe. Naibu Spika, bado Sekta yetu ya Afya hasa Hospitali ya Mnazi Mmoja inachangamoto kubwa sana ambao sijapata kuiona mimi.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Rais ametoa maagizo mbali mbali kuhusu kuimarika wa Sekta ya Afya nitatoa mfano. Mfano Mhe. Naibu Spika, mimi ni Mjumbe wa kamati ndogo ya chama iliyoundwa kuchunguza changamoto za Wizara ya Afya hasa

katika Hospitali ya Mnazi Mmoja na vitongoji vyake. Mhe. Naibu Spika, tulipokwenda huko tuliyoyakuta ni changamoto kubwa ambazo nyengine hazisemeki hapa. Lakini nyingi zao Mhe. Naibu Spika, palikuwa na mambo mawili tu ya kwanza uzembe na usimamizi mbovu wa baadhi ya watendaji na viongozi wa Mnazi Mmoja. (*Makofi*)

Naomba nirudie Mhe. Naibu Spika, bila ya kutafuta maneno uzembe tumeukuta Mnazi Mmoja ambao unasababishwa na usimamizi mbovu wa watendaji hasa wa Wizara ya Mnazi Mmoja wabovu hawafanyi kazi zao ipasavyo. Wanasababishwa watu kukatwa mikono hadi vifo katika Zanzibar. Mimi ni Mzawa ambaye mtoto wangu pia Mnazi Mmoja kauliwa, kama ingekuwa nchi nyengine asingekufa. Lakini Mnazi kwa sababu ya uzembe ninaujua na nimeushuhudia kauliwa na niliposema nikaambiwa nitashitakiwa nasema tena leo nishitakiwe basi.

Leo narudia tena maana yake walitokeza madaktari wakasema tutakushitaki, hivi na hivi narudia tena kusema leo Mnazi Mmoja mtoto wangu kauliwa na nishitakiwe, na watu baadhi yao wanawauwa kwa uzembe nasema tena leo bila ya kuficha. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, Mnazi Mmoja kuna uzembe kwa sababu ya usimamizi mbovu baadhi ya watendaji wanafanya makusudi usimamizi mbovu. Lakini tunamshukuru sana Mhe. Rais kwa utekelezaji wake wa kutaka kuwasaidia wananchi. Lakini bado kuna viongozi wazembe kuna wasimamizi wazembe hawafai kuongoza Mnazi Mmoja, tumeshachoka.

Mhe. Naibu Spika, Mnazi Mmoja ndio kioo chetu leo hii wananchi wa Zanzibar ....

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Naibu Spika, nikushukuru sana kwa kuniona nataka kumpa taarifa mchangia kuwa anachangia maslahi binafsi sio hoja kamili iliyoelekezwa mbele yetu. Tungemuomba arudi kwenye mstari asichangie yale yaliyokuwa yake na achangie hoja iliyokuwa imependekezwa mbele yetu.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa rudi kwenye hoja.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Naibu Spika, napenda kumshukuru sana Mhe. Komredi Mohamed Said Mohamed kwa kunirudisha katika mstari. Lakini yote kwa kutaka sana kuona maendeleo ndani ya Zanzibar hasa Sekta ya Afya kwa sababu ya jitihada za serikali na jitihada binafsi za Rais.

Mhe. Naibu Spika, kama tutafanya utafiti wa kutosha huyu mtoto amefanyiwa uzembe kama huu nchi za wenzetu analipwa *compensation.* Leo hii mtoto huyu ni ndogo ameshatiwa ulemavu maisha yale yatakuwaje kwa sababu ya wazembe.

Mimi naomba serikali kama kuna mtu kasababisha uzembe huu tumshitaki serikali imshitaki na pia serikali imfungie ku-*practice* kama ni daktari au *nurse* maisha yake. Naliomba sana hilo. (*Makofi*)

Lakini jengine naomba wizara imechaguliwa kufanya hii kazi isikae maofisini ikasimamie wananchi, ikasimamie utendaji wa utekelezaji wa Mnazi Mmoja kule watu ni wazembe wanafanya makusudi...

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa malizia muda wako umeshakwisha.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Naibu Spika, baada hayo machache naomba kuunga mkono hoja ya Mhe. Jaku Hashim Ayoub na sote Wawakilishi na Wawakilishi kwa jumla tuhakikishe tuisaidie serikali yetu katika kuwaletea maendeleo wananchi wetu. Lakini hasa sekta ya Mnazi Mmoja Wizara ya Afya bado uzembe na usimamizi upo mwingi na ubovu upo mwingi. Naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*).

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa fursa hii ili kuweza kuchangia hoja iliyopo mbele yetu.

Mhe. Naibu Spika, kwanza na mimi niungane na Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwa kuwasilisha hoja yake ambayo yenye masikitiko makubwa sana. Kama alivyotangulia kusema mwenzangu Mhe. Hassan Khamis Hafidh hapa kwamba hili suala linasikitisha sana na mimi kama Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na naomba sana hili Azimio ambalo tunaliomba kwamba iundwe tume ikafatilie ikachunguze ni mfanyakazi gani ambaye aliyesababisha mpaka kutokezea hali ile pale.

Lakini pia la pili kwamba hoja yetu au Azimio kwamba serikali imchukulie hatua yule daktari ambaye aliyesababisha masuala haya. Mhe. Naibu Spika, kwa kweli masuala ya Hospitali ya Mnazi Mmoja yanachosha kabisa na utashangaa kwamba inasikitisha kwamba Mhe. Rais au Wizara ya Fedha zinatoa pesa nyingi sana kwa ajili ya huduma ya afya au Wizara hii ya Afya. Leo tunashangaa tunasikitisha kwamba mpaka yanatokezea matatizo kama yale.

Leo mtizame mzazi wake hali ambayo aliyokuwa nayo ya unyonge leo kamzidisha unyonge kabisa na wameweza kumsababishia hatari kwa yule mtoto mwenyewe, maisha yake

kwa kweli mkitizama hali kama ile aliyokuwa nayo pale inasikitisha sana.

Mhe. Naibu Spika, kwa haya machache naunga mkono hoja. Ahsante. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe nimepata vikaratasi vingi sana hapa watu wengi wanataka kuchangia. Lakini nitawaomba radhi muda wetu nimesema tangu mwazo ni nusu saa. Kanuni yetu inatupa uwezo wa hoja za dharura kwa saa moja na tumegawana kwa hoja mbili za dharura.

Kwa hiyo, nimalizie akimaliza Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis tutamuomba na Mhe. Waziri sasa aje na yeye kama kuna jambo lolote aweze kulizungumza. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis karibu.

Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi nikushukuru kwa dhati kabisa kunipa fursa hii kuweza kuchangia hoja hii ambayo imewasilishwa na Mhe. Jaku Hashim Ayoub inayohusu kadhia iliyompata kijana wetu au mtoto huyu ambaye amewasilishwa hapa.

Mhe. Naibu Spika, kitendo kilichofanywa na madaktari wetu kusema la kweli ni kitendo cha kusikitisha sana na hasa ukizingatia waliofanya kitendo hiki sifikirii kama itakuwa ni madaktari au wafanyakazi wa chini, itakuwa ni watalaamu ambao wamewekwa makusudi au wamesomea makusudi kwa ajili ya kufanya shughuli hizi. Lakini leo wataalamu hao tunaowategemea ambao tukiwa na matatizo yetu kwenda kuonana nao ili waweze kutusaidia matokeo yake wanatufikisha hapa sijui tuna hatima gani.

Mhe. Naibu Spika, kitendo alichofanyiwa huyu mtoto mimi kwanza niwaombe Waheshimiwa wenzangu pamoja na jamii kwa jumla tukilaani. Kwa sababu inaonesha wazi kwamba wataalamu wetu wanapofanya kazi zao wanakuwa hawako makini na kutokana na sekta ile ya afya endapo hali itakuwa wataalamu wetu wanaenda katika hali kama hii naona mwisho wa siku watu watakata tamaa kwa kutegemea wataalamu wale.

Lakini Mhe. Naibu Spika, Hospitali ya Mnazi Mmoja kila siku tunaipigia kelele tunaitetea, tunailaumu lakini halafu tunaitetea kutokana na changamoto zilizopo na matokeo yake kama walivyosema Waheshimiwa wenzangu Wajumbe hapa kwamba bajeti inaongezwa kutokana na uzito na majukumu ya sekta ile.

Lakini katika Hospitali ya Mnazi Mmoja pana kitengo cha huduma za marekebisho nina imani kwamba mimi baada ya kupata Mhe. Jaku Hashim Ayoub baada ya kinidokeza niliwafuata wale watu pale. Kosa lililofanyika la yule mtoto ambalo litakuwa ni tishio au litaleta athari kubwa katika jamii kwa kitengo cha huduma za marebisho ambacho tunategemea wananchi ambao wanapata matatizo ya viungo kwenda pale kupatiwa matibabu, lakini vile vile watu wenye ulemavu kwenda pale kupatiwa marekebisho kwa ajili ya kuweza kumudu mazingira. Leo kitengo kile tunachokitegemea kutufanyia marekebisho watu wenye ulemavu kinaongeza ulemavu sijui tufika wapi. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, ndio nikasema hivi kitengo tulikuwa tunakitegemea sana lakini kutokana na matokeo haya watu wenye ulemavu ambao wanahamasishwa kwenda katika kitengo kile kupatiwa marekebisho tutawakatisha tamaa hali kama hizi kwa wataalamu kama hawa. Hii Mhe. Naibu Spika, kwa mtizamo wangu mie nahisi vitendo hivi vinafanyika kutokana na yale yaliyozngumzwa kwamba ufatiliaji haupo lakini hakuna hatua

zinazochukuliwa hata kama mtaalamu atafanya kosa, hakuna hatua zitakazochukuliwa. (*Makofi*).

Ingawa taratibu kanuni zinaeleza lakini naamini hakuna hatua, ingelikuwa kuna hatua wataalamu wanaofanya makosa kama haya wanachukuliwa za kisheria basi haya masuala yasingetokea au yangemalizika kabisa, kila mmoja angefanya kazi kwa mujibu wa utaratibu na kanuni zinavyomuelekeza.

Mhe. Spika, kutokana na kadhia hii ambayo mtu mwenye ulemavu amekwenda kufanyiwa operesheni wa miguu kwa ajili ya kufanyiwa marekebisho ili inyooke, aweze kuyamudu mazingira matokeo yake ameongezewa ulemavu. Kutokana na hili mimi ningependekeza yafuatayo:-

Mhe. Spika kuna sheria, Sheria Nam. 9 ya Mwaka 2006 inasema 'Haki na Fursa', sheria hii imezungumzia kifungu cha 44(1), "Mtu yeyote kwa uzembe atasababisha ulemavu kwa mtu yeyote atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini kiasi kisichopungua Tshs. 5,000,000/= au kifungo kisichozidi miaka mitano au adhabu zote mbili za faini na kifungo".

Vile vile kifungu cha 44(2) kinasema; "Mhe. Naibu Spika, Mahakama inaweza kutoa amri kwa mtu yeyote aliyetiwa hatiani chini ya kifungu hiki kumlipa muathirika kiwango cha fedha kama fidia kwa kiwango ambacho Mahakama itaona inafaa".

Hivyo basi, kutokana na sheria hii na kifungu hiki ambacho nimekinukuu niombe kuchukuliwa hatua za kisheria wale wote waliohusika na kusababisha hili, ili iwe fundisho kwa wao na wengine isiendelee kutokea.

Mhe. Naibu Spika, hii inaipa aibu serikali yetu tunasema tuna wataalamu,wataalamu wenyewe wanafanya vitu kama hivi!

Kusema kweli mimi hili limenisikitisha sana. Lakini vile vile niombe jamii nayo kuwa makini sana tusisubiri mpaka athari ikawa kubwa halafu ndio takaweza kueleza pale pale tuzingatie na sisi wenyewe tuwe macho katika upatikanaji wa huduma tuweze kufatilia.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru naunga mkono hoja.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis nakushukuru sana, Waheshimiwa Wajumbe na mimi ninasimama kutaka kuomba tu kwamba, nafikiri katika yale ambayo yamezungumzwa kuna maazimio ambayo Mhe. Jaku Hashim Ayoub amekuja na maazimio yake pamoja na yale ambayo amezungumza Mhe. Mwanatatu Mbaraka Khamis. Kwa hivyo, nilikua nimesimama hapa kuiomba sana serikali watupe majibu mazuri, tunataka majibu mazuri ya kutupa moyo na kutupa matumaini kuhusiana na Hospitali yetu ya Mnazi Mmoja. Sote sisi tunajua hali halisi ya Mnazi Mmoja ni mbaya sana, wapo wanaofanya kazi vizuri lakini wapo wanaoharibu.(*Makofi*)

Mhe. Waziri ukija hapa utueleze vizuri kwa sababu kila mmoja wetu kapata hisia kubwa sana kuhusiana na suala hili na hili si moja, hili ni moja tu katika hayo, mengi ambayo yanatokea ndani ya Hospitali ya Mnazi Mmoja. Kwa hivyo, naiomba sana serikali ije na majibu mazuri na majibu hayo yasiishie hapa yafanyiwe kazi. Kama vile maazimio ambayo ameyatoa Mhe Jaku Hashim Ayoub yaweze kuyatekelezwa, nakushukuru. Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, karibu.*(Makofi*)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika na mimi nikushukuru sana kwa kunipa ruhusa hii ya kusimama mbele ya Baraza lako tukufu, lakini pia nimshukuru Mhe. Jaku Hashim Ayoub aliyeleta hoja hii, hoja ambayo kila mmoja wetu aliyesikia imemsikitisha sana na imemhuzunisha

sana. Aidha, niwashukuru sana Wajumbe waliochangia, naelewa wametoa yaliyomo ndani ya sakafu ya mioyo yao wakieleza madhila na matatizo yanayojitokeza katika Hospitali yetu ya Mnazi Mmoja.

Sisi kwa upande wa serikali nataka niwahakikishie wajumbe hawa na Baraza lako tukufu Mhe. Naibu Spika, tumelisikia, tumeyasikia maelezo ya kina ya wajumbe, tunayapokea kwa kwenda kuyafanyia kazi na naamini wale wote ambao watakua kwa njia moja au nyengine ni wahusika kwa uzembe, utendaji mbovu, hujuma au kwa njia moja au nyengine kusabibisha wananchi wetu kupata madhara wakati serikali yao inachukua kila jitihada ya kutoa huduma katika sekta ya Afya. Kwa hivyo, wahusika wote watachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, serikali wakati wote ilikuwa inapanga mipango kwa mujibu wa sheria ili tupate huduma bora katika Hospitali yetu hii Kuu ya Mnazi Mmoja. Tumeanzisha sheria ya Hospitali ya Mnazi Mmoja msingi wake madaktari wetu, ma-*nurse*, wafanyakazi wote wafanye kazi kwa nidhamu, kujali utu wakijua kwamba wao wanahudumia binaadamu ambapo kwa njia moja au nyengine wanapaswa kuwa na moyo wa huruma katika kufanya hivyo.

Vile vile, serikali kwa mujibu wa sheria imeaanzisha mabaraza ya madaktari pale, imeanzisha Baraza la ma-*nurse,* msingi wake mkubwa mabaraza haya yakae yanapojitokeza matatizo wachukue hatua, lakini kama yameshindwa serikali sasa itachukua hatua zinazofaa kwa kila mhusika.(*Makofi)*

Imekuwa ni kilio cha muda mrefu katika eneo hili, serikali imeendelea ikifanya juhudi kubwa ya kuongeza bajeti katika Wizara ya Afya na kuongeza bajeti katika Hospitali ya Mnazi Mmoja. Imekuwa ikinunua vifaa, kuongeza wataalamu, kuongeza

mishahara, kujenga majengo mapya, na kuhakikisha kwamba inafanya kwa kila linalowezekana ili huduma bora za afya ziweze kupatikana. Kwa hivyo, kwa wale wanaofanya uzembe na wanao *sabotage* kwa makusudi hatutokubaliana nao. Kwa hivyo, nachukua maelezo yenu Waheshimiwa Wajumbe kwa masikitiko tuyapeleke serikalini yafanyiwe kazi na watakaohusika wote hatua za kisheria zitachukuliwa. Tunawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe mtuachie kazi hii tukaifanye na naamini matokeo yake nyote mtafurahi. Ahsante sana. *(Makofi*)

Utaratibu

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe.Naibu Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi hii na mimi nikataka utaratibu kidogo kuhusu jawabu ya serikali kuhusu hoja kusikitisha sana.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa unatumia kifungu gani cha kanuni?

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe Naibu Spika, nimetumia kifungu cha 63. Mhe. Naibu Spika, serikali imetoa jawabu itawachukulia hatua za kinidhamu watendaji wa serikali, lakini hoja ya Mhe. Jaku Hashim Ayoub moja haikujibiwa haikutolewa ufafanuzi, suala la kijana ambaye ameathirika kupatiwa matibabu ya uhakika, lakini vile vile kusomeshwa kufidiwa sasa hili limeachwa hivi hivi. Kama alivyoeleza Mhe. jaku Hashim Ayoub kwamba yule mzazi wa mtoto ni mnyonge wa Mungu na tumemouna pale hali yake inaonekana. Sasa hili limeachwa hivi hivi hizo taratibu za nidhamu yule baba mzazi wala hilo yeye zitakuwa hazimuhusu, yeye anataka kuangalia maisha ya mtoto wake atafidiwa vipi na atasomeshwa vipi. Hilo tunataka ufafanuzi. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Nimekuelewa Mhe. Hamza Hassan Juma, Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru na namshukuru Mhe. Hamza Hassan Juma kwa maelezo yake, kwakuwa Mhe. nimesema tunakwenda kulifanyia kazi na kwakuwa tunajua watoto ni watoto wetu sote, sote nimesema tunahuzunishwa na vitendo hivyo na vyengine vinavyotokea. Kwa hivyo, ni wajibu wetu kama serikali kulifanyia kazi kwa kina jambo hili, naamini kwa serikali yetu sikivu, serikali yetu inayopenda wananchi kila ambalo limezungumzwa hapa litafanyiwa kazi ipasavyo, ili yatoke majibu yenye uhakika na undani kwa mujibu taratibu zetu ndani ya serikali. Ahsante sana.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Waheshimiwa tumemaliza hoja hii, nimpongeze sana Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mhe. Jaku Hashim Ayoub unaweza ukazungumza kwa dakika tano.

Mhe. Jaku Hashim ayoub: Mhe Naibu Spika. nichukue fursa hii kuwapongeza kwa dhati kabisa Waheshima Wajumbe wa Baraza hili wote kabisa. Kama ulivyosema Mhe. Naibu Spika, wachangiaji walikuwa ni wengi na kila mtu limemgusa kwa masikitiko makubwa niwatambue wachangiaji kwa haraka haraka waliochangia kwa maneno alikua wa kwanza Mhe.Hassan Khamis Hafidh, nimpongeze kwa dhati kabisa.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh, nikupongeze, umempongeza sana Mhe. Rais kwa jitahada anazochukua lakini kuna uzembe unaofanyika nikubaliana na wewe, uzembe upo Mnazi Mmoja na hili tatizo lichukuliwe. Mnazi Mmoja kwa kweli hatua zichukuliwe na muhimu mtoto huyu ameumia alipwe fidia hili nikubaliane nae kwa mtoto huyu anataka kulipwa fidia.

Wa pili, nimshukuru sana Mhe. Asha Abdalla Mussa wa Kiwengwa. Mchango wake Tume iundwe inahitajika na hatua zichukuliwe namshkuru ipo haja ya kuundwa Tume. Lakini kwa aina yake nimshukuru sana jirani yangu Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis kwa mchango wake, yeye ni mtetezi mkubwa kwa watu wenye ulemavu na anauhitaji maalum hasa walemavu. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis amechangia kuhusu kitengo cha marekebisho ya Mnazi Mmoja, mimi naungana nae moja kwa moja ufuatiliaji wa hapo unaonesha makosa hatua za kisheria zichukuliwe kwa kweli hatua tunazipigia kelele siku tumeonekana vibaya namshukuru sana Mhe. Mwanatatu kwa mapendekezo hayo kwa mujibu wa sheria na mimi niungane nae.

Waliochangia kwa maandishi, kuna Mhe. Ali Khamis Bakari, waziri alikuwepo wapi? waziri hawezi kufanya yote waziri anajitahidi sana tukubaliane kwanza tulipotoka Mnazi Mmoja na tunapokwenda hivi sasa tuseme ukweli mabadiliko yapo, tusilaumu tu Mnazi Mmoja tulipotoka na tunapokwenda sasa hivi *change* zipo tuwe wa kweli tofauti na vile mwanzo kama hatua tatu tumepiga hatua tatu mwanzo palikuwa pana uwoza zaidi kwa *changing* zipo kidogo.

Baada ya hapo kuna mwengine Mhe.Mohamed Said Mohamed nimshukuru kwa dhati kabisa kwa mchango wake. Mhe. Mohamed Said Mohamed yule mtoto serikali itafikiria kumlea na kumpa masomo, maisha yake hakuyategemea yemetokana kwenye serikali matatizo aliyoyapata, kwa yule mtoto Mhe. Mohamed Said Mohamed nikushukuru kwa dhati kabisa mtoto yule serikali imtazame kwa elimu na ipatikane na wamlee kutokana na wazazi wake hawawezi kumsomesha.

Nimalizie kwa Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis nikushukuru kwa dhati kabisa nawe niungane nawe kabisa kwa mapendekezo yako, kuwa mnazi Mmoja matatizo yapo na baada ya kupungua

yanazidi wakati mwengine kwa hili lipo na hili pendekezo nipendekeze.

Mheshimiwa kwa kutilia mkazo niombe serikali ikubali kumshughulikia mtoto yule, yule mtoto kapata ajali kazini na katika mikono ya serikali. Kwa hivyo, yule mtoto serikali imchukue naiomba kama alivyosema Mhe. Mohammed Aboud Mohammed na alikua ni mchangiaji mwengine kuwa serikali ichukue wazo hili ifikirie na serikali haishindwi serikali hii ipo kwa ajili ya wananchi wanachi ndio serikali *otherwise* pasingeli kuwa na kitu kama pangelikuwa hapana wananchi, wananchi ndio serikali, pengine yule mtoto angelikuwa Mwakilishi humu ndani au angelikuwa waziri. Ahsante sana Mhe Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Jaku Hashim Ayoub, sasa niwahoji wajumbe wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Jaku Hashim Ayoub, wanyooshe mikono, Waheshimiwa Mawaziri wanakutazameni. Kwa hivyo, Baraza zima wamekubalina na hoja ya Mhe Jaku na mimi naamini kwamba serikali yale ambayo imeahidi kwamba yatafanywa na tutaomba sana Mhe.Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa *interest* yetu tutaomba sana katika hatua ambazo zitachukuliwa kutokana na kesi hii tunaomba tuletewe hapa ndani ya Baraza kujua nini kimefanyika.

Waheshimiwa Wajumbe sasa tunaendelea na hoja yetu ya pili ya Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf, Mhe. Nadir karibu sana. (*Makofi).*

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: *Bismillah Rahman Rahiim*. Mhe. Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia uzima lakini vile vile na mimi nitoe pole zangu za dhati kabisa kwa mama huyu aliyepata matatizo, Mwenyezi Mungu amjaalie kila la kheri serikali ipo itaangalia kama ilivyosema. Lakini na mimi ningetoa ushauri wangu mdogo

Waheshimiwa sote tuchangie shilingi 25,000/= tumpatieni angalau shilingi 2,500,000/= yule mama kama mchango wetu, Mheshimiwa hilo lilikuwa ni wazo langu tu.

Mhe. Naibu Spika, mimi nitaendelea na hoja yangu ambayo nimenyanyuka nayo, hoja ya dharura ya kuhusiana na Professor Kabudi, juzi alitoa *speech* ile kauli yake aliyoitoa Bungeni wakati alipokua akiulizwa swali alijibu huyu Waziri wa Katiba na Sheria *Professor* Kabudi, akajibu Waziri Kabudi aliliambia Bunge kuwa Katiba Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mkuu wa Nchi, hivyo Katiba inamruhusu kufanya hivyo. Amesema jamii inapaswa kutambua kuwa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pia ni Mjumbe wa Baraza la Mawaziri na la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania *Professor* Kabudi ametoa ufafanuzi huo Bungeni.

Vile vile alieleza kwamba …

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Nadir Abdul-Latif Yussuf utaratibu unakataza kusoma, huwezi kutoa hoja ikawa unasoma sehemu.....

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Haya alivyotoa yeye maelezo yake kwamba Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yeye ni mkubwa wa kila kitu kuhusiana na upande wa Zanzibar, na vile vile Mhe. Rais wetu Dkt. Ali Mohamed Shein na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pia ni mjumbe kama mawaziri wengine wa Jamhuri ya Muungano.

Mimi nitaanza kuanza na Katiba yetu ya Zanzibar ya mwaka 1984 sehemu ya kwanza inasema Zanzibar na mipaka yake kifungu cha 3 naomba kunukuu Mhe. Naibu Spika, “Zanzibar ni nchi ambayo eneo la mipaka yake ni eneo lote la Visiwa vya Unguja Pemba pamoja na visiwa vidogo vilivyozungukwa na bahari yake ambayo kabla ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ikiitwa Jamhuri ya watu wa Zanzibar”.

Kifungu namba 2 Zanzibar ni Miongoni mwa nchi mbili ninazounda Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania. Lakini hapo hapo kwenye Katiba hii ya Zanzibar nikienda kwenye kifungu cha 43(5) Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya mamlaka ya Rais ndio itakuwa na uwezo wa kufanya maamuzi juu ya sera za serikali kwa ujumla na mawaziri chini ya uongozi wa Makamu wa Pili wa Rais watawajibika kwa pamoja katika Baraza la Wawakilishi kuhusu utekelezaji wa shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Hapo hapo Mhe. Naibu Spika,nitakwenda kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania ya mwaka 1977, sehemu ya kwanza kifungu namba 4.

"Utekelezaji wa shughuli za mamlaka ya nchi sheria na shughuli zote za mamlaka ya nchi katika Jamuhuri ya Muungano zitaelekezwa na kudhibitiwa na vyombo viwili vyenye mamlaka ya utendaji vyombo viwili vyenyewe vyenye mamlaka ya utekelezaji utoaji haki na pia vyombo viwili vyenye mamlaka ya kutunga sheria na kusimamia utekelezaji wa shughuli za umma".

4(2) Vyombo vyenye mamlaka ya utendaji vitakuwa ni Serikali ya Jamuhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, vyombo vyenye mamlaka ya kutekeleza utoaji wa haki vitakuwa ni Mahkama ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Mahakama ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, na vyombo vyenye

mamlaka ya kutunga sheria na kusimamia utekelezaji wa shughuli za umma, litakuwa ni Bunge la Tanzania Bara na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar ndani ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, namba 3 kwa ajili ya utekelezaji bora wa shughuli za umma katika Jamhuri ya Muungano na kwa ajili ya mgawanyiko wa madaraka juu ya shughuli hizo, baina ya vyombo vilivyotajwa katika ibara hii, kutakuwa na mambo ya Muungano kama ilivyoorodheshwa katika nyongeza za kwanza iliopo mwishoni mwa katiba hii. Pia kutakuwa na mambo yasiyo ya Muungano ambayo haya ndio yanayomuhusu Dkt. Ali Mohammed Shein na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, ambayo ni mambo mengine yote yasiwe ndani ya mambo ya Muungano.

Namba 4, kila chombo kilichotajwa ibara hii kitaundwa na kutekeleza majukumu yake kwa kufuata masharti mengine yaliomo katika katiba hii.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusoma katiba hizi mbili na tukiangalia kauli ya waziri huyu *Professor* Kabudi. Unajua kuna watu wanakuwa na elimu sana wanakuwa ma-*professor* mwisho wanaruka akili wanakuwa wendawazimu.

Mhe. Naibu Spika, ninachotaka kuzungumza mimi kauli ya ....

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe tumia lugha nzuri, kusema kama mtu mgonjwa wa akili ni makosa makubwa.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Vipi?

Mhe. Naibu Spika: Nasema lugha unayotumia, tumia lugha nzuri.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. Kama nilivyoeleza kuna mambo hayaingii akilini. Leo kuinuka waziri wa Jamhuri ya Muungano sio mmoja wala sio wawili. Mfano unaotokezea tumeanza kuona, kuna kauli nyingi ambazo zinabishana na mwenendo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kuivunjia hadhi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na hususan *direct* na *indirect* kumu-*attack* Mhe. Rais wetu wa Zanzibar kwa mambo ambayo yasiyo ya kweli. Kwa kweli waziri huyu kenda kinyume na Katiba, katudhalilisha sisi Wazanzibari wote, kamdhalilisha Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Vile vile kafananisha na mawaziri ambapo *status* yake yeye ni Rais. Mhe. Rais amechaguliwa na wananchi wa Zanzibar na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano kachaguliwa na wananchi. Maamuzi yoyote na mambo yoyote yanayohusiana na mambo ya Muungano ni lazima ni vyema wakae Marais wawili washauriane, wajadiliane na wakubaliane na si vyenginevyo kunyanyuka waziri. Tumekuta tuna mawaziri hapa wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa kweli wana heshima za hali ya juu, hawajawahi kuwatovukia adabu hata mtu mmoja Tanzania Bara, inakuwaje leo Waziri wa Tanzania Bara ana-*attack* Unguja na wengineo wanafuatia.

Mfano mdogo nitamzungumza mwengine Mhe. Mbarawa, wakati anauliza Mhe. Saada Mkuya swali la kutetea Zanzibar, akamwambia kwamba wazanzibari Pemba vijiweni na Darajani vijiweni, mbona hakutaja Dodoma vijiweni na Dar es Salaam na Arusha vijiweni. Kwa maana hiyo kwamba Wazanzibari hawana akili na yeye tunampa salamu kwamba tabia kama hizi waziwache, Waziri huyu Kabudi, Mbarawa na wengine. Tunataka tuone nidhamu katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na sheria tunazozitunga sisi ziheshimike. Watambuwe kwamba Dkt. Ali Mohammed Shein ni Rais hapa, ana mamlaka yake na mamlaka

ambayo yamo kwenye Muungano Dkt. John Pombe Magufuli yanamuhusu, mambo ambayo hayamo kwenye Muungano Dkt. Ali Mohammed Shein ndio mambo yake.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante hoja imeungwa mkono na baadhi ya wajumbe. Waheshimiwa Wajumbe, Mhe. Nadir Abdul-latif katoa hoja naona wajumbe kidogo wamenyanyuka kukubali hoja yake. Sasa vipi ijadiliwe. Kama hamjaikubali ina maana tusiijadili. Mhe. Hamza Hassan Juma.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nikaweza kuchangia hoja mahususi ya Mhe. Nadir Abdul-latif aliyoileta kwenye kikao chetu hiki cha leo.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wangu na mimi napenda sana kutoa masikitiko yangu kwa mwendelezo wa kauli za kuidhalilisha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Mhe. Naibu Spika, kwa kweli Zanzibar sisi ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na bila ya Zanzibar kungekuwa hakuna Muungano, kwa sababu Muungano wowote unatokana na kuunganishwa kwa kitu kuanzia viwili kuendelea vingi. Tunawashukuru sana viongozi wetu waasisi ambao ni Mzee Abeid Aman Karume kwa upande wa Zanzibar na Mwalimu Julias Kambarage Nyerere kwa upande wa Tanzania Bara. Kwa nia njema kabisa kwa kuona kwamba nchi zetu mbili hizi wananchi wake wana mahusiano ya kidugu, ya kibiashara na ya kidamu na ndio maana wakaamua kuunganisha nchi zetu.

Mhe. Naibu Spika, kwa miaka mingi sana sisi tokea tuko wadogo walipokuwepo viongozi wetu hawa, hatukusikia kauli za kudhalilishana, za kuona huyu mdogo, labda za kuona huyu

mkubwa au huyu ana mamlaka gani na huyu mwengine ana mamlaka gani.

Lakini Mhe. Naibu Spika, kama alivyosema wenzangu hawa kwamba sasa hivi watu wamesoma sana, na kila watu wakisoma sana wanajaribu kuchambua. Sasa wanaanza kuondoa ile dhana ya nia njema ya Muungano wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, baina ya Tanganyika na Zanzibar. Mhe. Naibu Spika, mimi pia niliwahi kusikia kauli kwa kupitia vyombo mbali mbali vya habari kauli ya Professor Kabudi. Kwa kweli kauli yake ilikuwa sio sahihi na tatizo la Professor Kabudi inaonesha haelewi anachokizungumza leo na anachokizungumza kesho.

Mhe. Naibu Spika, tatizo tulilokuwanalo tuna hii mitandao ya kijamii. Jambo unalolizungumza leo baada ya miaka mitano au sita bado lipo linaonekana na sasa hivi tayari watu wanaanza kurushiana *clip* wanajiuliza Professor Kabudi ndio huyu wa juzi na huyu wa sasa hivi. Kwa hivyo, mimi nadhani Mhe. Naibu Spika, sisi kama wanasiasa tujitahidi sana kuchunga ndimi zetu, tujitahidi sana kufuata maadili, lakini vile vile tuuangalie Muungano huu uwasisi wake ulikuwa ni kitu gani.

Kwa hivyo, kauli waliyoizungumza kwamba Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mkuu wa nchi, ni kweli yeye ni mkuu wa nchi, ana mamlaka yote, ni kweli ana mamlaka yote. Lakini katiba hiyo ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inazungumzia kwamba kutakuwa na mamlaka mbili za utendaji ndani ya serikali. Kama ibara ya 64 ilivyoeleza ambayo Mhe. Nadir Abdul-latif ameisoma sina haja ya kurudia kupoteza muda, *Hansard* itachukuliwa ile ya Mhe. Nadir Abdul-latif.

Mhe. Naibu Spika, lakini mimi nilikuwa nataka niingie katika katiba hiyo ya Jamhuri ya Muungano ukurasa wa 88 Sura ya Nne Ibara ya 102 Mhe. Naibu Spika, naomba univumilie kidogo

niisome ili tupate kujua kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inatambulikana ndani ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Ibara 102(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Kutakuwa na Serikali ya Zanzibar itakayojulikana kama "Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar", ambayo itakuwa na mamlaka katika Zanzibar juu ya mambo yote yasiyo mambo ya Muungano kwa mujibu wa masharti ya katiba hii.

(2) Bila ya kuathiri masharti yaliyomo katika ibara hii na katika ibara zifuatazo za katiba katika sheria hii na Katiba, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaundwa na kutekeleza madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya katiba hii ya Katiba ya Zanzibar, 1984.

Sasa mheshimiwa anaposema kwamba Rais wa Jamhuri ya Muungano anaweza kutoa agizo kwa waziri yeyote wa Zanzibar, sio sahihi. Mhe. Naibu Spika, mawaziri hawa waliokuwepo hapa wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wanawajibika kwa Baraza la Wawakilishi, hawawajibiki Bungeni. Sasa leo nani anaweza kusema kwamba waziri wa Zanzibar anaweza kupewa agizo na kiongozi yeyote, hilo sio sahihi. Professor Kabudi kama kasoma sheria na sisi tumesoma sheria tunajifunza. Mzee Karume alituambia tulisoma hatukujua, lakini tumejifunza tumejua.

Kwa hivyo, naomba sana na utaratibu wa viongozi wetu hawa tokea asili na jadi, linapotokezea jambo Rais wa Jamhuri ya Muungano kwa jambo ambalo sio la Muungano, anawasiliana na Rais mwenzake Rais wa Zanzibar, anamwambia kuna jambo moja, mbili. Rais wa Zanzibar yeye ndiye anapaswa kumpa agizo atekeleze jambo lolote waziri wa Zanzibar. Kwa sababu leo Rais wa Jamhuri ya Muungano hawezi kumuajibisha Waziri wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, isipokuwa Rais wa Zanzibar

yeye ndio ana uwezo wa kumuajibisha waziri kwa sababu yeye ndiye aliyemteuwa.

Kwa hivyo, mimi naomba sana Mhe. Naibu Spika, kuna viashiria ambavyo kidogo havituletei afya. Mhe. Naibu Spika, Zanzibar ni nchi ambayo imekaa kama yai,

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe malizia muda wako umekwisha.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Namalizia. Kwa hivyo, jambo lolote linapogusa maslahi ya Zanzibar, basi Wazanzibari damu zao zinachemka. Sasa hivi kila unapopita vijiweni, wapi huko na hata huko alikosema Mhe. Makame Mbarawa, katika hivi vijiwe alivyovidhalilisha vijiwe vyetu. Sisi tunavithamini ndio vinotupa kura. Sisi tunapata kura Micheweni, Darajani, Kwamtipura, Shaurimoyo kila pahala. Sasa kama yeye kapata kura Dodoma, sawa, lakini sisi tunachaguliwa, na Rais wa Zanzibar anachaguliwa na Wazanzibar na ndio hao waliokuwepo katika vijiwe.

Naomba Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo machache naunga mkono. Lakini nina ombi kwa serikali, tunamuomba Waziri wa Katiba na Sheria wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, atukutanishe baina ya Bunge la Jamhuri ya Muungano na Baraza la Wawakilishi tuzungumze, kuna mambo mengi mheshimiwa, kuna changamoto nyingi. Nimejaribu kunukuu hapa kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano, kuna mambo haya nahitaji yafanyiwe ufafanuzi, kuna changamoto. Naomba nimalizie kwa haya. Katika nyongeza ya kwanza Orodha ya Mambo ya Muungano

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Hamza Hassan ulikuwa umeshamaliza.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Ndio namalizia. Suala la mikopo na biashara za nje tuna changamoto, tuna suala la kodi ya mapato tuna changamoto, kuna suala la bandari tuna changamoto, tuna suala la leseni za viwanda na takwimu tuna changamoto, tuna suala la elimu ya juu tuna changamoto, tuna suala la maliasili mafuta hili kidogo limeshapata ufumbuzi lakini bado kuna changamoto na suala la usafiri na usafirishaji wa anga kuna changamoto. Sasa haya aje ili tuzungumze naye, asikae tu akazungumza mambo ya ajabu ajabu, sisi hizi ndio tunazofanyia kazi.

Mhe. Naibu Spika, ni lazima tuzungumze na hili naomba sana serikali yetu tukae Bunge na Baraza la Wawakilishi, sisi ndio tuliopewa jukumu la kutunga katiba. Hatuzungumzii katiba mpya, tunazungumzia kurekebisha matatizo yaliyokuwemo ndani ya katiba zetu.

Baada ya hayo Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, naunga mkono hoja ya Mhe. Nadir Abdul-latif. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Mjumbe. Mchangiaji wa pili atakuwa ni Mhe. Miraji Khamis Mussa Kwanza. Nafikiria baada ya hapo tutampa nafasi Mhe. Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii ya Mhe. Nadir Abdul-latif. Kwanza nimpongeze sana Mhe. Nadir Abdul-latif kwa kuwasilisha hoja hii. Lakini pia nimpongeze mchangiaji aliyemaliza, na mimi sitokuwa na mengi sana.

Mhe. Naibu Spika, kweli kauli aliyosema Mhe. Waziri sio kauli sahihi, hasa kwa kuzingatia uwepo wa katiba mbili. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Katiba ya Zanzibar,

ambapo Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama ambavyo mwenzangu alivyosema, ndio inayoitambua Katiba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, na yapo mambo ambayo yametajwa ndani ya katiba. Ukifuatilia utakuta katika *Article of Union* kuna mambo 22 tumekubaliana kwamba haya yaende katika Sura ya Muungano, lakini yapo mambo ndani ya Katiba hiyo ya Jamhuri ya Muungano haya yatasimamiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano lakini kwa masuala ya Tanganyika. Lakini yapo mambo yatafanyiwa kazi na kumaliziwa kwenye Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, huo ndio Muungano wetu. Sasa atakapotokea waziri akaanza kutoheshimu maneno yaliyokuwemo ndani ya katiba, sisi tunapata mashaka sana na ndio maana leo hoja hii imekuja kwa sababu tayari inaingilia majukumu ya kikatiba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, narejea kusimamia viongozi wetu hawa wa pande zote mbili. Kwanza tunaendelea kuwaomba na kuwanasihi waheshimu sana katiba mbili hizi ya Jamhuri ya Muungano, lakini na Katiba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Muungano huu utaishi vizuri, serikali mbili hizi zitaishi vizuri. Lakini kauli iliyotoka inaashiria kuongeza changamoto nyengine ndani ya zile changamoto ambazo zipo ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sasa.

Sasa Mhe. Naibu Spika, kuleta hoja hii na kusimama kwetu, zaidi sisi tunawakumbusha wenzetu kuisimamia katiba. Nilizungumza mapema kuwa yapo mambo ya Jamhuri ya Muungano, lakini yapo mambo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Lakini pia kauli ile, sisi tunakubali kama Rais wa Jamhuri ya Muungano ni Mkuu wa Nchi, lakini kwa yale mambo ambayo yametajwa ndani ya katiba, lakini mkuu wa nchi katika mazingira ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mambo ambayo sisi sehemu ya mambo yale tumo kama Zanzibar. Lakini yapo mambo ambayo yanasimamiwa

na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ndio tunayogombana nayo sasa.

Mhe. Naibu Spika, kubwa katika yote haya basi sote viongozi tuziheshimu katiba tulizoziweka, hakuna jambo jengine zuri zaidi ya hili. Lakini Mhe. Naibu Spika, jambo moja ambalo ni zuri zaidi kwa sote pande zote mbili ya Jamhuri ya Muungano, lakini na sisi Zanzibar. Kuendelea kustahamiliana pia, kwa pale viongozi wetu wanapoteleza tuyaseme haya wao wakae warekebishe sehemu ya kauli zao, lakini na sisi tuwakumbushe au sisi watukumbushe pale ambapo wanateleza. Maana kauli moja kubwa ambayo sisi iliturejesha nyumba ni kuteleza kwa waziri aliyoitoa kauli ile juzi. Kwa hivyo, tunawaomba wenzetu waendelee kuiheshimu Katiba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa sababu katiba hiyo imetajwa ndani ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kuunga mkono hoja hii, mimi sina mengi kwa sababu katiba zote mbili alizisema Mhe. Nadir Abdul-latif. Lakini kwa ujumla nimpongeze sana Mhe. Nadir Abdul-latif na Mhe. Hamza Hassan. Mimi naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Mjumbe nakushukuru. Sasa nafikiri ni nafasi ya *AG* Mwanasheria Mkuu, na yeye atazungumza machache. Karibu Mhe. Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya angalau kusema machache ya kuchangia hoja hii ya Mhe. Nadir Abdul-latif ambayo amekuja nayo leo asubuhi. Lakini mengi ambayo Mhe. Nadiri Abdul-latif ameyazungumza, ameyazungumza kwa ku-*refer* vifungu vya katiba, lakini na wajumbe wengi ambao wamechangia wamejenga pia hoja zao kwa ku-*refer* vifungu vya katiba, tena katiba zote mbili. Katiba ya

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984.

Hiyo ndio misingi ya nchi yetu Mhe. Naibu Spika. Nchi yetu inaongozwa kwa kuzingatia masharti ya katiba na sheria ambazo zinatungwa na Baraza la Wawakilishi au na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuzingatia masharti ya Ibara ya 64 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Ibara ya 64 imetoa mamlaka kwa Bunge kwa kutunga sheria ambazo ni za Muungano, lakini pia kutunga sheria ambazo sio za Muungano ambazo zitatekelezwa kwa Tanzania Bara.

Pia tujue hayo hayo Mhe. Naibu Spika, kama pia nguvu za kutunga sheria kwa mambo yote ambayo sio ya Muungano yako mikononi mwa Baraza la Wawakilishi, kwa mujibu wa kifungu cha 78 cha Katiba ya Zanzibar. Sasa tuondowe hofu Waheshimiwa Wajumbe mambo haya yanapozungumzwa majibu yake ni kama haya ambayo Waheshimiwa Wajumbe wameyajibu. Mtu anapozungumza wewe mwelekeze kwenye masharti ya sheria na masharti ya katiba, ndio nchi hii inavyoongozwa. Nchi hii haiongozwi kwa maagizo, kwa sababu maagizo utekelezaji wake ni wa kisheria.

Sasa kama agizo ambalo limetoka utekelezaji wake unahitaji kutekelezwa kwa sheria ambayo imetungwa na Bunge itatekelezwa, na kama maagizo yametoka kwa sheria ambazo utekelezaji wake unahitaji matekelezo hayo kutekelezwa kwa sheria zilizotungwa na Baraza la Wawakilishi zitatekelezwa. Hakuna haja ya kushindanisha nguvu kwenye mambo ya kisheria, mambo ya kisheria yako wazi Mhe. Naibu Spika. Tokea tuungane viongozi wetu wakuu wanaheshimiana katika kuongoza, kila mtu anajua ana mipaka yake ya kikatiba na ya kisheria.

Kwa hivyo, niwatowe hofu sana Waheshimiwa Wajumbe, kama haya mambo ambayo wameyachangia na mimi nashukuru wameyachangia kwa kuzingatia masharti ya Katiba na masharti ya Sheria. Lakini Mhe. Naibu Spika, hakuna mtu anaepinga kuwepo kwa Rais wa Zanzibar, hata ibara ya 103 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imetambua kuwepo kwa Rais wa Zanzibar. Kwa hiyo hili jambo la kisheria na la Kikatiba na mipaka yake imelezwa kwa mujibu wa kifungu 51 cha Katiba ya Zanzibar kama madaraka yote ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yatakuwa mikononi mwa Rais atayatekeleza yeye mwenyewe au atakasimu madaraka kwa viongozi wengine. Sasa hao waliokaa mbele hapa ndio ambao wamekasimiwa hayo madaraka ya Mhe. Rais, kutekeleza mambo yote ambayo si ya Muungano kwa Zanzibar, huo ndio utaratibu wa kisheria ulivyo.

Sasa mimi niwatoe hofu sana Waheshimiwa wajumbe mambo haya yanapozangumzwa tuyajibu kwa kufuata misingi ya Katiba na misingi ya sheria, kama ambavyo Waheshimiwa wajumbe wamechangia na hio ndio kazi yetu na hiyo ndio *role* ya Waheshimiwa Wajuumbe wa Baraza la Wawakilishi, anapokwambia mtu wewe mrudishe kwenye sheria na mrudishe kwenye Katiba hapo tutaelewana na kama jambo halitekelezeki kwa mujibu Katiba au sheria zilizokuwepo jambo hilo haliwezi kutekelezeka, ama litatekelezeka kwa upande wa Zanzibar au litatekelezeka kwa upande Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hiyo ndio misingi ambayo tunayo.

Mhe. Naibu Spika, sasa mimi niungane nazo hoja zote ambazo waheshimiwa wajumbe wametoa ambao wame-*refer* Katiba ya Jamhuri ya Muungano Tanzania, lakini pia wame-*refer* Katiba ya Zanzibar kuzungumzia namna ya madaraka na uwezo wa kisheria uliopo katika nchi zetu hizi mbili.

Baada ya kusema hayo Mhe. Naibu Spika, na mimi niunge mkono hoja kwa asilimia moja.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu ya Pili wa Rais: Mhe**.** Naibu Spika nakushukuru, Aidha nimshukuru sana Mwanasheria Mkuu kwa kutoa ufafanuzi kwa ufasaha kabisa wa kisheria kuhusiana na mada ya Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy aidha na mimi nimshukuru sana Mhe. NadirAbdul-latif Yussuf Al-Wardy kwa kuleta hoja hii na niwashukuru wajumbe wote waliotangulia, waliochangia hoja.

Mhe. Naibu Spika, Muungano wetu umeundwa kwa misingi ya udugu na misingi ya kukubaliana kushauria na kusaidiana. Viongozi wetu waliotutangulia marehemu mzee Abeid Amani Karume na marehemu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere walifanya kazi kwa mapenzi makubwa na kuhurumiana na kukubaliana, wamejenga msingi mkubwa sana kwa kuendeleza muungano huu, na viongozi waliopo sasa wamefuata nyayo hizo Rais wetu Dkt. Ali Mohamed Shein na Dkt. John Pombe Magufuli wanashauriana, wanakubaliana wanaendeleza Muungano wetu naamimi msingi wa Muungano wetu huu uliojengwa ni imara na utaendelea kuwa imara.

Kwa hiyo Mhe. Naibu Spika, jambo la msingi hapa patapotokea sitofahamu ya aina yoyote au neno lolote ambalo linakera upande mmoja wa muungano wetu utaratibu mzuri ni huu ambao Mwanasheria mkuu ameueleza na baadhi ya wajumbe wameueleza hapa, kwamba msingi wetu ni Katiba yetu msingi wetu ni sheria zetu na msingi wetu nidhamu yetu tunayokaa pamoja ya kushauriana mambo na kujenga nchi yetu.

Mhe. Rais wa Zanzibar kwa mujibu wa Katiba yetu ndio mkuu wa nchi ya Zanzibar na ndio mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, na wakati wote hufanyakazi kwa kufuata misingi ya

Katiba na Sheria. Vile vile anaposhiriki katika Baraza la Mawaziri wa Jamuhuri ya Muungano anashiriki akiwa Rais wa Zanzibar na anaapishwa na Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa msingi wa kutambua kwamba yeye ni Rais wa Zanzibar anakuwa pia mjumbe wa Baraza la Mawaziri katika Baraza la Mawaziri wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Si kwa kuteuliwa ni kutokana na nafasi yake ya kuwa Rais wa Zanzibar na kwa mujibu wa taratibu zetu Rais wa Zanzibar ni kiongozi wa tatu wa kitaifa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania badala ya Rais wa Jamhuri ya Muungano, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano anaefuata ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Kwa hiyo utaratibu wetu uko wazi, uko safi na tunafanyakazi kwa mujibu wa Katiba na Sheria, naomba sana Waheshimiwa wajumbe na wananchi wote tuendelee kuheshimu Katiba yetu, tundelee kuheshimu sheria zetu, tuendelee kuheshimiana na kupeana nidhamu ya hali ya juu kwa nia ya kuimarisha muungano wetu. Nia na dhamira ni kuundeleza na kuuimarisha zaidi na pale panapotokea hitilafu ya aina yoyote tunakaa chini kuzungumza hitilafu hizo na kuondoa jambo linalotokea.

Kwa hivyo niwaombe sana viongozi wenzangu, kwa upande wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa upande wa Zanzibar, tusimame katika Katiba zetu, tusimame katika sheria zetu, tusimame katika misingi ambayo viongozi wetu walianzisha ya kupendana, kuheshimiana na kuishi pamoja katika nidhamu ya hali ya juu ili kuepusha aina yoyote ambayo inaweza kusababisha migongano, inaweza kusababisha mivutano, inaweza kusababisha changamoto mbali mbali katika Muungano wetu. Naamini tutaendelea kuwa pamoja, kufanyakazi kwa pamoja na kila tatizo litakalotokea tutalirekebisha kwa madhumuni ya kuimarisha Muungano na kuendeleza mbele Tanzania yetu.

Baada ya maelezo haya Mhe. Naibu Spika nakushukuru sana. *(Makofi).*

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru, namshukuru Mwenyezi Mungu vile vile na mimi kunipa nafasi hii ya kusimama hapa. Niuungane na wote waliochangia hoja hii nimshukuru sana Mwanasheria mkuu nimshukuru Waziri wa Nchi Ofsi ya Makamu wa pili wa Rais kwa maelezo yao.

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka nitangaze hapa hadharani si mwanasheria, *by profession* ni mwalimu *Professor* Kabudi yeye ni Mwanasheria kabobea Chuo kikuu, lakini uongozi unataka hekima na busara zaidi. Unaweza ukawa *professor*, unaweza ukawa *doctor*, unaweza ukawa vyovyote vile ulivyo ukikosa busara na hekima basi mambo utayaharibu. Mimi nimewahi kukutana nae mara moja na nikamwambia sana kwamba Waziri nakuomba sana fanya siku uje Zanzibar tukutane tuzungumze, kwa maelewano ya kuimarisha Muungano wetu, akanambia sawa nitafanya hivyo kachelewa hakuja mpaka leo ndio maana yake zinakuja kauli kama hizi.

Sasa kuna mtu alinambia hakuna kero za Muungano lakini kuna watu ndio kero za Muungano zenyewe, sasa hawa wengine baadhi ya mawaziri hawa wamekuja na mambo kama yanatuharibia muungano wetu haileti tija. Viongozi Wakuu wote tokea wakati wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alishirikiana vizuri na viongozi wote, Mzee Mwinyi, akaja Rais BenjaminWillian Mkapa, Rais Mstaafu Kikwete, akaja Mhe. Rais John Pombe Magufuli wote wanasaidiana wanashirikiana wanaheshimiana na Rais wetu wa Zanzibar. Sisi Rais wetu wa Zanzibar tunampenda na tuna imani naye hatutokuwa tayari kwamba atokee Waziri kumdhalilisha Rais wetu au kuidhalilisha Serikali yetu hilo haliwezeni kabisa.

Kwa hivyo mimi nadhani mwezangu huyu Waziri wa Katiba na Sheria ni mpya bado hajaelewa siasa za Tanzania kuna haja kubwa ya kujifunza zaidi siasa za Tanzania ili aweze kwenda sambamba na utaratibu wetu. Kwa hivyo naomba sana kwamba tushirikiane kujenge nchi yetu na Katiba iko *very clear* imesema vizuri kwamba Tanzania imeundwa kwa nchi mbili, yaani Zanzibar ni miongoni mwa nchi mbili huru zilizoungana pamoja na Tanganyika zikafanya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katiba iko *very clear* kwamba hii ni serikali kamili ina uongozi kamili na kila kitu haiwezekani sasa akatokea mtu yoyote akaidhalilisha Katiba yetu Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika baada ya hayo naungana na wenzangu wote na inshaallah naomba kuwasilisha.

Mhe. NadirAbdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Naibu Spika, namshukuru kwanza Mwenyezi Mungu na kukupongeza wewe kwa kunipa nafasi hii tena, kwanza niwapongeze sana waliochangia wote, maana mimi niloinuka ni mwanafunzi, lakini wakainuka walimu wote kunisaidia naomba sana niwapongeze kwa mipango yao mizuri na fikra zao nzuri walizozitoa na mimi nimepata kusoma zaidi kwenye haya waliyochangia, nimtambue tu:-

1. Mhe. Hamza Hassan Juma
2. Mhe. Miraji Khamis Mussa
3. Mhe. Mwanasheria Mkuu
4. Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais
5. Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora.
6. Mhe. Ali Khamis Bakari kachangia kwa maandishi kasema na yeye analaani jambo lile.

Mhe. Naibu Spika, kama walivyosema wazee wangu wote na walimu wangu atakae mdharau Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohamed Shein katudharau wazanzibar, katudharau wawakilishi wote humu ndani tunataka heshima irudi.

Mhe. Naibu Spika, haya kama walivyoeleza baadhi ya Wajumbe, lazima Katiba ziheshimike lazima waangalie wazee wametoka wapi hakuna Tanzania, kama ingekuwa sio Zanzibar. Wakati huo kuna Tanganyika na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar. lazima Mawaziri wanapoingia lazima nao wajifunze nidhamu ya kuzungumza na viongozi wakubwa katika nchi hawawezi tu wakaanza kuropokwa ropokwa wakati hapa kuna Rais inamlinda Katiba. Kuna mambo ya Muungano wapo pamoja lakini kuna mambo ambayo hayapo kwenye Muungano Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi yanamuhusu yeye moja kwa moja.

Mhe. Naibu Spika, ningeomba Serikali ichukue hatua na ikiwezekana aombe radhi Waziri yule kwa mambo aliyoyazungumza ambayo yapo kinyume katika Sheria na Katiba ya Nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Sasa niwahoji Wajumbe,Wanaokubaliana na Hoja ya Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy, wanyooshe mikono, Wanaokataa, Wanaokubali wameshinda.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy na mimi nichukuwe fursa hii kukupongeza kwa hoja yako na niiipongeze Serikali vile vile kwa majibu mazuri sana na basi nadhani sana wananchi wengi wamesikia kwa sababu ni hoja ambayo ikizungumwa sana, kwa hiyo tunafikiria kwamba hayo ambayo yamezungumzwa mengine yatafanyiwa kazi.

Waheshimiwa Wajumbe, sasa tunaendelea na utaratibu wetu wa *order paper* yetu.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria kufuta Sheria ya Adhabu, Kutunga Sheria mpya ya Adhabu na kuweka Masharti Bora zaidi pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nilikuwa na majina yasiozidi sita kwa wale wanaotaka kuchangia mswada huu, wengine wameniomba wawili lakini nataka kusema hivi, Wajumbe ambao watachangia sasa nitakaowataja naomba watumie dakika tano tano tu zinawatosha kabisa. Halafu baadae nitaanza na Waheshimiwa Mawaziri. Mchangiaji wa kwanza atakuwa Mhe. Jaku Hashim Ayoub, atafuata Mhe. Nadir na baadae atafuata Mhe. Hassan Diaspora.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana na mimi nitajitahidi kutumia dakika tano kama ulizonipa. Nianze kidogo kwa kutoa hadithi: *"Manrran-minkum mukran falyughiru biyadihi faman-yastatiu wafibidisanihi waman yastatigh wabi-kablihi wazalika – abahu liman"*.

Mhe. Naibu Spika, kuna kitu kimegusa dini humu ndani kidogo na ndipo nikachangia lakini nisingeinuka, na kama inavyosema mwenye kuliona baya aliondoe kwa mikono yake ama kwa ulimi mwisho achukie kifungu 108(a) Mwanasheria, DPP kidogo elimu yangu ni ndogo mimi nataka nielimishwe 108(a) ambae si mke wake, au mke wake ambae atatenganishwa na kisheria bila ya ridhaa yake wakati wa maingiliano kingono. Sheria hii naijua

mimi Waislamu haiwahusu, waislamu hupatanishwa, hawatenganishwi. Waislamu hupatanishwa kama nimegombana na mke wangu hatutenganishwi ni kupatanishwa. Wenzetu wakristo na dini mbili nnazozijua mimi kubwa hapa ni Waislamu na Wakiristo, kuna *separation*, kutenganishwa hii nafikiri ndio inayowahusu. Likishindikana hilo unaitwa *divorce* talaka, kwa hii Mwanasheria Mkuu, na DPP kakifikiria kifungu hicho kukiondoa, nchi hii inawaumini asilimia tisini na tisa waislamu.

Hii kauli ya kutenganisha ni fitina tutafute njia watu wamegombana kupatanisha, ni fungu kwa Mwenyezi Mungu ni kifungu kikubwa sana, ulimi ni sadaka , kwa hii hichi ambae si mkewe au mkewe ambae ametenganishwa nani anatenganisha mtu na mkewe ni makosa, kutenganishwa na mkeo, mtafute njia na hupewa talaka moja na una haki ya kumrudia ndio hapa nimeguswa sana Mhe. Naibu Spika, kifungu hiki mimi sitounga mkono pamoja na elimu yangu kuwa ndogo unaambiwa jambo ukiliona baya utumie mkono wako, ulimi wako na mwisho imani dhaifu ndio paliponigusa zaidi hapa Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, nije sehemu ya pili ya eneo la matumizi ya sheria, hapa kidogo Mwanasheria, na DPP tusaidiane. Mamlaka ya Mahkama ya Zanzibar kwa madhumuni ya sheria hii ni sehemu yote ya ndani ya Zanzibar na sehemu yake baharini na makosa yatotendwa kwenye bahari kuu katika vyombo visivyosajiliwa, hapa nitahitaji nipewe maelezo, hapa nisikilize kwa makini. Mwanasheria Mkuu na DPP, tunatunga sheria hizi halafu tunakuja kulaumu, tunamtaja Kabudi bure humu wakati mwengine, tuwe wa kweli tunajitungia sheria humu ndani ya Baraza kuna watu walishtakiwa wakawa mahaini kuna waziri alishtakiwa, kwa hivyo hizi sheria tunapozozitunga tuwe wakweli sisi kuja kutusokota mbele tunakuja kutafuta mchawi mchawi, mchawi nani? Sisi wenyewe. Kifungu hichi tuna Mahakama zetu, tuna DPP wetu tuna AG wetu halafu tunakuja kulalamika

tunamlalamikia nani. Kifungu hichi mimi aa! Mnatupa wakati mgumu wakati mwengine sisi tuliopo Dodoma kule, tuna Mahakama zetu leo anakamatwa mzanzibari anapelekwa Bara tena inamhukumu Mahkama ile ile ya Mkoa anatolewa hapa anapelekwa Bara, hatuna Mahkama ya Mkoa, AG, DPP hatuna Mahkama ya Mkoa, halafu tunalalamika tunamlalamikia nani tunajidhulumu wenyewe.

Serikali muwe makini viongozi mlioko mbele muwe makini, tatizo letu mkataka kufahamishwa na sheria utaambiwa chama fulani, hatuwezi kwenda tuwe wakweli viongozi mnaokaa mbele, watu wanapelekwa Mahkama ya Mkoa Dar es Salaam ndio wanaoshtakiwa mali ile ingebaki Zanzibar,si ingetusaidia. Leo tunapiga kelele wakati mwengine tunajipeleka wenyewe tujitungie sheria ambazo zinotusaidia nchi yetu mimi. Mimi nilikuwa nikinuka sana katika Bunge la Jamhuri ya Muungano kwa maslahi ya Zanzibar wala sifichi huyu Kabudi nimezungumza mimi juzi tulisokotana sana ndani na mkiitafuta *hansard* mtaiona tulisokotana sana kwa maslahi ya Zanzibar. Ubaya wenyewe Katiba hii hapa ya Jamhuri ya Muungano, na kiti alikalia Chenge.

Kifungu cha 64:

> "Endapo sheria yoyote iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi inahusu jambo lolote katika Tanzania Zanzibar ambalo lipo chini ya Mamlaka ya Bunge, sheria hiyo itakuwa batili na itaanguka na pia endapo sheria yoyote iliyotungwa na Bunge inayohusu jambo lolote ambalo lipo chini ya mamlaka ya Baraza la Wawakilishi sheria hiyo itakuwa na batili na itaanguka".

Tunafanya nini, si maneno yangu haya Katiba ya Jamhuri ya Muungano. Kwa hiki kifungu tuna DPP wetu, tunae AG wetu, kifungu hiki lazima kifanyiwe marekebisho. Na atakaempeleka

mtu huko tutafute njia za utaratibu, kifungu hiki AG uje unieleze, DPP mje mtufahamishe, tunae AG wetu tunae DPP wetu, tuna Magereza yetu, utachukuaje mtu umpeleke kule, hili silifahamu na kila mmoja na muono wake.

Mhe. Spika, nije katika kifungu cha 27 mtu ambae anapanga, anaeanzisha, anaezusha na anaekusudia tendo lolote la jambo la dhana kueleza kwamba kutamka na kutangaza mambo ya kuanzisha, kuzusha na kukusudia huko, kuchapisha chapisho lolote na maandishi kwa tendo lolote dhahiri kuwa tendo lolote ambalo linalokusudia kuleta na kusababisha kitendo au kuleta mabadiliko ya Serikali kinyume na utaratibu wa Katiba, atakuwa ana makosa. Hizi sheria tunazotunga humu ndani, kuna kesi *Criminal application* namba nane Machano siyo Mwenyekiti wa Kamati aa siye.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa umebakisha dakika moja.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kuna Machano na wengine nasema humu ndani wengine leo Mawaziri, wameshitakiwa katika kesi ya uhaini sasa hayo mambo hivi aliyekuwepo mbele mngoje chini. Baada ya mauti kuna uhai, baada ujana kuna uzee. Hivi vyeo tunapita kesho hatupo watakuja wengine hizi sheria tukizitunga mbovu tusije tukatafuta mtu mwingine tunajitungia wenyewe, hizi sheria tunazozitunga, halafu tunamtafuta Kabudi, Kabudi katukosa nini, sisi tuziangalie mambo humu ndani, leo mtu Waziri alikuwa katika kesi ya uhaini Machano na wenziwe sijui kumi na saba wale au kumi na nane na wengine wakawa Mawaziri humu ndani tuziangalie sheria.

Mhe. Naibu Spika, jengine kwa kumalizia 52, hapa Mhe Rais kama mnataka kumshusha cheo chake.

Kifungu cha 52:

"endapo jumuia itatangazwa na kukosa jumuia halali kwa amri ya Rais mambo haya yatavunjwa yatahusika"

hapa atafutwe mtu tu Rais hapa kumshusha hadhi yake hakuna AG kutumia kipengele hiki. Rais ana mambo mengi na hiki sitaki maelezo, hii ni jumuiya tu jumuiya Mwanasheria au DPP anaweza akaifuta. Leo mpaka Rais ana majukumu mangapi Mhe. Rais, hamkuliona kitu kama hiki kumpa Mhe. Rais, angalia AG, 52 haya si majukumu ya Mhe. Rais kumshushia hadhi.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa muda umekwisha.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi nikushuru.

Mhe. Naibu Spika: Kama utakuwa na mchango mwengine naomba upeleke kwa maandishi.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Ahsante Mhe. Naibu Spika, Mimi nafikiri ntaongea dakika mbili tu kwa sababu sitaki kuchangia isipokuwa kwa kuwa mjumbe wa kamati hii nitaomba kuongea machache tu. Nitaomba nichangie mswada huu wa sheria wa kufuta sheria ya adhabu na kutunga sheria mpya ya adhabu.

Mhe. Naibu Spika, kwanza mimi niipongeze sana Wizara kwa ujumla kuanzia Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu wote, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, pamoja na wanasheria na DPP, kwa kushirikiana nao vizuri sana kwenye kukubaliana kwenye masuala ya sheria ambazo sisi tumeona zina umuhimu sana, na niwahakikishie wananchi mmoja anaeongea humu ndani kuhusiana na suala la sheria liwe ngumu na adhabu kali mmoja ni mimi nikiwa ni Mwakilishi wa Jimbo la Chaani. Ninachotaka kuwahakikishia Wajumbe wenzangu, adhabu

tulizozipendekeza za safari hii ni nzuri sana na ziko kali sana, kama watapoangalia nyuma na hizi zinazokuja basi mambo yanakwenda vizuri. Kwanza adhabu ya kifo hatujaiondosha, itakuwepo *you never no* nani atakuja kuwa Rais mbele ataitumia.

Mwenyezi Mungu akinijaaliwa nikija kuwa mimi Rais nitafata mienendo ya Mhe. Mzee Ali Hassan Mwinyi Rais Mstaafu alijitahidi nae kuchukua hatua hizi ili kukomesha na mimi ntamfata yeye mzee wangu. Sasa ndio maana ukakuta suala la kunyonga hatujaliondosha, lakini vile vile sheria nyingi tulizozipendekeza ziwe za kifungo cha miaka ishirini na tano, miaka thelethini, nyingine maisha. Haya yote yanatokana na mwenendo mkubwa ambao ulokuwa ndani ya nchi hii kwamba tumeona kuna mambo mengi yanaharibika na watu wanacheza na sheria wameona tu sheria ndogo ndogo sheria nyepesi analipa fidia, lakini sasa hivi kuna sheria nyingi hazina dhamana. Sheria za Madawa ya kulevya, mtu atakaebaka, atakaedhalilisha, mtu atakaekamatwa mwenye jinsia moja zote zimeondoshwa dhamana.

Mhe. Naibu Spika, na hii nitawaomba sana Wawakilishi wenzangu tuipitishe na tushauri na tuipitishe kwa nguvu zote sheria hizi, kwa kweli sheria ni nzuri, huko mbele tukiona kunahitajika ziada tutaitana tena tutakaa tena kama watu wanavyokaa katika vikao vya kubadilisha na sisi wenyewe ndio tunaobadilisha sheria na kutunga.

Mhe. Naibu Spika, mimi kwa kweli nimefurahika sana na nikiwa mjumbe wa kamati hii nitahakikisha sheria kali zote zinakuja Zanzibar na zinapita kwa uwezo wa Mwenyezi mungu na zinatekelezwa, mimi niwapongeze sana tu Wizara tunapopitisha hapa waweze kuja kuzifanyia kazi na huko nje tuone kwa vitendo na siyo kwenye makaratasi.

Mhe. Naibu Spika, naunga mkono hoja ya mswada huu nakushukuru sana.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kukupongeza wewe kwa kunipa nafasi ya mimi kuchangia mswada huu muhimu uliowasilishwa na Serikali kufuta sheria ya adhabu na kutunga sheria mpya ya adhabu.

Mhe. Spika kama tunavyojua adhabu ni kitu kichowekwa hata na Mwenyezi Mungu, adhabu lazima itekelezwe pale mtu anapotenda kosa na ikithibitika kweli ametenda kosa lazima aadhibiwe. Imo katika vitabu vyote vya dini adhabu hata ya kifo imo kunako msahafu na vitabu vyengine vya dini.

Mhe. Naibu Spika, mimi nitachangia ukurasa wa 283 kifungu 27 uhaini na makosa mengine dhidi ya Serikali, Mhe. Naibu Spika, kama tunavyojua kwamba majukumu ya sisi viongozi wa Chama cha Mapinduzi Zanzibar hasa vijana ni kuhakikisha kwamba tunayalinda Mapinduzi matukufu pamoja na kuulinda Muungano wetu, narudia tena tunayalinda Mapinduzi matukufu ya Januari 1964 ambayo yamekuja na maslahi ya kuwatetea wakwezi na wakulima kwa maendeleo ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, tunapozungumza uhaini lazima tujue nini maana ya uhaini, Mhe. Naibu Spika uhaini ni yale mambo ambayo mtu au kikundi cha watu kimekusudia kwa mfano kuipindua Serikali au kumuua kiongozi wa Serikali au kufanya jambo lolote baya zaidi dhidi ya Serikali au na mambo yanayohusiana na hayo, huyo ndie anaitwa haini au watu hao ni mahaini.

Mhe. Naibu Spika, nchi nyingi duniani kesi hii ya uhaini imewekewa adhabu ya kifo, kwa nini imewekewa adhabu ya kifo, kwa sababu haitakiwa uthubutu wala ufikirie kutaka kumpindua

kiongozi au uongozi ulioko madarakani kwa kutumia aina yoyote ile kumuua au kuwaua au kufanya lolote. Sasa 27 katika hii sura ya 6 imeweka makosa ya uhaini.

Mhe. Naibu Spika, lakini naomba kusema leo tupo Baraza la Wawakilishi la Zanzibar tunatunga sheria ya kufuta sheria ya adhabu na kuweka sheria mpya ya adhabu na tumeiweka uhaini, na kwa kumbukumbu nilizonazo Zanzibar imeshatokea uhaini. Uhaini uliotokea Zanzibar wa kwanza walimuua Mwanamapinduzi hayati Mzee Abeid Amani Karume, na watu wale walihukumiwa na kesi ya uhaini, nakumbuka kama sikosei ile kesi ilikuwa na Nurubhai Issa Nurubhai na wenziwe. Lakini leo pia Zanzibar Mhe. Naibu Spika, ilitokezea kesi nyingine ya uhaini ambayo naomba kuisoma ya tarehe 8/2000. SMZ *vice* Machano Khamis Ali *and other eighteen.* Hii ilikuwa ni kesi ya Machano dhidi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na watu wengine kumi na nane.

Mhe. Naibu Spika, huyu si Machano Mwakilishi, si Machano Othman Said huyu ni Machano mwengine maana yake mwenyewe ameshituka hapa siyo yeye, Machano mwengine na ndie aliyehukumiwa na kesi ya uhaini na wenziwe kumi na nane.

Mhe. Naibu Spika, lakini baada ya kesi hii kuhukumiwa, ndio maana leo nasema hiki kipengele ni muhimu lakini tukiangalie vyema, baada ya kesi hii kama ulivyo utaratibu wa kesi nyingine zinaposhinda katika Mahakama hizi unaweza kukata rufaa Mahakama nyingine. Watu hawa Mhe. Naibu Spika, wakakata rufaa katika Mahakama inayoitwa Mahakama ya Rufaa. Kufika Mahkama ya Rufaa Mhe. Naibu Spika, naomba nisome:

"*For the reason given above, we have revealed a nation we have found that the treason cannot be committed against a sovereign"* kwamba haiwezi kutokea Mapinduzi *committed*

against a sovereign in Zanzibar. "However a treason is a brench of security which in the United Republic union matter. Therefore the sovereignty is a United Republic not Revolution Government of Zanzibar". Yaani kwamba Mapinduzi hayawezi kutokezea katika Zanzibar yanaweza kutokezea katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tu.

Akaendelea kusema *"The Head of Zanzibar or Head of the Executive Zanzibar Tanzania who is also called President of Zanzibar"*. Kwa tafsiri wanasema Mapinduzi hayawezi kutokezea Zanzibar wala kwa Kiongozi wa Zanzibar, yanaweza kutokezea kwa Kiongozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Leo mmetuletea Sheria ya Serikali hapa kwamba tunapitisha uhaini nae pia ahukumiwe. Lakini haini huyu inayomjua Zanzibar ni haini akifika Mahakama ya Rufaa kwa mujibu wa taratibu na *case study* hii, wale waliosoma sheria wanajua inaitwa *case law* hii anakwenda kuachiwa kama walivyoachiwa hao.

Sasa leo mmetuletea sheria kwamba alofanya jambo la uhaini ahukumiwe Zanzibar, lakini akishahukumiwa Zanzibar akifika huko Bara kunakoitwa Mahakama ya Rufaa anaambiwa wewe hujakuwa haini, kwa sababu Zanzibar haiwezi ukatokezea uhaini, wanaume hawa watatu walikaa wakaamua hivyo wanavyojua wenyewe sheria zao sijui wamesoma wapi kwamba Zanzibar haiwezi kutokezea uhaini na sababu zao wamezitoa hizi zipo hapa, ukienda ku-*search* kesi ya Machano na wenziwe kumi na nane utazikuta. Machano yule siyo Machano Othman Said.

Kwa hiyo ninachokiomba, Zanzibar ni Nchi kwa mujibu wa Katiba sehemu ya kwanza, lakini sehemu ya 26 ya Katiba ya Zanzibar kutakuwa kuna kiongozi wa Serikali wa Nchi ya Zanzibar ambae ni Rais.

Mhe. Naibu Spika, sasa leo kama kiongozi wa Serikali ambaye ni Rais kafanyiwa jambo lolote baya aidha kapinduliwa au kawa *threaten* kupinduliwa aidha kauliwa, lakini kwetu sisi tunamjua huyu haini. Lakini akifika Bara Mahakama ya Rufaa anaambiwa huyu si haini. Ibara ya 102 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inamtambua Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ni nani. Lakini bado Mahakama ya Rufaa inamuachia mtu ambaye kataka kuipindua Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, mimi niliezaliwa na nikaambiwa na bibi yangu mengi lakini moja niliambiwa uyalinde na uyatetea Mapinduzi Matukufu ya Januari 1964, jambo hili sikubaliani nalo kwamba Zanzibar tunataka kupinduliwa au kuna mtu anataka kumuua Rais wetu amefanya vyovyote vile, lakini akifika Bara anaachiwa anambiwa huyu si haini. Kwa hivyo, Zanzibar kesi ya Uhaini haipo.

Mhe. Naibu Spika, naomba sana hawa wanasheria wajuaji wajanja wanaojua wakae hichi kipenge kifutwe kisiende Bara hichi kimalizie mwisho Chumbe hapo hapo Vuga. Kama mtu kahukumiwa uhaini Zanzibar na kweli Zanzibar ime-*prove* wanasheria wake huyu ni haini basi tena huyu asipelekwe Bara kwa sababu atakwenda kuachiwa kwa sababu hii *case law* ndio ipo na itabakia milele 18 wameshaachiwa. Kwa maana hiyo naomba iseme kwamba kesi zote ambazo zitashindwa Zanzibar zitakuwa na uwezo wa kwenda Mahakama ya Rufaa isipokuwa kesi ya uhaini. Kwa sababu kesi ya uhaini kule Bara wanakwenda kuachiwa, wanaambiwa si haini na hoja zao inakuwa kwamba kule Zanzibar huwezi mtu kufanya uhaini na sababu zao wameziweka.

Hapa Mhe. Naibu Spika, itakuwa tunayakosea na tunayakashifu Mapinduzi matukufu.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa muda wako umekwisha.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Nashukuru Mhe. Naibu Spika, namaliza.

Kuzipeleka kesi za uhaini katika Mahakama ya Rufaa itakuwa hatujayatendea haki Mapinduzi, itakuwa hatujayalinda Mapinduzi wala hatuyapendi Mapinduzi na sisi wengine tumekula kiapo ya kuyapenda, kuyalinda na kuyatetea Mapinduzi.

Mhe. Naibu Spika, kwa heshima kubwa namuomba Mwanasheria Mkuu naamini kwa hili hatukuja na sheria zake nyingi, lakini na yeye namjua ni Mwanamapinduzi kwa hiyo kesi ya uhaini haitokwenda tena Mahakama ya Rufaa kwa sababu nitaomba Wajumbe wenzangu wa Baraza la Wawakilishi hapa tusikubali kesi ya uhaini ipelekwe Bara kwa sababu wanakwenda kuachiwa na uhaini kama umetokea Zanzibar.

Baada ya haya machache Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha huku nikitoa msimamo wangu waziwazi siko tayari kuona kesi ya uhaini inakwenda Mahakama ya Rufaa.

Naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri asiyekuwa na Wizara Maalum: (Mhe. Said Soud Said): Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi kuchangia mswada huu.

Kabla ya yote kwanza naunga mkono mswada huu mia kwa mia na sababu za msingi za kuunga mkono mswada huu kwanza nachukua nafasi ya kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kusimamia vyema misingi ya Katiba na Utawala Bora kwa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, kwanza ningeomba jambo zuri sana kwa watunga Sheria wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kuzingatia mila na desturi za Wazanzibari na kwenda sambamba na mazingira yanayoikumba Zanzibar ili Zanzibar iendelee kulinda heshima yake ya asili ya Wazanzibari.

Mhe. Naibu Spika, nachukua nafasi hii kuwaomba Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wachukuwe fursa ya kuwaeleza Wazanzibari wote juu ya mabadiliko ya sheria hii, ili wananchi wa Zanzibar wapate nafasi ya kuelewa kwamba sasa Zanzibar imechoka kuvumilia vitendo vya udhalilishaji na inapambana na watu wote watakaochukua mila na desturi za nchi za Magharibi na kuzileta katika nchi yetu kwa ajili ya kupotosha utamaduni wetu. Kwa vile, watu wetu wana tabia ya kusikiliza na kuachia.

Lakini sisi kama Wawakilishi iko haja ya kuchukuwa fursa ya kuwaleza Wazanzibari kwamba sasa umefika wakati wa kukomesha vitendo vya udhalilishaji wa watoto, umefika wakati wa kukomesha vitendo vya udhalilishaji wa wanawake, umefika wakati wa kukomesha vitendo vya jinsia moja, umefika wakati wa kuifanya Zanzibar irudi kwenye mila na desturi za nchi hii. Ndio maana sasa, kamati ya Baraza la Wawakilishi ambayo ilikuwa inajadili sheria hizi ikaona kwamba iko haja ya kufanya mabadiliko makubwa ya kuongeza adhabu na mimi nasema kwamba yule ambaye angekuwa atapatikana na kosa la kubaka amembaka mtoto mdogo wa miaka mitatu mpaka miaka kumi na nane, basi licha ya kufungwa miaka thelathini lakini ingekuwa pia anahitaji kufanyiwa utaratibu wa kuhasiwa. Ili akirudi awe hana uwezo wa kufanya lolote na awe anahasiwa kila mwezi kule jela, apigwe masindano ili akitoka awe hajifai kabisa. Kwa sababu ni aibu Zanzibar kwa matendo yanayofanywa katika kipindi cha mazingira tunayokwenda nayo. Wanaitia aibu Serikali wanalitia aibu taifa la Wazanzibari bila ya kuzingatia kwamba dini zote zinakataza mambo kama hayo.

Mhe. Naibu Spika, Serikali inayoongozwa kwa misingi ya sheria na katiba, mara nyingi sana inahitaji kuona wananchi wake wanaishi katika maisha bora ambayo hayaambatani na vurugu wala matatizo. Ndio maana leo tukafika pahala tukasema ipo haja sasa kutunga sheria ili na watoto na wao waweze kupata haki yao ya msingi kama vile tulivyopata sisi wakati tulipokuwa watoto, kwa vile adhabu zinazotolewa au zitakazotolewa maana yake ni kulinda taifa lijalo ili liweze kuishi kama vile wazazi wao walivyokuwa wakiishi.

Mhe. Naibu Spika, mchango huu mimi naamini hauna mabuti wala hauna vikwazo kwani kila mmoja humu ni mzazi na kila mzazi anahitaji kuona mtoto wake hapati matatizo kama hayo ambayo yamezuka. Kwa hivyo mimi nachukua nafasi hii kuwapa pole wazazi wote ambao watoto wao walifikishwa na matatizo kama hayo na Serikali yao sasa iko tayari kupambana na matatizo kama hayo. Kwa vile kimsingi tunasema kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar italinda mila na desturi za Zanzibar sambamba na mazingira yaliyopo hivi sasa.

Mhe. Naibu Spika, siku zote Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi amekuwa akitoa haki za msingi kwa raia wote wa Zanzibar, wazazi, walezi, watoto na hata wazee ambao hawajiwezi tena. Sasa na sisi tunaomba sheria hii bila ya kusita aitie sahihi mara moja ili adhabu kali zitolewe kwa watu wote watakaokamatwa na vitendo kama hivi, kama sheria inachukua siku ishirini na moja basi mimi naomba hata siku tatu isifike itiwe sahihi ili watu wote waliokuwa wanafanya vitendo vya unyama kama huu adhabu kali zichukuliwe ili kuikomesha jamii na mpango huu ambao wameuanisha kwa makusudi ni aibu kwa taifa la Tanzania, ni aibu kwa Taifa la Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, ahsante sana huo ndio mchango wangu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana nakushukueu Mhe. Said Soud mchangiaji wetu anayefuata ni Dkt. Sira Mamboya.

Mhe. Waziri asiyekuwa na Wizara Maalum (Mhe. Dkt. Sira Ubwa Mamboya): Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, pia na mimi kunipa fursa hii niweze kuchangia Mswada huu ambao ni Mswada muhimu Mswada wa Sheria ya Adhabu 2018.

Mhe. Naibu Spika, tulivyofahamishwa kwamba hii ndio Sheria mama ndio sheria muhimu kwa usalama wa nchi yetu ya Zanzibar, wakati tunaelekezwa tumefahamishwa hivyo na sisi kutokana na yaliyomo tumefahamu. Mhe. Naibu Spika, sheria hii imebeba sheria zote, hasa ikizingatiwa kwamba kila kosa la jinai limetajwa ndani ya sheria hii. Kwa hivyo yale yote tuliyokuwa tukiyalalamikia kwenye sheria hii mpya mambo yamerejekebishwa na sasa hivi imeleta sura nzuri na matumaini kwa wale ambao waliokuwa wanakosa haki.

Mhe. Naibu Spika, mimi ningependa kuanza na sura namba 6 nitoe mchango wangu katika sehemu hii, kwa sababu kama tunavyofahamu kipengeleza hichi tafsiri ya sita kinazungumzia uhaini wa makosa mengine dhidi ya Serikali. Kati ya wale waliotazaliwa kabla ya Mapinduzi na wakayaona Mapinduzi wakiwa na fahamu zao mimi ni mmoja wapo. Kwa hivyo msinitizame kwa wembamba wangu mkafikiria ni mdogo ni mzee hasa lakini najitahidi, wakati Mapinduzi yanafanywa mimi nina miaka kumi. Baba yangu alikuwa ni mmoja kati ya hao watu ambao walioshiriki lakini sio kwa dhahiri kwa sababu wakati huo wasomi na wafanyakazi wa Serikali walikuwa hawaruhusiwi lakini nilikuwa naziona pirika pirika zinazoendelea pale kwetu na watu wanaoingia na kutoka.

Nalikumbuka tukio moja ambalo lilitokea kabla ya Mapinduzi wakati Mzee Abeid Karume alipotoka Dar es Salaam akafikia

Kizimkazi, baba yangu akampakia kwenye gari alikuwa muafrika wa mwanzo mwenye gari, akenda nae mpaka Bungi, akaja baba yake Waride Bakari Jabu akampokea pale na kwa muda wa siku tatu hakurudi nyumbani.

Nilikuwa namuona bibi yangu kila siku analia anasema mwanawe hatorudi, nilikuwa sifahamu kwa nini. Lakini baadae nilielewa kilichokuwa kinaendelea, kwa sababu si muda mrefu Mapinduzi yalifanyika na tukafungwa vitambaa vyeupe mikononi hilo tukio nalikumbuka mpaka leo, ilikuwa ni wakati wa skukuu mambo yale yalitokea Mwezi wa Ramadhani na sikukuu lakini sikukuu mwaka ule hatukula kwa sababu kulikuwa hakukutulia. Kwa hivyo nayakumbuka Mapinduzi na ninayafahamu. Sasa kutokana na hilo sisi wengine tumekuwa katika mikono ya wana Mapinduzi tumesomeshwa na wana mapinduzi, tumesomeshwa na Serikali ya Mapinduzi mpaka nilipofikia kusoma. Kwa hivyo nina haki ya kuyatetea na kuyalinda Mapinduzi kwa nguvu zangu zote. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nimefanya hivyo na nitaendelea kufanya hivyo mpaka siku yangu ya kufa, historia ya Mapinduzi kwetu haikuanza hivi hivi na hayakuja tu Mapinduzi kwa sababu Serikali watu walikuwa wanataka waipindue kulikuwa na dhulma inafanyika dhidi ya waafrika kwa kipindi hicho. Kwa hivyo walijaribu mara nyingi kwa miaka mingi chaguzi nyingi zilifanyika kuanzia mwaka 1957 mpaka mwaka 1963, majaribio ya chaguzi nyingi waafrika walishinda lakini hawakupewa haki yao. Kutokana na hilo ikafika pahala wakasema tumechoka sasa tuchukue Serikali kwa nguvu hiyo ndio sababu ya Mapinduzi.

Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, kifungu hichi kukaa sisi kama wana Mapinduzi kama watoto wa wana Mapinduzi tukakaa tukawa labda hatukipi uzito unaostahiki kama ilivyo kwenye sheria tutakuwa hatutendi haki, kwa hivyo tuko pamoja na

walioitunga sheria hii hasa kwa kipindi hichi tutayalinda kwa nguvu zetu zote kama vile ambavyo watoto au vijana wa siku hivi wanavyosema tutafanya kazi kuhakikisha kwamba mapinduzi yanalindwa. Hatutokua tayari kwa wale ambao wanaotaka kujaribu kuondosha Mapinduzi. Kwa sababu mengi tu yamefanyika lakini kutokana na sheria zetu kuwa zilikuwa zinapwaya hazikuwa na meno ya kukabiliana na yale yanayotokea ndio maana kuna wale ambao wameweza kujaribu mtu unatangaza tu ata kama hujatangiziwa, Tume haijasema wewe unasema umeshinda tu kwa sababu ilikuwa sheria zetu zilikuwa zinapwaya. Lakini kwa sheria hii ninafikiri sidhani kama kuna mwengine tena atakayethubutu kufanya anavyotaka.

Mhe. Naibu Spika, niendelee kuangalia na vifungu vyengine kuna kifungu hapa sehemu ya kumi na tatu kinachozungumza makosa dhidi ya maadui. Kifungu hichi kina sehemu nyingi ambazo zimeguswa mimi ningependa nianzie kifungu 107, 108 mpaka nifike 116. Katika maeneo haya kwanza nishukuru kwa sababu hatimae kilio cha wawakilishi wanawake kimesikika wanawake wa Baraza tulikaa pamoja tukifahamu jambo hili na hatimae hoja binafsi ililetwa, ilipoletwa hapa kwa umoja wetu tuliipitisha na kilichokuwa kikielezwa kwamba tumechoka na yanayotendeka hasa kuhusu masuala ya udhalilishaji.

Tuishukuru Serikali yetu imejitahidi sana kupiga kelele imelaani, imechukua hatua nyingi lakini kwa vile sheria zilikuwa bado hazijakaa vizuri mambo yanatendeka na ndio kwanza mkoko unaalika maua. Sasa ni matumaini yetu kwamba sasa hivi baada ya kupitishwa sheria hii masuala yale yatakuwa kwa kiasi fulani yamedhibitiwa na yule yoyote atakayejaribu atakumbana na mkono wa Sheria kwa sababu sheria zimesharekebishwa na hali halisi sasa hivi haitoruhusu.

Mimi nasema suala la udhalilishaji si zuri si kwa mwanamme wala si mwanamke, sheria hapa imepanga vikundi maalum, wanawake mbali, wanaume mbali lakini mimi naona wote ni binaadamu, hakuna anayetakiwa kudhalilishwa si mwanamme wala si mwanamke sote ni watu ambao tunatakiwa kupata heshima, kuheshimu wenzetu, kuheshimu afisi na kuhakikisha kwamba kwa wale wanaotendewa yale yasiyostahiki wanapata haki zao. Ingawa utakuta kwamba wanawake mara nyingi wanadhalilishwa wakiwa wadogo mpaka utu uzimani kwao, wanaume wanadhalilishwa lakini mara nyingi wakiwa wadogo.

Wengine wanapokua mungu anawajaalia hawaendelei na yale kwa sababu hawakuwa wanayafanya isipokuwa walikuwa wanalazimishwa kufanya. Wengine kwa bahati mbaya wanaendelea tena na maisha yao yote wanakuwa katika utaratibu kama ule haipendezi wala hatufurahi kuona kwamba tu asiyestahiki kuwa mwanamke anakuwa mwanamke, asiyestahiki kuwa mwanamne anakuwa mwanamme asiyestahiki kwa zote pande mbili anafanya visivyokuwa mungu ambavyo alivyoumba, mungu hakuwa na makosa kutuumba wanaume na wanawake alikuwa ana sababu zake na tulitakiwa tuishi hivyo.

Ukiwa mwanamke uwe mwanamke, ukiwa mwanamme uwe mwanamme kwa hivyo ukiwa unafanya tofauti na hivyo unakwenda kinyume na yale ambayo tulitarajiwa kuyafanya, kwa hivyo mimi ninashukuru kwamba angalau tumepata sheria sasa za kuweza kuyadhibiti hayo na hatua itachukua mkono wake.

Nikiangalia kifungu chengine ambacho nimekiona labda nikizungumze ni kifungu cha 150 na 151 vifungu hivi vinazungumzia masuala ya kutelekeza watoto. Sasa hivi imekuwa ni jambo la kawaida wanaume hawataki kutunza watoto tangu wanawake wawe na uwezo kusoma kwetu na kufanya kazi kwetu kumewafanya wanaume waache majukumu yao wanawatelekeza

watoto na akiwa kakuacha ndio kabisa hakushughulikii. Ukiwa na mtoto mwenye ulemavu ndio kosa utafikiri wewe mwanamke ndio uliyekuwa unataka uzae mtoto mwenye ulemavu, anasahau kama mtoto tulizaa wawili bila ya mimi na yeye tusingekuwa na mtoto. Sasa iweje leo mtoto akizaliwa akiwa na ulemavu inakuwa sasa ni kosa la mama unamwachia, na sisi wamama pia tunajisahau mtoto akishakuwa na ulemavu tunahisi kwamba si mtoto, kwa hivyo tunafanya tunavyojaaliwa kukifanya kiumbe kile kidhalilike wakati si kosa lake.

Kwa hivyo mimi nawaasa akina mama na akina baba tusitelekezeane majukumu kila mmoja atimize wajibu wake na mama kama wajibu wako kumlea mtoto hata akiwa mlemavu yule ni mtoto ni kiumbe kina roho anaumwa kama anavyoumbwa mwengine. Kwa hivyo tusiwaache tukawafanya wakaishi vibaya eti tu kwa sababu ni walemavu. Mimi nafikiri ifike wakati tujue kwamba kile nacho ni kiumbe kimeumbwa na ukiwa utafanya hivyo basi ujue kwamba unachukua jukumu.

Kifungu chengine labda ambacho kiwe cha mwisho kwa mimi kukichangia ni sehemu hii ya mwisho ya kifungu cha 20 sehemu ya 21 inayozungumza suala la jinai la kutojali na kupuuza, nimeona nikizungumzie kifungu hichi kwa sababu maalum hoja iliyotolewa leo na Mhe. Jaku Hashim Ayoub mimi kama mfanyakazi niliyefanya kazi katika Wizara ya Afya, mimi kama daktari kwa kweli inasikitisha, imenisikitisha kwa sababu imetudhalilisha wafanyakazi wa Wizara ya Afya.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Dkt. Sira Ubwa Mamboya tunazungumzia mswada sasa, mswada wa Sheria hoja ya Mhe. Jaku imekwisha.

Mhe. Waziri asiyekuwa na Wizara Maalum (Mhe. Dkt. Sira Ubwa Mamboya): *No,* sio suala la Mhe. Jaku limekwisha kuna

kifungu hapa kinachozungumza mtu yoyote ambaye ni daktari mwenye sifa zinazokubalika au vyenginevyo akiondosha kiungo cha binaadamu bila ya ridhaa ya wazazi wake akiwa hai au amekufa, ndicho ninachotaka kukizungumza hapo simchangii Jaku mimi.

Mhe. Naibu Spika: Sawa tuendelee basi lakini muda wako unakwisha umebakia dakika mbili.

Mhe. Waziri asiyekuwa na Wizara Maalum (Mhe. Dkt. Ubwa Sira Mamboya): *Inshaallah,* kwa kifungu hichi na ndicho ninachomalizia kwamba hili lililoandikwa hapa kwamba anapoondosha kiungo cha binaadamu katika mwili wa mtu akiwa mtu huyo hai au amekufa bila ya idhini ya mtu huyo, kwanza najiuliza huyu mtu ameshakufa idhini ataitoa vipi? Aliyehai atatoa lakini keshakufa, lakini kama kuna ndugu zake wametoa idhini hii haya yanatendeka sasa hivi kwa sababu kuna watu ambao wanatolewa viungo kwa kutiwa walio hai sasa hapa kuna sheria hii.

Lakini suala la kwamba mtu hakutia saini kwamba hichi kifanyike hamumuelezi mnamkatia mtoto mkono mnamfanya awe mlemavu mara mbili kwa kweli hapa tumedhalilika na mimi naomba niombe radhi kwa wafanyakazi wenzangu kwa hili lililotokea, watusamehe sana.

Baada ya kusema haya nakushukuru. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Dkt. Sira kwa mchango wako mzuri sana sasa nimpe nafasi Naibu Waziri wa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto, Mhe. Naibu Waziri dakika kumi.

Mhe. Naibu Waziri Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Vijana, Wazee, Wanawake na Watoto: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kuweza kunipatia nafasi hii kuweza kuchangia machache katika Mswada huu uliopo mbele yetu, kwana nichukue nafasi hii kumshukuru Mhe. Waziri wa Katiba, Sheria kwa kuweza kutuletea Mswada huu umekuja wakati muafaka.

Lakini Mhe. Naibu Spika, na mimi kwanza niungane kwa dhati kabisa na Mheshimiwa mama yangu mama Panya kwa mchango wake aliotoa ule kuhusiana na suala zima la tendo linalofanywa kwa baadhi ya wanawake kwa wanawake. Mimi nasema nalaani kwa nguvu zangu zote kwa kila kitu changu nalaani suala hili kwa sababu Mwenyezi Mungu nae ametuamrisha katika Dini na kusema unapoliona tendo baya basi ulikemee, ulikataze na kama huna nguvu za kuweza kulikataza basi ulikemee, basi na mimi nalaani kitendo hichi kwa nguvu zangu zote.

Mhe. Naibu Spika, mimi nimesimama hapa nikiwa kama ni muathirika kwa njia moja au nyengine nasema hivi kwa sababu gani, sijasimama hapa kwa sababu kama Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji wa Vijana, Wanawake na Watoto tunaoshughulikia na masuala haya ya udhalilishaji nimesimama pia kama mama kulizungumzia hili suala la udhalilishaji wa kijinsia linalofanyiwa wanawake na watoto ndio maana nikasema na mimi ni muathirika Mhe. Naibu Spika, Waziri hapa ananiuliza muathirika wa nini, muathirika wa udhalilishaji.

Mhe. Naibu Spika, niendelee kusema kwamba Mswada huu ni mzuri na vifungu vyake nasema vimepangika vizuri na vijajitosheleza vya kutosha, kwa hivyo niwaombe sana waheshimiwa wenzangu wawakilishi tuweze basi kuupitisha mswada huu kwa umoja wetu ili na sisi Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto tuweze kulifanyia kazi

hususan tukiangalia hili suala la udhalilishaji lilivyoikumba nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, wenzangu wamechangia mengi mno na vifungu wamevichambua, lakini mimi sitaki kuchambua kifungu hadi kifungu lakini nataka nikizungumzie hichi kifungu cha 116 juu ya kumdhalilisha mtoto mwenye ulemavu.

Mimi naweza nikawa shahidi Nam. 1 kwa masuala hayo. Nikiwa pale Afisini tunashuhudia mambo mengi ndiyo maana nikasema ni muathirika kwa njia moja au nyengine. Tunaletewa pale watoto ambao tayari wameshafanyiwa hayo matendo. Wewe kama mzazi unaona tumbo linakukata, nguvu zinakuishia, unatamani kama ardhi ipasuke uingie kwa masuala yale. Hususan hawa wenzetu wenye ulemavu kwa sababu wao masikini pengine wanaonekana kama hawana ushahidi wa kutoa pale ukaweza kuridhisha na wakaweza kwa hali halisi hawa wakaweza kutiwa hatiani moja kwa moja. Kwa hivyo nishukuru sana Mhe. Waziri kwa kifungu cha 116 kimejieleza vizuri na vyengine vyote.

Lakini pia tunabadilisha Sheria mbali mbali hapa, lakini kama tunavyoambiwa kwamba bila ya ushahidi hakuna kesi. Naomba nichukue fursa hii kwa dhati kabisa kuwaomba wananchi washirikiane na serikali yao katika suala zima la kutoa ushahidi. Tumezungumza hapa tunasema sheria zetu nzuri, vipengele vizuri lakini kama hakuna ushahidi itakuwa ni kazi bure. Tushirikiane na serikali yetu katika suala zima la kutoa ushahidi na kuhakikisha kwamba haya masuala ya udhalilishaji wa watoto yanaondoka kabisa katika nchi yetu. Kama alivyozungumza Mhe. Waziri Said Soud Said kwamba hili janga sasa hivi limekuwa aibu kwa nchi yetu na sisi wenyewe hasa Wazanzibari. Kuna maneno yayosemwa kwamba ukijulikana Mzanzibari hayafai hata kuzungumzwa, kwa kweli ni kero na ni aibu kubwa sana.

Mhe. Naibu Spika, niwaombe sana Waheshimiwa wenzangu tuunge mkono huu Mswada wetu tuupitishe kwa nia moja sote hapa ili tuweze kutelekeza majukumu yetu katika kuondokana na suala zima hili la udhalilishaji.

Baada ya kuzungumza hayo machache Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana na mimi naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Naibu Waziri, sasa nimpe nafasi Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto, karibu.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika, kwa heshima na taadhima napenda nichukue fursa hii kwanza kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, kuwashukuru sana viongozi, kuwashukuru wote waliohusika katika suala hili.

Mheshimiwa tokea tumeanza kujadili mswada huu na hasa ile siku ambayo tuliyokuwa tumetolewa semina nilianza kupata usingizi kwa kiasi fulani. Kabla sijaendelea naomba nimshukuru sana Mhe. Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dr. Ali Mohamed Shein, kwa jitihada ambazo amekuwa akifanya kuhakikisha kwamba tumefikia katika hatua hii ni pamoja na kuonesha alipofanya ufunguzi wa uzinduzi wa masuala ya kupinga udhalilishaji katika mwezi wa Agosti tarehe 26 akiungana na juhudi za kimataifa. Nimshukuru pia Makamu wa Pili wa Rais, Balozi Seif Ali Idd katika mikutano yote amekuwa akichangia sana suala zima la kuhakikisha kwamba masuala ya udhalilishaji yanatoka.

Mhe. Naibu Spika, napende kumshukuru sana Waziri wa Afisi, Katibu Mkuu Kiongozi pamoja na Makatibu wake wakuu

waliokaa kwa pamoja kuhakikisha kwamba wameyajadili na kuyapitia masuala yote haya hata yametufikia sisi mahali hapa. Lakini niishukuru pia Afisi ya AG na Afisi ya DPP na watendaji kwa kutoa elimu ya awali, vyenginevyo hapa pasingetosha. Walitupa elimu ya awali kabla hatujaingia kwenye Baraza kuhakikisha kwamba tumepitia vipengele vyote ambavyo vimeletwa hapa mezani.

Mhe. Naibu Spika, pia niwashukuru sana Wawakilishi wenzangu ambao wamechangia kwa upana, nimefarijika sana kwa kuongezeka kwa muda katika masuala mbali mbali ambayo yalikuwa yanawadhalilisha wanawake. Kwa lugha hiyo kuna mengi ambayo yamekuwa yakizungumzwa na sheria zimebadilishwa kama hivi tunavyoziona. Naamini wasikilizaji wanaotusikiliza sasa hivi wanaingia amani. Ni leo tu asubuhi kulikuwa kuna hoja ikizungumzwa kwenye redio, walikuwa wanasema ikiwezekana mtu huyo afungwe au afe na kama alivyokuwa amesema Mhe. Said Soud Said hawa labda huyu ahasiwe. Walikuwa na hasira ya mambo mengi lakini naamini wakishayasikia masuala haya tutayopitisha katika vifungu muda mchache ujao sasa hivi watatuunga mkono na kuona kwamba juhudi inaendelea.

Mhe. Naibu Spika, nilikuwa naomba tu niseme kwamba kuna Mheshimiwa mwenzangu mmoja amezungumza kwamba lugha ya kusema kumshambulia mtoto. Nadhani ilikuwa na lugha ya nguvu mno siyo kumshambulia mtoto mara nyingi watoto tunawarudi, hatuwashambulii. Wasije wakachukuliwa kwamba watoto unapomrudi unakuwa unamshambulia. Nia yako kama mzazi ni kuhakikisha kwamba mtoto awe katika mazingira mazuri.

Mhe. Naibu Spika, pia niseme tu mchango mkubwa uliotolewa na Baraza la Wawakilishi Wanawake (UWAWAZA) imesaidia sana, katika kuhakikisha kwamba wametoa michango yao vizuri sana

walipokaa kwenye Kamati na najua hii yote imetokana na juhudi za Mwenyekiti wa UWAWAZA ambaye ni Mhe. Naibu Spika, katika kuhakikisha kwamba Semina nyingi zilizokuwa zinaombwa zikichangiwa na Mataifa, zilihakikisha kwamba sheria zinapitiwa kimoja hadi kimoja na hatimaye kujenga watu kuwa na uwezo wa kujiamini hata tukapata Mwakilishi mwenzetu aliyetoa hoja kuhusiana na suala la udhalilishaji, Mhe. Asha Abdalla Mussa napenda nimpongeze sana na kusema kwamba katika jitihada hizo tumefikia katika hatua hizo tunazokwenda.

Mhe. Naibu Spika, pia nitoe wito kwa wanasheria mambo yanayoletwa mezani yanawekwa humu na wananchi wengi wanakuwa wanahisi kwamba Sheria mpaka zikasomwe Mahakamani asomewe Sheria ndiyo aone kwamba amekosa. Kumbe kosa ni kutofahamu sheria haina maana itakufanya wewe hujakosa. Kwa hivyo suala zima la kutoa elimu kwa wananchi na sisi wenyewe wananchi tuweze kuhakikisha kwamba tunajifunza sheria ili tuweze kuzitambua madamu zimeshakuwa wazi.

Pia niwashukuru sana waratibu wangu katika Wilaya, Masheha, ambao wamekuwa wakisaidia katika suala zima la masuala ya udhalilishaji, katika kuhakikisha sheria na kesi nyingi ambazo zimepita sasa hivi ambazo watu wapo vifungoni na nilipata nafasi ya kuwatembelea wengine wakasema kwamba tunajuta tukitoka hatutorudia tena. Lakini wakawa wanasema mbona mengine tunakuwa tunashirikiana na hao wasichana, tunapatana, lakini wanapofungwa wanafungwa wao peke yao. Suala ni kwamba wao wamekosa wamefanya utoroshi, na mambo mengine imebidi waingie ndani.

Pia mchango mwengine uliotolewa na polisi, uliotolewa na watu wengine ambao bado tunahitaji msaada mkubwa sana kwa polisi kuhakikisha kwamba haya masuala yasipoletwa na DPP anavyosema kwamba kama sheria hakutokuwa na ushahidi wa

kutosha basi masuala haya yote hayatowezekana kwa sababu ni lazima kuwepo na ushahidi. Lakini inapoingia masuala ya ushahidi kunakuwa na masuala ya muhali, tukiondosha muhali tunaweza tukafanikiwa tukafika mahali pazuri.

Mhe. Naibu Spika, lakini niseme pia kwamba sheria ambazo zimetolewa mpaka kufika miaka 30 ya kufungwa ambayo inatutia moyo kwamba labda watu wataogopa na kuacha. Ukiangalia katika kifungu cha 109 kwenye ukurasa wa 308 kinachozungumzia masuala ya kubaka mtu mmoja au kubaka kwa makundi na pia katika kujaribu kubaka, vifungo vyao vimekuwa vyengine vya maisha na vyengine miaka 30.

Pia kuna suala la kumuingilia mtoto kinyume cha maumbile kulikuwa kuna miaka imepunguzwa kidogo lakini Kamati wamependekeza kwamba iongezeke. Ningependa Kamati kama walivyopendekeza kiweze kuongezwa.

Lakini pia niungane Kamati kutokana na hali iliyokuwepo sasa hivi imekuwa kila siku imekuwa ni hadithi za kawaida na kwamba ubakaji unaonekana kama ni zoezi la kusema kwamba fulani kafanya basi na mimi nifanye.

Mhe. Naibu Spika, kuna suala zima la kufuga mtoto ukurasa wa 311 kifungu 119 kinachosema kuwa mtu atakapokuwa anafuga mtoto wa kiume na kumuuza hapa hajaandikwa mtoto wa kike wanaoingiliwa, wameweka katika miaka mitano mpaka 10 ikiwezekana iongezeke zaidi. Kwa sababu hata anayefuga mtoto wa kike kumfanya atumikishwe kama ni Malaya au kwa ajili ya kujiuza kimwili nayo ionekane kwamba ni kosa ambalo ni kubwa.

Kumkamata mtu yeyote sio lazima polisi na hii sheria ukiangalia kwenye ukurasa kusema kuwakamata mtu gani anayehusika katika kuwakamata watu, ukisema katika eneo lile utakuta

kwamba vifungu vya sheria vimeonyesha kwamba watu wengi wanaweza kuhusika kuwakamata watu wanaofanya makosa pasipokuwa na hati. Kwa hivyo hivi viachwe wazi watu wajue wasingoje kwamba mtu ametenda mpaka anakimbia hawezi wakampata anajificha halafu inakuwa namna ya kumkamata mtu aliyehusika hayupo.

Mhe. Naibu Spika, niseme tu kwa ujumla Mheshimiwa mimi nimepata faraja na ninaamini wasikilizaji na wao wamepata faraja kwamba zile kesi ambazo nilikuwa nasema kwamba na pia dhamana, hakuna dhamana sasa. Wewe mwenye mawazo ya kutaka kubaka kesho ole wako hakuna dhamana. Ninamuomba Mheshimiwa saa itakayofika hii karatasi aitie sahihi kabisa ili kuweza kuhakikisha kwamba watu sasa hivi hakuna muhali tena.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo napenda niipongeze Kamati nimpongeze Waziri, Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwenye ofisi yake, niwapongeze viongozi wote waliohusika, Wawakilishi. Lakini pia nawapongeza tuendelee kushikamana na haya. Ikiwa mambo mengine wakiona tumeyasahau tusichelewe kubadilisha Sheria tena. Kwa sababu kama kuna mengine tumeyasahau hapa tunaona kama hatujayazingatia naamini hutotuzuia kuendelea kuleta hoja kwa ajili ya kubadilisha sheria hizo.

Baada ya kusema haya nawashukuru na Mungu awabariki sana. Ahsante.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto, sasa mchangiaji wetu anayefuata ni Mhe. Naibu Waziri wa Wizara ya Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma, Mhe. Naibu Waziri karibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika,nikushukuru nami kunipatia nafasi hii ya kuchangia Mswada huu miongoni mwa Miswada muhimu sana. Mimi nitakwenda moja kwa moja kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya hoja za Wajumbe ambao walichangia Mswada huu. Naanza moja kwa moja kwa Mhe. Omar Seif Abeid.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Omar Seif Abeid aligusia kifungu cha 3, kilichokuwa na neno tafsiri mwanamke. Tafsiri hiyo imewekwa ili kutofautisha baina ya mwanamke na mtoto wa kike na pia kwenda sambamba na Sheria ya Watoto Nam. 6 ya 2011. Kuhusu kifungu cha 8(1) kuhusiana na neno "Uzembe" kifungu hicho kimeanza kwa maneno bila ya kuathiri masharti yaliyotajwa katika sheria hii kuhusiana na vitendo vilivyofanywa au kuachwa kufanywa kwa uzembe.

Mhe. Naibu Spika, makusudio ya kifungu hichi ni kwamba kama ikithibitika kuwa mtu ametenda au ameacha kutenda kwa uzembe hiyo haitokuwa kinga, kwa hivyo masharti ya sheria hii kuhusu jinai yatatumika kwa makosa na adhabu.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Omar Seif pia alizungumzia kifungu cha 12 kuhusiana na ulevi. Kifungu cha 12 kinachohusiana na ulevi, kwa ujumla kulewa hakutochukuliwa kuwa ni utetezi katika kosa lolote la jinai. Ulevi unaweza kuwa ni utetezi endapo tu:

a) Hali ya kulewa huko ilisababishwa bila ya hiyari yake kwa kitendo cha ubaya au uzembe wa mtu mwengine au

b) Kwa sababu ya kulewa mtu aliyeshtakiwa ana matatizo ya akili ya muda mfupi au vyenginevyo wakati wa kutenda huko au wakati wa kuacha kutenda.

Kuhusu matumizi ya kujilinda katika Kifungu cha 17 ambapo pia imechangiwa na Mhe. Mussa Foum Mussa na Mhe. Hamza Hassan Juma. Mhe. Naibu Spika, mtu ataruhusiwa kutumia nguvu katika kujilinda lakini nguvu anazoruhusiwa kisheria kuzitumia zilingane na kiwango cha nguvu anazotumia mshambuliaji. Kwa hivyo suala hilo hupimwa zaidi kwenye ushahidi Mahakamani.

Kuhusu neno "haijalishi", Mheshimiwa amependekeza lisomeke "bila ya kujali". Matumizi ya neno "haijalishi" ni sahihi kwani kisheria maneno "bila ya kujali" yana maana tofauti kabisa na neno haijalishi.

Aidha neno "alimradi" lilitumika katika kifungu cha 24(1), neno hili ni neno la Kiswahili ambalo linakubaliana, linatumika na linapatikana katika Kamusi ya Kiswahili fasaha kabisa lilotolewa na Baraza la Kiswahili la Zanzibar BAKIZA mwaka 2010 ukurasa wa 10 ambalo linaweza kutamkwa almuradi alimradi au ilimradi.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu adhabu ya kubaka kwa vijana katika kifungu cha 109 ambacho pia Mheshimiwa alikigusia Mhe. Omar Seif Abeid adhabu hiyo imefanyiwa utafiti kwa sababu yeye alitakakujua anaona kwamba adhabu hii ni kubwa. Kama tujuavyo kwamba adhabu ya kubaka adhabu yake ni kifungo cha maisha isipokuwa katika mazingira yaliyoelezwa katika kifungu kidogo cha 109(2) na katika hali nyengine yoyote atapewa kifungo kisichopungua miaka 30 na faini. Halikadhalika zaidi ya adhabu hizo ataamuriwa alipe fidia kwa kiwango kitakachoamuliwa na Mahakama kwa madhara ya kimwili ambayo yule aliyepata ile kadhia alisababishiwa.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu adhabu ya kubaka kama nilivyosema ni adhabu ambayo imefanyiwa utafiti wa kutosha na tunaona

ibakie kama ilivyopendekezwa kutokana na mazingira yalivyo hivi sasa.

Kuhusu kinga kwa Maafisa wa Mahakama katika kifungu cha 114. Hili ni jambo la kawaida kwa mihimili yetu yote. Kwa mfano Rais amewekewa kinga ya Kikatiba katika kutekeleza majukumu yake. Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi nao wamepewa kinga ya kikatiba na kisheria katika kutekelezaji wa majukumu yao. Maafisa wa Mahakama na wao kinga zao zimetajwa katika kifungu cha 14 cha Mswada wa Sheria hii.

Mhe. Naibu Spika, sasa niende katika hoja ya Mhe. Dk. Mwinyihaji Makame Mwadini, kwanza kabisa tumshukuru Mheshimiwa kwa mchango wake na tunakubaliana na yeye kwamba Mahakimu na Majaji wafanye kazi kwa uweledi na maadili. Kuhusu chombo kinachowasimamia watendaji wa Mahakama kwa maana ya Majaji na Mahakimu ni kama ifuatavyo:

(a) Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa upande wa wasimamizi wa Majaji lakini kwa upande wa wasimamizi wa Mahakimu, Kamisheni ya Utumishi wa Umma, Tume ya Utumishi wa Mahakama na Mrajis wa Mahakama Kuu.

Kuhusu kifungu cha 25(k) kinachohusu kufuta au kuisitisha leseni ya udereva chini ya Usalama Barabarani. Adhabu hiyo siyo adhabu pekee kwani Sheria ya Usalama Barabara zimeainishwa pia adhabu nyengine kali zaidi. Kuhusu utekelezaji wa adhabu ya kifo kuthibitishwa na Mhe. Rais, suala hilo limefafanuliwa katika Mswada wa Sheria wa Mwenendo wa Jinai ambao nao utajadiliwa hivi karibuni.

Sasa niende katika hoja ya Mhe. Mussa Foum Mussa, yeye alichangia katika masuala ya kuwepo au kutokuwepo kwa adhabu ya kifo. Kuhusu kuwepo au kutokuwepo kwa adhabu ya kifo kifungu cha 25(a), mjadala huu bado unaendelea lakini kwa sasa ni vyema ikabakia kama ilivyopendekezwa hadi mjadala huo utakapofikia mwisho ya uamuzi kupatikana.

Mhe. Dk. Makame Ussi pia alichangia kuhusu utekelezaji wa adhabu ya kifo kwa kosa uhaini katika kifungu cha 27 cha Mswada huu ambapo hoja yake inafanana na mjadala wa kuwepo au kutokuwepo kwa adhabu hiyo ya kifo.

Kuhusu adhabu ya matendo ya usagaji katika kifungu cha 136 ambayo pia imechangiwa na Mhe. Hidaya Ali Makame, Mhe. Panya Ali Abdalla na Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma, tunaona kwamba adhabu hiyo iliyopendekezwa katika Mswada huu wa kifungo kisichopungua miaka mitano au kisichozidi miaka kumi inatosha na inakidhi mahitaji yaliyopo.

Kuhusu utolewaji wa adhabu hiyo katika kifungu cha 136 kwa mtoto wa kike ambaye pia imechangiwa na Mhe. Hidaya Ali Makame utolewaji wa adhabu katika kosa hilo utazingatia pia masharti ya sheria yaliyopo katika Sheria ya Watoto Nam. 6 ya Mwaka 2011.

Mhe. Naibu Spika, ni vyema sasa nikenda kuangalia hoja za Mhe. Hidaya Ali Makame, yeye pamoja na mambo mengine alizungumzia kifungu cha 144 juu ya idhini ya maandishi ya Mkurugenzi wa Mashtaka. Kuhusu kifungu 144 juu ya idhini ya maandishi ya Mkurugenzi wa Mashataka, Mkurugenzi wa Mashtaka kwa mujibu wa kifungu cha 56(a) cha Katiba ya Zanzibar ndiyo mwenye mamlaka ya jumla katika ufungaji na uendeshaji wa mashtaka ya jinai.

Kwa hiyo kifungu cha 144 kinakwenda sambamba na kifungu cha Katiba, endapo Mkurugenzi wa Mashtaka atakuwa hayupo basi yeyote anayekaimu nafasi hiyo atatekeleza jukumu hilo kwa mujibu wa matakwa ya Katiba na Sheria.

Pia Mkurugenzi wa Mashtaka amepewa Mamlaka ya Kukasimu majukumu yake. Suala hili la idhini ya Mkurugenzi wa Mashtaka pia limechangiwa na Mhe. Miraji Khamis Mussa ambalo majibu yake ni hayo. Kuhusu kifungu cha 186 kinachohusu matangazo kwa mali iyoibiwa, mantiki ya kifungu hiki ni kuzuwia vitendo vya wizi kwa kisingizio cha kuokota.

Mhe. Dkt. Makame Ussi na yeye alichangia mambo yafuatayo, lakini niseme tu kwamba tumepokea mchango wa Mhe. Dkt. Makame Ussi kwamba ni lazima tujiandae kuwa na vyombo au vifaa vya kufanyia ushahidi wa kitaalamu yaani unajulikana kwa jina la kitaalamu *Forensic Evidence*.

Kuhusu umbali wa bahari uliotajwa katika kifungu cha 4 eneo la Zanzibar linalohusu matumizi ya sheria hii mipaka yake ni ile ile iliyoainishwa katika Katiba ya Zanzibar, kuhusu mtu aliyefanya kosa akatoroka kwenda nje ya nchi Mhe. Naibu Spika, mtu huyu atakaporudi atakamatwa na kushitakiwa. Kwa ujumla hakuna ukomo wa muda katika mashitaka ya jinai isipokuwa kwa kosa la uhaini au makosa madogo madogo ambayo adhabu zake ni ndogo kama yaliyotajwa katika mswada wa sheria ya mwenendo wa jinai.

Kuhusu adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka miwili kwa udanganyifu utakaofanywa na watumishi wa umma uliotajwa katika kifungu cha 94 tunaomba kwamba adhabu hiyo ibakie kama ilivyo.

Mhe. Naibu Spika Mhe. Miraji Khamis Mussa na yeye pia alipata kuchangia kuhusu bahari kuu katika kifungu cha 4.

Mhe. Naibu Spika kwa mujibu wa sheria ya kimataifa bahari kuu haina mwenyewe kosa linalotendwa katika bahari kuu hutegemea bendera inayo peperushwa na chombo husika na pia usajili wa chombo hicho, kwani mantiki hiyo kifungu cha nne hakina mgongano na Katiba ya Tanzania kuhusiana na bahari kuu.

Mhe. Naibu Spika pia Mhe. Miraji aligusia tendo lote la siri kuhusiana na kosa la uhaini, Mhe. Naibu Spika kuhusu tendo lolote la siri kuhusiana na kosa la uhaini katika kifungu cha 27 kwa ujumla hili kosa la jinai likamilike lazima pawepo na nia ovu yaani *mens rea* na kutekeleza tendo la dhahiri yaani *actus reus* kuwepo na nia ovu ya kutenda kosa hakuwezi kuunda kosa la jinai mpaka hii nia ovu ionenakanwe au ijitokeze katika matendo na matendo hayo ndiyo yanajulikana kuwa ni matendo ya dhahiri.

Mhe. Naibu Spika,kifungu cha 27 nacho pia kiligusiwa na Mhe. Miraji kinawagusa watu wote yaani wageni na wenyeji alitaka kujua kwamba kinawagusa wenyeji tu lakini kinagusa watu wote. Kuhusu kifungu cha 30(b) nakubaliana kuwa tuongeze maneno wakuu wa Idara Maalum katika orodha iliyopo. Kuhusu kuongeza maneno vyombo vya habari kufungu cha 31(a) tunakubaliana na ushauri wa Mhe. Miraji na hivyo yanaongezwa maneno au kuvamia vyombo vya habari baada ya maneno kutekeleza mamlaka na majukumu yao.

Kuhusu kifungu cha 43 kifungu kidogo (1) ambacho pia kimechangiwa kwa maandishi na Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma tunaona adhabu iliyopo inatosha ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi sita na kisichozidi miaka miwili kwa kuchapisha taarifa za uongo, kifungu 46 kifungu kidogo 2(a) kuhusiana kutoa *notice* kwa Rais au Katibu Mkuu Kiongozi huu

Mhe. Naibu Spika, ndio utaratibu uliopo na unatumika sasa ambao hauna matatizo yoyote ya kiutendaji.

Kuhusiana kifungu cha 47 kinachohusina na maswali ya uharamia kifungu hiki kimezingatia pia vyombo vya angani.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mussa Ali Mussa naye alikuwa na hoja zifuatazo, aligusia kufungu cha 114 kinachozungumzia shambulio la aibu. Mhe. Naibu Spika kifungu 114 kinachozungumzia shambulio la aibu ambapo Mhe. Mussa maelezo yake yameonekana kuelemea zaidi kwenye shambulio la kawaida, shambuli la kuumiza mwili na shambulio la hatari ambayo yapo katika vifungu cha 229, 230 na 231. Tunamuomba Mhe. Mussa aendelee kuvisoma vifungu hivyo kwa ufafanuzi zaidi. Tunampongeza Mhe. Mussa kwa upande mwengine kwa ufahamu wake na maelezo yake mazuri katika masuala ya uvunjaji wa nyumba kijinai kuhusiana na matendo na nia ovu chini ya kifungu cha 290 cha mswada huu.

Mhe. Naibu Spika kuhusu suala la kuhughushi *passport* kuwa ni kosa la muungano ambalo pia hili liligusiwa na Mhe. Mussa sehemu ya 32 ya mswada huu inahusisha kosa la kughushi kwa ujumla wake bila kujali kitu gani kinaghushiwa kwa hivyo aina yoyote yakughushi ni kosa kwa mujibu wa mswada wa sheria hii.

Kuhusu kifungu cha 69(1) kukisia kwa kutumia nguvu adhabu iliyopo ya kifungo kisichozidi miaka miwili tunaona inatosha kwa vile kosa husika na kutishia tu kwa kutumia nguvu. Pia hoja hii ilichangiwa na Mhe. Panya. Aidha tunamshukuru Mhe. Mussa Ali Mussa kwa mchango wake makini kuhusiana na watoto kuhitaji kupewa malezi mazuri na matumaini yetu jamii imemsikia. Mhe. Hamza Hassan Juma naye pia alipata kuchangia Mhe. Hamza alitaka kujua sheria inayosimamia mawakili, sheria

inayosimamia mawakili ni Sheria ya Mawakili na Mavakili sura ya 28 ya Sheria ya Zanzibar.

Kuhusiana na kifungu cha 13 kuhusu umri mdogo Mhe. Hamza alitaka tuainishe na Sheria ya Watoto tunapenda kumthibitishia Mhe. Hamza kuwa jambo hilo limefanyika na limezingatia ipasavyo katika mswada huu, tunampongeza Mhe. Hamza kwa mchango wake kuhusu kifungu cha 27 juu ya uhaini na tumeupokea mchango huo.

Kuhusiana na kosa la kujitangaza kuwa Rais Mhe. Naibu Spika, kuhusiana na kujitangaza kuwa Rais kosa hilo limeelezewa katika Sheria ya Uchaguzi na adhabu yake pia inapatikana katika sheria hiyo pia.

Kuhusu uchochezi katika mitandaa ya kijamii kosa hili limeelezewa katika Sheria ya Makosa ya Mitandao ya Tanzania ambayo pia inatumika Zanzibar pia hoja hii ilichangiwa kwa maandishi na Mhe. Hamida Abdalla Issa.

Adhabu katika kifungu cha 55 kuhusu mtu anayeshiriki katika mkusanyiko usio halali ambapo imetoa kwa kipindi kisichozidi mwaka mmoja tunaona kwamba adhabu hiyo iliyopendekezwa katika mswada huu inatosha.

Kifungu cha 61 kinachohusi kufanya fujo na kubomoa majengo tunaona kwamba adhabu iliyopendekezwa katika mswada huu inatosha ya adhabu ya kifungo cha maisha. Aidha kifungu cha 64(1) kuhusu kutembea na silaha hadharani tunaona kwamba adhabu iliyopendekezwa katika mswaada huu inatosha ya kifungo cha miaka miwili na silaha kuchukuliwa na serikali kwani kuna kifungu kidogo cha 2 kinachohusu kumiliki silaha bila halali tayari kinatoa adhabu kubwa zaidi kuliko hiyo, pia Mhe. Panya alichangia kuhusu kifungu hiki.

Mhe.Panya Ali Abdalla na yeye kwanza tunampongeza na kumshukuru kwa mchango wake mzuri na wenye nasaha nyingi na mawaidha kuhusu mswada kwa ujumla kuhusu kifungu 140 kuhusu muungano wa watu wa jinsia moja tunaona kwamba adhabu iliyipoendekezwa katika mswada huu inatosheleza.

Kuhusu uchukuaji wa mali za jumuiya isiyo halali mali ambazo ziko nje ya zanzibar kifungu cha 53 kinaelezea utaratibu wa mali zilizopo ndani ya Znzibar, kwa mali zilizopo nje ya Zanzibar ni lazima upatikane usaidizi wa kisheria wa mahkama wa nchi ambazo mali hizi zipo kwa makubaliano rasmi.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu tangazo kwa jina la Rais katika kifungu cha 57 huu ni utaratibu wa kisheria unaomtaka afisa anayetoa tangazo aseme kuwa anatoa tangazo hilo kwa nia ya Rais linalowataka watu waliokusanyika watawanyike kwa amani.

Pia Mhe. Panya ametaka kujua kama ipo sheria ya umiliki wa silaha katika zanzibar hakuna sheria inayoruhusu umilikaji binafsi wa silaha ispokuwa wanaoruhusiwa kuwa na silaha ni vikosi vya ulinzi na usalama na Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika mjumbe mwengine aliyepata nafasi ya kuchangia ni Mhe. Shamata tunamshukuru Mhe. Shamata kwa mchango wake na nasaha zake kuhusiana na mswada huu na kwamba anajaribu kututanabahisha kwamba masharti yaliyopendekezwa ndani ya mswada tuyapitishe kama yalivyo ili kwanza tuone utekelezaji wake na kama marekebisho yaje baadae kutokana na kasoro zitakazojitokeza katika utekelezaji wa sheria.

Mhe. Saada naye pia alipata nafasi kuhusu kifungo cha nje kimeorodheshwa kwenye kifungu cha 25(j) na kinasomeka kama ifuatavyo:

"Kuachia kwa masharti chini ya sheria inayohusu waangalizi wa wahalifu"

Aidha adhabu ya kifungo cha nje pia imetajwa katika mswada wa mwenendo wa jinai katika vifungu 297, 328 na 329. Kosa la kuendesha gari kwa mwendo wa kasi na makosa mengine yanayohusiana na hayo yapo katika sheria ya usafiri barabarani makosa yaliopo katika kifungu cha 173 hadi kifungu cha 176 adhabu zake zinapatikana katika kifungu cha 26 cha mswada huu.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Hamida naye alipata kuchangia kwanza tunamshukuru Mhe. Hamida kwa kuhimiza utekelezaji wa sheria hii hasa katika kifungu cha 68 kinachohusu kuchochea mapigano ya watu wawili. Kuhusu dhamana kwa makosa ya kubaka hii imeelezwa kwa vizuri zaidi katika mswada wa sheria ya mwenedo wa jinai.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mohamed Said Mohamed (Dimwa) naye alipata fursa ya kuchangia. Tunamshukuru Mhe. Mohamed Said Mohamed (Dimwa) kwa pongezi alizozitoa kwetu kuhusu vifungu vinavyotaja mawakili, vifungu hivyo vipo katika Mswada wa Sheria ya Mwenendo wa Jinai. Pia kama tulivyoeleza awali kuwa ipo sheria inayosimamia mawakili na mavakili yaani sura ya 28 ya Sheria ya Zanzibar.

Kuhusu chombo kinachoratibu mawakili ni Mhe. Jaji Mkuu pamoja kwa mamlaka aliyopewa ndani ya sheria hiyo sura ya 28. Hata hivyo, serikali inafanya mapitio ya sheria hiyo ili kuainisha maeneo yanayohitaji marekebisho na kufanyiwa marekebisha au kutungwa upya.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Salha naye alikigusia kifungu cha 91 kuhusu kifungu cha 91 kinachohusu adhabu ya mtu anayemuesha

mtu mwengine kutoroka kizuizini Mhe. Salha alipendekeza mtoroshaji apewe adhabu ya kifungo cha yule mtu aliyetoroka katika utaratibu wa jinai mtu huwepa adhabu kwa kosa lake mwenye na siyo kwa kosa la mtu mwengine kwa hiyo, mtu anayetorosha atapewa adhabu kulingana na kosa hilo la kutorosha kwa mujibu wa kifungu hiki ambayo tunaona inatosha.

Kuhusu adhabu katika 119 tayari lishaongezwa na marekebisho ya kamati kutoka miaka mitano hadi miaka kumi, kuhusu kifungu namba 221 kutowataja wakala wakata vilimi na utata Mhe. Naibu Spika, suala hili lilijadiliwa katika kamati na ilionekana kwamba bado hakuna tatizo kubwa linalohitaji kuwekewa masharti ya kisheria hivyo iliamuliwa kubakia na kosa la kuondosha *ma-tonsils* peke yake kwa vile limeonekana athari yake ni kubwa.

Mhe. Naibu Spika kwa hayo machache na mimi naomba kuunga mkono mswada huu wa Sheria ya Adhabu asilimia mia kwa mia. Ahsante.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Naibu Waziri wa Wizara ya Katiba na Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora Waheshimiwa Wajumbe sasa tunampa nafasi Mhe. Mwanasheria Mkuu na yeye aweze kuchangia katika mswada huu, Mwanasheria Mkuu karibu.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Naibu Spika nakushukuru kwa kunipa nafasi angalau na mimi niseme machache sana kwenye hoja hii iliyopo mbele yetu ya Mswada wa Sheria ya Adhabu. Mengi yamesemwa tokea tumeanza kwenye kamati, tokea twende kwenye semina lakini na michango mingi ambayo waheshimiwa wajumbe wamechangia tokea hoja hii ilipowasilishwa ndani ya Baraza hili.

Lakini pili nimshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa kazi kubwa ambayo ameifanya ya kutoa utatanuzi kwenye baadhi ya hoja ambazo waheshimiwa wajumbe walikuwa nazo. Naamini sana ufafanuzi wa Mhe. Naibu Waziri na ule ambao atakuja kuotoa waziri mwenye husika utasaidia sana wakati tukikaa kama Kamati ya Kutunga Sheria kupitisha mswada huu kifungu kwa kifungu, lakini kupitisha tena bila yale mabuti ambayo tumeyazoweya yawepo tu mabuti ya kutaka ufafanuzi lakini siyo yale ya kutumia muda mrefu kujadiliana.

Lakini Mhe. Naibu Spika, na mimi nichukuwe fursa hii kuwapongeza sana Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kutimizia ahadi ambayo tuliitoa wakati wa kupitisha bajeti ya 2017/2018 Mhe. Waziri aliahidi hapa kwamba atahakikisha miswada hii miwili anaileta ndani ya kipindi cha bajeti cha mwaka huu wa fedha kwa hiyo niwapaongeze sana Mhe. Waziri na Watendaji wake wote ambao wamesaidiana nao katika kuhakikisha kama ametimiza ile ahadi ya Mhe. Waziri ambayo ameitoa.

Mhe. Naibu Spika sura ya tatu ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kuanzia kifungu cha 11 mpaka kifungu cha 21 kinawenga kinga za lazima wajibu na uhuru wa mtu binafsi ili usome vizuri sheria hii inabidi pia usome na sura ya tatu ya Katiba ya Zanzibar sura ile ndiyo inayoweka msingi mzima wa haki za binadamu ndani ya katiba, haki zote za binadamu ambazo zinatakiwa mtu awe nazo basi zimeelezwa kwenye sura ya tatu ya katiba ya Zanzibar na kifungu cha 12 Mhe. Naibu Spika, kifungu cha 12(6)(b) kinaeleza kuwa mtu aliyeshitakiwa kwa kosa la jinai hatatendewa kuwa mtu huyo mwenye kosa hilo mpaka itakapothibitika kuwa anayo hatia ya kutenda kosa hilo kwa lugha ya kawaida tunasema kila mtu yuko huru mpaka pale atakapotiwa hatiani na mahkama sasa uhuru huo ni uhuru wa kikatiba ambao umeainishwa kwenye kifungu cha 12 kufungu cha 6 (b) na ili mtu

sasa atiwe hatiani maana sasa tunahitaji sheria hizi za makosa ya jinai lakini pia tunahitaji Sheria ya Adhabu ambayo ndio leo tutaipitisha lakini pia Sheria ya Ushahidi namba 9 ya mwaka 2016 ambayo tayari tumeshaipitisha. Sasa sheria tatu hizi Mhe. Naibu Spika, ndio sheria ambazo zinasimamia masuala ya jinai katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, ukisoma pia kifungu cha 14(1)(2) kifungu cha 14(1) na Kifungu cha 14(2) cha Katiba yetu ya Zanzibar kinatoa kinga kwa kila mtu kuwa huru na kuishi huru, kinatoa kinga kila mtu kuwa huru na kuishi kama mtu huru. Lakini kifungu kidogo cha 2 cha kifungu cha 14 kimeweka masharti ya namna gani uhuru huu ambao mtu amepewa kikatiba unaweza ukaondosha.

1. Katika hali na kwa kufuata utaratibu uliowekwa na sheria lazima kuwe na sheria ambayo itaweka utaratibu wa kuondoa uhuru wa mtu.

2. Katika kutekeleza hukumu amri au adhabu iliyotolewa na mahkama hayo ndio maeneo mawili ambayo uhuru wa mtu unaondoka moja ni kama sheria itaeleza hivyo na sheria zenyewe ni hizi kama mtu atatenda kosa na jinai basi uhuru wake utaondoshwa au kama mahkama itatoa hukumu ya yeye kuwekwa kizuizini au kupelekwa Chuo cha Mafunzo basi pia na yeye uhuru wake utaondoshwa.

Sasa kama nilivyosema mwanzo Mhe. Naibu Spika, inahitaji sana sana tusome vizuri sura yetu ya tatu ambayo ndio inaweka masharti ya lazima za kinga na uhuru wa binadamu wa wananchi wa Zanzibar.

Lakini jengine Mhe. Naibu Spika, ambalo nataka kulizungumza ni yale ambayo yamezungumzwa na Waheshimiwa Wajumbe na hasa kwenye adhabu. Waheshimiwa Wajumbe wengi wamesema

adhabu hizi ziko sawa, wengine wamesema hazitoshi tuongeze nyengine mimi niwaombe sana waheshimiwa wenzangu wawakilishi, hizi adhabu hatuwatungii watu waliokuwa nje huko, hizi adhabu tunajitungua sisi wenyewe kwa hiyo tuwe makini sana katika kushughulikia hizi adhabu.

Lakini hizi adhabu Mhe. Naibu Spika zimeletwa hapa baada ya utafiti mkubwa ambao umefanywa na watendaji na kujirisha kama adhabu hizi zimependekezwa ndani ya mswada huu basi zitatosha kukidhi haja ya hali ilivyo sasa hivi, lakini ukisoma pia mswada huu kuna adhabu ambazo zimewekwa za juu kabisa lakini kuna adhabu za chini ambazo pia mahkama inatakiwa itowe kwa hiyo mahkama imepewa uwezo tofauti na ilivyokuwa zamani. Kama inasema miaka miaka saba lakini sasa hivi sheria inasema mahkama itatoa adhabu isiyopungua miaka fulani na isiyozidi miaka fulani. Kwa hiyo niwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe kwenye adhabu mimi naomba tukubaliane kama haya ambayo yameelezwa na ufafanuzi ambao ameutoa Naibu Waziri basi pia tukubaliane naye.

Lakini hoja nyengine ni hii ambayo ameitowa Mhe. Hassan kuhusiana na makosa ambayo yameelezwa kwenye sura ya sita makosa ya uhaini, lakini na uhaini wenyewe ambao umeelezwa kwenye sura hii ya sita na ametaja kesi ile ya *Machano and eighteen others* ni kweli lakini kama anavyojua Mhe. Hassan kama tarehe 7/10/2000 baada tu ya Mhe. Amani kuwapishwa na kuwa Rais Serikali ilipeleka hati ya kufuta mashtaka kwa kisheria inaitwa serikali ili-*internolle* maana yake iliwafutia mashtaka wale watu. Kwa hiyo, mashataka haya walifutiwa kabla ya Mahakama ya Rufaa haikutoa uamuzi wake. Wasomi wengi wameijadili kesi hii. Kuna wengine wanaosema Mahakama ya Rufaa haikutakiwa kuizungumza ile kesi kilichotakiwa ni ku-*withdraw* kwa sababu kosa lile lilikuwa tayari limeshaondoshwa na serikali. Sasa mengi haya hoja zake za kisheria ni nyingi na

Mhe. Hamad Rashid Mohamed yupo pale anatikisa kichwa anajua hoja zake juu ya jambo hili ni kubwa.

Mhe. Naibu Spika, lakini wazo lake ambalo amelitoa ni wazo ambalo linatekelezeka kikatiba. Mhe. Naibu Spika, ukisoma Katiba ya Zanzibar, kifungu cha 99 kinaeleza na kinatoa uwezo kwa Mahakama ya Rufaa kusikiliza kesi za jinai ambazo zinaanza kwenye Mahakama Kuu. Lakini kifungu hicho hicho cha Katiba kikaeleza kesi ambazo hazitokwenda Mahakama ya Rufaa. Moja, ni tafsiri ya Katiba, tafsiri ya Katiba ya Zanzibar haipelekwi kukatiwa rufaa kwenye Mahakama ya Rufaa. Utaratibu wake unasikilizwa na Jaji mmoja lakini baadae unasikilizwa rufaa yake na Majaji watatu, na lazima tutoe haki ya mtu kukata rufaa. Kwa sababu haki hii imeelezwa kwenye kifungu cha 12 cha Katiba. Lakini Katiba ikasema na kesi ambazo zimeanzishwa kwenye Mahakama ya Kadhi zinazozungumzia masuala ya Kiislamu nazo pia haziendi kwenye Mahakama ya Rufaa. Hayo ni maeneo mawili ambayo yametajwa moja kwa moja na Katiba.

Mhe. Naibu Spika, lakini kifungu cha 99(c) cha Katiba yetu ya Zanzibar ya 1984 kikatoa fursa ya makosa mengine ambayo ama yataelezwa na Katiba moja kwa moja, ama yataelezwa na sheria ambayo itatungwa na Baraza la Wawakilishi. Sasa wengi ambao wamechangia humu wamesema kwa makosa haya basi tutumie uwezo wa kikatiba wa kifungu cha 99(c), na makosa haya ambayo yameelezwa kwenye sura ya sita, basi yaanze kusikilizwa na Jaji wa Mahakama Kuu lakini baadae rufaa yake isikilizwe na Majaji watatu wa hapa hapa Zanzibar.

Mimi nadhani hoja hiyo ni ya msingi na hoja hiyo kwa makofi haya nadhani tunaikubali na haina shaka kwa sababu ni hoja ya kikatiba na Katiba imetoa fursa ya kuongeza makosa mengine ambayo kesi zake hazitosikilizwa na Mahakama ya Rufaa. Kwa hiyo, najua Mhe. Waziri ana mengi ambayo atakuja kuyajadili na

kuyatolea ufafanuzi kwa kina na sitaki nimuondolee hamu yake, niseme tu haya machache lakini niungane na wengi ambao wametoa mchango kwa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Mhe. Naibu Spika, nakushukuru. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mwanasheria Mkuu, Waheshimiwa Wajumbe, kwa kuwa muda uliobakia hautamtosha Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuja kufanya majumuisho pamoja na kujibu hoja, lakini vile vile kwa kuwa kuna wachangiaji wengine wapya walijitokeza na wanahitaji majibu kutoka kwa waziri. Kwa hiyo, nafikiri tumpe muda wa kwenda kufanya majumuisho na baadae tukirudi saa 11:00 Mhe. Waziri ataendelea na kutoa majumuisho na baadae tutapitisha vifungu.

Waheshimiwa Wajumbe, kabla ya kuakhirisha naomba nitoe tangazo kutoka kwa Mwenyekiti wa *CPA*, tawi la Zanzibar anawatangazia Wajumbe wa *CWP* pamoja na *CPA* kuwa kutafanyika kikao chumba Nam.2 baada ya kuahirisha Baraza, hivyo wale wahusika wanaombwa wafike chumba Nam.2. Baada ya kusema hayo Waheshimiwa naomba sasa nisitishe kikacho chetu hadi 11:00 jioni.

(Saa 6:47 mchana Baraza liliahirishwa mpaka saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, awali ya yote naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu *(Subhanahu Wataala)* kwa kutujaalia kufika hapa wakati huu salama na amani kabisa. Aidha, naomba nichukue nafasi hii Mhe.

Naibu Spika, kukushukuru wewe mwenyewe binafsi pamoja na wajumbe wote kwa jinsi walivyochangia na kuujadili mswada wetu huu wa sheria ya adhabu ambayo inafuta ile ya awali.

Mhe. Naibu Spika, nachukua nafasi hii vile vile kuishukuru sana na kuipongeza Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi. Mheshimiwa kamati hii imefanya kazi usiku na mchana, maana yake nimeshuhudia safari hii kamati imekutana siku nne mfululizo jambo ambalo si la kawaida. Lakini nishukuru sana kazi nzuri iliyofanywa na Ofisi ya Baraza la Wawakilishi chini ya Katibu Mkuu kwa jinsi walivyoshirikiana na sisi katika suala hili.

Aidha, nilikuwa na mawazo mengi wakati ule tunafanya semina nikasema semina hii tukishamaliza siku mbili tatu hizi basi mambo yetu kule bondeni itakuwa rahisi, matokeo yake kumbe tumechomoa masuala mengi zaidi na maelezo mengi, lakini yote haya kwa sababu wananchi na wajumbe hapa wana hamu ya jambo hili lifanyike na litendeke, kwa sababu wananchi wetu wameshapata shida sana miaka mingi. Nawashukuru sana wamesoma, wameelewa, wamefahamu, nawapongeza sana.

Vile vile nichukue nafasi hii kushukuru na kutoa shukrani maalum kwa Naibu Waziri wa Wizara ya Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora; nimshukuru sana Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar. Huyu Mwanasheria wetu amebobea yeye na nashukuru sana anaisaidia sana serikali yetu kama anavyosaidia wizara yetu, namuomba aendelee kutusaidia na leo hapa kafanya kazi ya kunifanyia kazi yangu iwe nyepesi sana. Kwa sababu yeye ni mtaalam wa masuala haya ya sheria na asubuhi nilisema hapa kwamba mimi si mwanasheria, mimi ni mwalimu, lakini husaidia saidia tu kutoa mawazo na taaluma. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo sasa naomba uniruhusu kwanza niwataje waliochangia wote kwa kusema na wale waliochangia kwa maandishi. Mswada huu umepata baraka za kuchangiwa na watu 37, waliochangia moja kwa moja ni 28 na tisa wamechangia kwa maandishi.

Mhe. Naibu Spika, wajumbe waliochangia kwa mdomo ni kama hawa wafuatao:

1.Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis Makamu Mwenyekiti wa Kamati

2. Mhe. Ali Suleiman Ali
3. Mhe. Zulfa Mmaka Omar
4. Mhe. Shehe Hamad Mattar
5. Mhe. Asha Abdalla Mussa
6. Mhe. Rashid Makame Shamsi
7. Mhe. Said Omar Said
8. Mhe. Suleiman Sarahan Said
9. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma
10. Mhe. Tatu Makame Ussi
11. Mhe. Omar Seif Abeid
12. Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini
13. Mhe. Mussa Foum Mussa
14. Mhe. Hidaya Ali Makame
15. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi
16. Mhe. Miraji Khamis Mussa
17. Mhe. Mussa Ali Mussa
18. Mhe. Hamza Hassan Juma

Mhe. Hamza Hassan Juma kachangia kwa *style* yake safari hii, kwanza kachangia kwa kusema lakini pia kachangia na kwa

maandishi, lakini huko kwa maandishi kaleta karatasi 12 za kuchangia tu. Sasa bahati mbaya hayupo lakini akija aambiwe tu kwamba aliyotuchangia yote tumeyapokea na tutayafanyia kazi. Aidha, waliochangia wengine ni:-

19. Mhe. Panya Ali Abdalla
20. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
21. Mhe. Hassan Khamis Hafidh
22. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf
23. Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum)
24. Mhe. Sira Ubwa Mamboya (Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum)
25. Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto
26. Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto
27. Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora
28. Mhe. Mwanasheria Mkuu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, tukisema Mwanasheria Mkuu lazima tuongeze na neno "mahiri". *(Makofi)*

Waliochangia kwa maandishi ni:

1. Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ
2. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa
3. Mhe. Hamida Abdalla Issa
4. Mhe. Mohamed Said Mohamed
5. Mhe. Salha Mohammed Mwinjuma
6. Mhe. Mgeni Hassan Juma (Naibu Spika)
7. Mhe. Zaina Abdalla Salum

8. Mhe. Simai Mohamed Said na
9. Mhe. Nassor Salim Ali

Mheshimiwa nawashukuru sana wote hao waliochangia. Nimefurahi sana kwamba Naibu Spika umechangia vizuri sana mchango wako na maelezo yako tunayafanyia kazi tumeyapokea yote. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nikianza na Makamu Mwenyekiti kwa niaba ya Mwenyekiti kwa mara ya mwanzo tokea nimekuwa waziri katika serikali hii, mara nyingi sana huwa tunapokea maoni ya kamati, tunapokea baadhi na mengine tunasema haya tunayaangalia vizuri au tunayafanyia kazi. Lakini kwa mwaka huu au kwa safari hii tunakubaliana na marekebisho yote yaliyopendekezwa na kamati kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Hili ni jambo zuri na la kupigiwa mfano. Hii maana yake nini, wameifanyia kazi sana au wameufanyia kazi mswada wetu mpaka chini kabisa kwenye *root* wamefika na wamefanya kazi. Hii kamati Mhe. Naibu Spika, kama kuna utaratibu wa kupewa zawadi nadhani wanastahiki kupewa zawadi. *(Makofi)*

Nimshukuru sana Mhe. Ali Suleiman Ali ana jina kubwa huyo, maana yake mimi ni Haroun Ali Suleiman sasa na yeye ni Mhe. Ali Suleiman, kwa kukubali mswada huu na kukubaliana na adhabu hasa zilizoainishwa katika vifungu 109, 110, 111, 112, 113, 114 na 115. Vyote hivi tumevipokea na tunamshukuru sana kwa kuviunga mkono na tunamuahidi kwamba safari hii serikali hii tujue kwamba kama ilivyo siku zote itazidi kusimamia masuala haya kuhakikisha kwamba wale wananchi wetu waliokuwa wanapata matatizo, wanalalamika hawaendelei kupata matatizo yale tena.

Mhe. Zulfa Mmaka Omar kwa upande wake naye amechangia mchango wake uliohusu suala la dhamana, ambapo suala hilo haliko katika mswada huu bahati mbaya. Sheria ya Adhabu, yaani Mswada huu wa Sheria ya Adhabu bali liko katika Mswada wa Sheria ya Mwenendo wa Jinai huu ambao tutauwasilisha muda mfupi ujao.

Aidha, alitaka kujua juu ya makosa ya mtandao hasa usambazaji wa picha za ngono na ujumbe wa simu *message*. Makosa haya hayakuingizwa kwenye mswada huu kwa sababu tayari kuna Sheria ya Makosa ya Mtandao ya Tanzania ambayo imesharidhiwa na Baraza la Wawakilishi na tayari inatumika Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Shehe Hamad Mattar tunaupokea sana ushauri wake na tunamshukuru. Kuhusu marekebisho madogo madogo tutajitahidi kuwa makini zaidi katika kuyafuatilia na kuyarekebisha hayo.

Kuhusu adhabu ya kosa la kuua mtoto mchanga katika kifungu cha 187 ambalo pia limechangiwa na Mhe. Rashid Makame Shamsi. Bado tunaamini adhabu hiyo sio ndogo hasa kutokana na mazingira ya kosa hilo.

Kuhusu kosa la wizi wa karafuu katika kifungu 267 imekusudiwa kuwa karafuu ambazo ni mali ya serikali au mashirika yake. Makosa ya karafuu ambazo ni mali ya mtu binafsi na ya ujumla wake yametajwa katika Sheria ya Maendeleo ya Karafuu Nam. 2 ya mwaka 2014. Utaratibu wa kupanda mikarafuu na kuilea inategemea maandalizi ya maelekezo yaliyotolewa na Chuo cha Mafunzo.

Mhe. Asha Omar Mussa ushauri na maoni yake yamepokewa na tunamshukuru sana kuhusu adhabu kwenye kifungu 114 na 135

tunakubaliana na yeye moja kwa moja Mheshimiwa. Katika kifungu cha 114 ndio itumike pia katika kifungu cha 135 na hilo tunakubaliana naye.
Mhe. Rashid Makame Shamsi tunakubaliana naye kwamba kuongezeka kwa adhabu sio muarubaini wa kupunguza makosa, suluhisho la msingi ni jamii kubadilika na kubadili maadili. Hilo ni kweli kabisa na ni sahihi, kama jamii hatujabadilika katika suala hili tutapata mitihani mingi. Kwa hivyo, lazima kila mmoja awe ni mwalimu wa mwenzake na jamii lazima ibadilike katika suala hili.

Halikadhalika alizungumza suala zima la kutembea nusu uchi kwa kuvaa nguo fupi za karaha ni suala la kimaadili zaidi kuliko kisheria. Kwa mantiki hiyo, viongozi wa dini, viongozi wa siasa na jamii kwa jumla tujitahidini kushirikiana katika kuimarisha maadili yetu sote jukumu letu. Hata sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tuna wajibu huo.

Kuhusu upimaji wa mizani ya akili, mara zote upimaji wa mizani ya akili ni suala la kitaalam linalothibitishwa na ushahidi wa daktari, mtaalam wa magonjwa ya akili.

Kuhusu uwezekano wa mtoto wa kike kujifungua. Uwezekano wa mtoto wa kike kujifungua upo kutokana na kuwepo kwa tatizo la mimba za utotoni. Kuhusu ushauri wa kupunguza adhabu katika kifungu 319(b) na (c) kwa kweli makosa hayo, adhabu hizo zimefanyiwa utafiti wa kina na kwa vile madhara yake ni makubwa bado tunaona zibakie kama zilivyopendekezwa katika mswada huo.

Mhe. Said Omar Said tunamshukuru kwa mchango wake mzuri na muhimu sana hususan katika kuunga mkono hoja za serikali kuhusu mapendekezo ya mtiririko wa adhabu zilizotajwa katika

kuweka dhamana kwa ajili ya kutunza amani na kuwa na tabia njema.

Kifungu 142, amependekeza maneno "bila ya ruhusa ya mume wake" yaondoshwe, kwani hakuna mume atakayeruhusu mke wake afanye uzinifu. Pia hoja hiyo imechangiwa na Mhe. Mussa Foum Mussa ambaye alipendekeza kifungu 142(2) kisiwepo. Sheria hii ni kwa ajili ya watu wote waliopo Zanzibar, yaani Wazanzibari na hata wageni wanaokuja Zanzibar. Hivyo, kuna umuhimu wa maneno hayo kubakia kwani baadhi ya wageni wanaoingia Zanzibar wana utamaduni tofauti.

Kuhusu tofauti ya adhabu baina ya mkosaji mwanamme na mkosaji mwanamke kwenye kifungu 143 ambacho pia kimechangiwa na Mhe. Mussa Foum, hii inatokana kuwa mwanamme ana uwezo wa nguvu kubwa zaidi ya ushawishi kuliko mwanamke.

Kuhusu adhabu ya kukashifu dini nyengine ambayo pia imechangiwa na Mhe. Suleiman Sarahan Said, tunaona kwamba adhabu iliyopendekezwa inatosha. Mhe. Suleiman Sarahan tunamshukuru kwa mchango wake na kuunga mkono hoja.

Kuhusu kuelimisha jamii juu ya sheria kuhusu kifungu cha Nam. 6. Ushauri huo ni mzuri na tunaupokea. Pia Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi amechangia kuhusiana na kifungu hiki.

Kuhusu ugonjwa wa akili kuwa usitumike kama kisingizio cha kufanya makosa. Tunakubaliana naye na kwa hivyo ndivyo itakavyotekelezwa na Mahakama wakati wa uendeshaji wa kesi.

Kuhusu umri mdogo kuangaliwa vizuri zaidi. Jambo hilo limefanyika na sheria hii imeoneshwa na Sheria ya Watoto Nam. 6 ya mwaka 2011. Kuhusu kifungu cha 26 cha adhabu ya faini

kuendana na kifungu, tunakubaliana naye kwamba isomeke "faini isiyozidi shilingi milioni mbili".

Kuhusu ushahidi wa kosa la usagaji katika kifungu cha 136 ambalo pia limechangiwa na Mhe. Mussa Foum Mussa. Ushahidi wa kosa hilo unaweza kuwa ni moja kwa moja au kwa kimazingira.

Kuhusu suala la wezi wa Mahakama kutozwa faini, suala hili liko katika mswada wa mwenendo wa jinai utakaowasilishwa hivi punde.

Aidha, tunakubaliana na Mhe. Suleiman Sarahan kwamba utekelezaji wa sheria hii unahitaji ushirikiano mkubwa miongoni mwa vyombo vyote vya usimamizi wa jinai.

Mhe. Mwanaasha Khamis Juma, Mwenyekiti wa Baraza kuhusu kosa la kujaribu kutorosha. Kosa hilo lipo katika mswada huu kwenye kifungu 388 na 389. Kuhusu kifungu cha 222 kuhusiana na uondoshaji wa viungo vya binadamu. Daktari mwenye sifa zinazokubalika anaweza kufanya hivyo iwapo tu, atatekeleza masharti yote yaliyotajwa kwenye kifungu hicho ikijumuisha kwamba, idhini ya mhusika au idhini ya mtu wa karibu mzee au mlezi.

Kuhusu kupokea mali za wizi katika kifungu cha 309. Kifungu hicho kimejumuisha kuuza na kununua mali ya wizi kwani limetumika neno kuhaulisha ambalo kisheria linatumika katika miamala ya kuuza, kununua, kuweka rehani na kuondosha.

Mhe. Tatu Mohamed Ussi tunamshukuru kwa kuunga mkono marekebisho ya kamati kifungu 119 ya kuongeza adhabu ya kifo kwa kipindi cha miaka kumi badala ya miaka mitano.

Kuhusu kifungu 151 kupuuza kutoa chakula kwa watoto au mtu mwenye ulemavu, 197 kusaidia kujiua na 198 kujaribu kujiua. Adhabu zake zinapatikana katika kifungu 26(1) kinachoeleza kuwa: "Pale katika sheria hii hakuna adhabu iliyotamkwa kwa kosa lolote, kosa hilo litaadhibiwa kwa adhabu za kifungo kisichozidi miaka miwili na kulipa faini isiyozidi shilingi milioni mbili au vyote viwili kwa wakati mmoja".

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Omar Seif Abeid na waheshimiwa wengine waliobakia wote sitawataja maelezo yao yalitolewa kwa ufasaha na Mhe. Naibu Waziri, sina haja ya kuyarejea yote yale.

Mhe. Naibu Spika, mwisho kabisa naomba nithamini sana michango iliyotolewa na Waheshimiwa wote katika mswada huu na naomba sasa nitoe hoja.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe Mhe. Waziri ameshatoa hoja sasa niwaulize wale wanaokubaliana na hoja hiyo wanyooshe mikono. Wanaokataa, wanaokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Kutunga ya Sheria ili kupitia mswada huu kifungu kwa kifungu.

KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe kutokana na ukubwa wa mswada wetu mswada huu tutaupitisha kwa mafungu. Kwa hiyo, kwa wale wote ambao watakuwa wana maeneo ambayo wanataka kuyajengea hoja au kuyapigia buti wawe makini sana katika mafungu na sio vifungu. Kwa maana hiyo, tutakwenda sehemu kutoka Sehemu ya Kwanza mpaka Sehemu ya Arobaini ya mswada huu.

Mswada wa Sheria ya Adhabu, 2018

Sehemu ya Kwanza

Masharti ya Awali

Kifungu 1-3

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nachangia Sehemu ya Kwanza kifungu namba 27 kinachohusu haini nilisema kwamba...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa bado hatujafika.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 4 Mamlaka ya Mahakama ya Zanzibar kwa madhumuni ya sheria hii ni sehemu yoyote ndani ya Zanzibar na sehemu yake ya bahari na makosa yatakayotendwa kwenye Bahari Kuu katika vyombo vilivyosajiliwa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, hapa nilikuwa na hoja nzito, tuna mahakama zetu, tuna wanasheria wetu, tuna *DPP* wetu, tuna magereza yetu, tuna Sheria zetu. Nilikuwa naomba kiongezwe kifungu cha mtu pindipo atakapokamatwa Zanzibar ahukumiwe hapa Zanzibar asije kupelekwa Bara. Nilikuwa nina mapendekezo hayo kwa maslahi ya nchi tumeona mifano chungu nzima imejitokeza. Sasa

sijui waziri atakuwa tayari kupokea mawazo haya kwa faida ya nchi wala si kwa faida ya Jaku Hashim Ayoub.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, kwanza kifungu cha 4 kama kilivyo hakina matatizo kwa hoja ya Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Lakini Mhe. Jaku Hashim Ayoub anataka tuongeze maneno ambayo yeye anaona kwa mazingira ambayo yanatokea labda anaona suluhisho ni kuandika kifungu kipya. Lakini nataka nimwambie Mhe. Jaku Hashim Ayoub kuna utaratibu, kuna sheria inaitwa *Extradition Act* ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania unaweza ukatenda makosa sehemu nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini ukachukuliwa na ukenda na ukashtakiwa sehemu nyengine.

Sasa si tatizo kama utaratibu wa kisheria utakuwa umefuatwa na umeelekeza hivyo. Si tatizo kwa mtu yeyote ambaye anaweza akachukuliwa kwa sababu kuna sheria ya *Extradition* ambayo inaruhusu utaratibu huo. Kwa makosa ambayo yanatumika Zanzibar sheria hii ndio itatumika na kwa makosa mengine yoyote ambayo utaratibu utaelezwa kisheria basi utafuta ule utaratibu ambao upo kisheria.

Sasa kwa kifungu hichi mimi sina khofu ambayo anayo Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwa sababu tu ya mazingira ambayo yanatokea na ambayo hatuna *full detail* zake mpaka tukataka kuongeza na vifungu ambavyo kwa maana yoyote vile havitoweza kutumika Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, nimemsikia sana Mhe. Mwanasheria Mkuu nasema hili si maslahi yangu tumeshuhudia ndio yale tuliyokuwa tunapiga kelele Dkt. Kabudi, Profesa Kabudi ndio haya mnatupa wakati mgumu wakati mwengine kule Bungeni. Tuna mahakama yetu, tuna sheria zetu, tuna *AG* wetu ambaye ni wewe, tumeshuhudia watu kuchukuliwa

hapa hivi majuzi tu. Kwani kuongezwa hichi pesa zikabaki hapa kuna matatizo gani.

Hivi sasa nyie mnavutana huko ndani hamjui watu muwapeleke mahakamani kwa kifungu gani na hilo nalijua si pahala pake pa kuzungumza. Mimi nikuombe tena kwa unyenyekevu wa hali ya juu Mheshimiwa *AG* hili kwa maslahi. Leo baada ya siasa kuna maisha nje, baada ya uhai kuna mauti, baada ya ujana kuna uzee, tufikiri hili kuna pesa hapa zinaweza zikapatikana tusaidiane, vyenginevyo...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim Ayoub umemaliza.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Nimemaliza.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Jaku Hashim Ayoub pia angesoma sura ya 4 sehemu ya 4 ya Katiba kuanzia kifungu cha 101 ambacho kinasema:

"Hati zenye maagizo yaliyotolewa na Mahakama za Tanzania Bara na Mahakama za Zanzibar katika mashauri ya madai ya aina zote na mashauri ya jinai ya aina zote pamoja na hati za kuamuru kukamatwa watu zinaweza kupelekwa mwahala popote nchini Tanzania na maagizo hayo yanaweza kutekelezwa mwahala popote nchi Tanzania kwa kufuata masharti yafuatayo".

Sasa utaratibu huu wa kisheria ukifuatwa hakuna mashaka yoyote kama kesi hizo zitafuata utaratibu wa kisheria ambao upo. Sasa Katiba imeshaeleza hivyo iko wazi tunachozungumza hapa ni kama hayo mambo yenyewe yaelezwe kisheria na yafuatwe masharti ambayo yameelezwa kwenye sehemu hii ya 4 kuanzia 101 cha Katiba ya Zanzibar.

Sasa khofu ya Mhe. Jaku Hashim Ayoub, yeye sasa hoja yake ingelikuwa utaratibu uko wa Kikatiba. Lakini haufuatwi, hiyo haufuatwi ingelikuwa ndio hoja yake. Sasa hiyo tungeweza kumjibu lakini asiseme kama hakuna utaratibu wa kuweza hizi hati au watu kukatwa sehemu yoyote ya Jamhuri kwa sababu kifungu cha 101 ndio kinaeleza hivyo cha Katiba. Hata ya Jamhuri ya Muungano nacho kuna kifungu kama hichi kinachoeleza hivyo hivyo Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim Ayoub mara ya mwisho.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kama utaratibu haufuatwi sasa basi ndio hicho ninachosema ndio huyo anayechukua hapa, pana kesi imefunguliwa Mahakama Kuu juzi hapa hapa akatoka kiongozi akampeleka mtu Dar es Salaam na Mahakama imeshafunguliwa hii ni kudharau Mahakama zetu. Kwa hiyo, tuweke *specific* kwa atakayefanya kitendo hichi basi aadhibiwe yeye, juzi kesi imeshafunguliwa Mahakama Kuu na iko Mahakamani, katoka kiongozi tu kampeleka mtu. Kwa maana hiyo, tusije tukajilaumu tuna sheria zetu, tuna magereza yetu...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim Ayoub tuendelee basi nafikiri umeshafahamu Mwanasheria Mkuu alivyofahamisha.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mimi sijawahi kuona mtu akakamatwa Muscat akaletwa Tanzania, wa Tanzania Bara hajaletwa Zanzibar, kwa nini sisi tuwapeleke kule, anayekamatwa Pakistan na unga mwache aletwe huku. Dunia nzima unapofanya kosa ndipo unaposhtakiwa ndio sheria zilivyo za dunia, sijapata kuona kitu kama hicho mimi, tusisokomezane tu tujenge hoja. Haya maisha...

Mhe. Mwenyekiti: Tunaendelea Mhe. Jaku Hashim Ayoub.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Aah bado mimi sijakubaliana na kifungu hichi.

Mhe. Mwenyekiti: Basi nahoji Wajumbe, wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Jaku Hashim Ayoub wanyooshe mikono, wanaokataa. Wanaokataa wameshinda. Tuendelee. (*Makofi*)

Sehemu ya Pili

Eneo la Matumizi ya Sheria

Kifungu 4-5 Eneo la Matumizi ya Sheria

Sehemu ya Tatu

Misingi ya Ujumla kuhusu Uwajibikaji wa Kijinai

Kifungu 6- 21 Pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Nne

Washiriki kwenye Makosa

Kifungu 22-24 Pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Tano

Adhabu

Kifungu 25-26 Pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Sita

Uhaini na Makosa Mengine dhidi ya Serikali

Kifungu 27-44 Pamoja na marekebisho yake

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mimi niko kwenye uhaini, nchi yetu ni nchi ya kimapinduzi. Namshukuru sana Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa ku-*acknowledge* kwamba sasa atakayehukumiwa kwa uhaini kesi yake haitokwenda kwenye Mahakama ya Rufaa.

Lakini tujue umuhimu na uzito wa hili jambo lenyewe la uhaini ni jambo kubwa hasa katika nchi yetu ya kimapinduzi maana yake lazima tufike pahali mtu hata asi-*attend* kutaka kujaribu kufanya kosa la uhaini nchi hii.

Sasa nilikuwa namuomba Mwanasheria Mkuu anikubalie kitu kimoja. Kifungu cha 99 cha Katiba ya Zanzibar imeyataja makosa ambayo hayaendi katika Mahakama ya Rufaa.

(a) tafsiri ya Katiba hii;
(b) mambo ya Kiislamu ambayo yameanzia katika Mahakama za Kadhi;
(c) mambo mengine yoyote yaliyoainishwa katika Katiba hii na Sheria nyengine yoyote iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi.

Sasa nilikuwa namuomba Mwanasheria Mkuu anikubalie kwamba suala hili la uhaini nalo litaingia kuwa (d) katika Katiba ya Zanzibar kwamba haitokwenda rufaa kwa nini? Kwa sababu Katiba ndio Sheria Mama kuliko sheria yenyewe. Kwa hivyo, aliingize kwenye Katiba kwa sababu Katiba ndio Sheria Mama na ndio sheria kubwa inayofuatwa. Kwa hivyo, anikubalie hilo na ili kwa sababu kesi yenyewe ya uhaini ni kesi kubwa kwa nchi yetu ya kimapinduzi ili tuendelee mbele.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, wakati Mhe. Hassan Khamis Hafidh alipokuwa akitoa hoja yake na wakati mimi nikichangia hoja hiyo vifungu ambavyo ame-*refer* ndio vifungu ambavyo nimevitaja katika kuchangia hoja yangu. Nikasema kwamba Katiba yetu kuanzia kifungu cha 99 imetoa aina ya kesi ambazo zinakwenda Mahakama ya Rufaa na kesi ambazo haziendi Mahakama ya Rufaa. Katika mashauri ambayo yametajwa moja kwa moja ambayo hayaendi Mahakama ya Rufaa ni tafsiri ya Katiba. Hilo la kwanza.

La pili, Katiba ikasema mambo ya kiislamu ambayo yameanza katika Mahakama ya Kadhi haya ni maeneo ambayo yametajwa moja kwa moja na Katiba. Lakini Katiba kwenye kifungu cha (c) kikatoa fursa kwa maeneo mengine ambayo ama yatatajwa na Katiba ama yataelezwa na sheria ambayo imetungwa na Baraza la Wawakilishi.

Kwa hivyo, hoja ambayo amekuja nayo tumesema tumeipokea na tutatumia masharti ya kifungu cha 99(c) ya kutaja kwenye mswada ambao tunapitisha kama makosa hayo hayatokuwa ni katika makosa ambayo yanakwenda kusikilizwa na Mahakama ya Rufaa. Hayo ndio ambayo tumeyaeleza na nadhani Mhe. Waziri nae aliyajibu hayo hayo. Kwa hivyo, hoja aliyoisema ndio hoja ambayo ilikuwa na serikali. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Mwanasheria Mkuu nafikiri hoja yangu ameanza kunifahamu, lakini hajanifahamu.

(a) Imesema wazi wazi tafsiri ya Katiba hii, Katiba ya Zanzibar imeitaja tafsiri ya Katiba hii.
(b) Imesema wazi wazi mambo ya kiislamu imeyataja, lakini na
(c) Kwa mujibu wa Katiba imesema mambo mengine.

Sasa mimi nilikuwa namuomba yatakapokuja mabadiliko ya Katiba kutokana na umuhimu wa hili suala lenyewe la uhaini liingizwe siku itakayokuja mabadiliko ya Katiba kwa sababu hili suala ni muhimu. Ndio suala langu lipo hapo tu hoja yangu nimekubali ame- *acknowledge* na amenifahamu. Lakini kutokana na uzito wa mambo yenyewe kiislamu imetiwa tafsiri ya Katiba. Je, uhaini nchi yetu ya kimapinduzi nayo itiwe ndani ya Katiba kwa kuzingatia Katiba ndio sheria kubwa kuliko sheria zenyewe. Naomba kuwasilisha Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hassan Khamis Hafidh tunaendelea kwa sababu Mhe. Mwanasheria Mkuu pamoja na Mhe. Waziri wamelieleza wazi. Tusubiri mpaka huo wakati wake na wewe ndio ulivyosema. Mabadiliko ya Katiba ndiyo ambayo hayo yatakuwa *endorse* nafikiri ndio nilivyomfahamu Mwanasheria Mkuu pamoja na Mhe. Waziri.

Kwa hivyo, naomba tuendelee kwa sababu maelezo mengine yameshaelezwa na wewe ulivyoelezea umefahamu vizuri sana. Inaonesha umefahamu vizuri sana majibu yameshatoka. Mhe. Hassan Khamis Hafidh majibu yameshatoka.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Kwa heshima yako Mhe. Mwenyekiti, naomba tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante, tuendelee.

Sehemu ya Sita

Uhaini na Makosa Mengine dhidi ya Serikali

Kifungu 27-44 Pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Saba

Makosa Yanayoathiri Mahusiano ya Nchi za Nje na Utulivu wa Nje

Kifungu 45-47 Pamoja na marekebisho yake

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu cha 46(2) nilichangia lakini majibu hayakuniridhisha na nilisema 46 (2)(a) ilikuwa inazungumzia suala la taasisi ambayo inamhusu Mhe. Rais na Katibu Mkuu Kiongozi. Katika maudhui mazima ya hapo nikasema katika busara za hapa tusichanganye Taasisi ya Mhe. Rais kwenda kupokea ile *notice* au *notice* hiyo wakati huo huo aipokee Katibu Mkuu Kiongozi na nikasema abakishwe Rais ila Katibu Mkuu Kiongozi aondoke. Kwa hiyo, hapo sikupata majibu sasa naomba kupata majibu.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, utaratibu wa kumtaja Katibu Mkuu Kiongozi ni mgeni katika sheria zetu za Zanzibar. Ukisoma sheria namba 3 ya mwaka 2010 ambayo inasimamia madai yote ya serikali inaeleza wazi kuwa pale ambapo unataka kushtaki serikali basi taarifa hiyo utapeleka kwanza kwa Katibu Mkuu na utatoa *notice* ya siku 60.

Kwa hiyo, utaratibu wa kumtaja Katibu Mkuu Kiongozi si utaratibu mgeni kwa sheria zetu, ametajwa kwenye sheria namba 10 ambayo ni *Government Ac*t na anatajwa pia kwenye sheria hii ambayo pia inaongoza mambo ya jinai. Kwa hiyo, si utaratibu mgeni wa kumtaja Katibu Mkuu Kiongozi kwenye sheria zetu. Ni utaratibu wa kawaida na ambao unatumika.

Kwa hiyo, nimuombe Mhe. Miraji Khamis Mussa kama kifungu kilivyo hakina matatizo wala asiwe na khofu ya kwamba atakuja Katibu Mkuu Kiongozi mwengine na anaweza akawa na mambo

mengine. Ni utaratibu wa kawaida na wa kisheria ambao upo kwenye sheria hii.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, mimi khofu sina, wasi wasi wangu kuchanganya taasisi kubwa ya Mhe. Rais na mtendaji wa serikali kwenye taasisi hii ambao moja kwa moja wajibu unakwenda kwa Rais kama hujampata Rais maana yake au uende kwa Katibu Mkuu Kiongozi. Mashaka yangu kuchangia taasisi hizi wakati fulani leo tuna Katibu Mkuu Kiongozi ambaye ana busara sana, mtu mmoja mzuri tu tunamuamini na hakuna tatizo. Lakini anaweza kuja kutoa Katibu Mkuu Kiongozi asifanane na yeye akaja akapokea kitu hicho ambacho kikamuathiri hata huyo Rais ambaye pengine tumemtaja kwenye sheria ndio dhamira yangu. Hatuoni maana yake tunaanza kutengeneza mazingira ambayo wakati fulani yanaweza yakawa si rafiki. Mimi nikipata majibu hayo mazuri Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa umesema unataka majibu. Nimesikia kama umesema mwisho tuendelee.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Nimesema hivi wasi wasi wangu katika mazingira ya maneno niliyoyasema yalishamaliza wala sitaki kurejea na Mwanasheria Mkuu kanifahamu vizuri. Akishayatoa hayo majibu mazuri ambayo yatakuwa kwenye *hansard* za Baraza hili basi tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mwanasheria Mkuu majibu yake nafikiri atarudia yale yale ni utaratibu wa serikali kutumia katika sheria nyengine jina la Katibu Kiongozi. Sidhani kama Mheshimiwa labda uongezee.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mheshimiwa majibu ambayo nimeyatoa ndio hayo hayo na kama nilivyosema hii sio sheria ya

kwanza inayomtaja Katibu Mkuu Kiongozi na nimetaja sheria namba 10 ya mwaka 2010 ambayo inaitwa *Government Proceeding Ac*t. Lakini kwenye hii wala haichukui kazi anachotakiwa kupeleka ni kutoa *notice* ama kwa Rais ama kwa Katibu Mkuu Kiongozi kwa yeyote atakayetoa ile *notice* itakuwa imefika. Kwa hiyo, hakuna dhara lolote la kisheria kumtaja Katibu Mkuu Kiongozi.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante, tuendelee.

Kifungu 45-47 Pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Nane

Mikusanyiko Isiyo Halali, Maandamano, Ghasia na Makosa Mengine dhidi ya Utulivu wa Jamii

Kifungu 48-74

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Wenye serikali wapo kujibu wao hizi hoja. Nilichosema mimi kifungu cha 52 kwamba Rais ana majukumu mengi sio kila kitu tukamtwisha Mhe. Rais tumuonee huruma. Kifungu cha 52 pamoja na watoto wake wote Mhe. Mwanasheria Mkuu angalia. Rais huyu tutamtosha tumuonee huruma kazi kubwa anayofanya, kuna Makamishna, kuna watendaji kiondoeni hichi kifungu Rais ana majukumu mengi tena mazito ya nchi hii kutoka mwanzo mpaka na vitoto vyake hivi hebu viangalie.

Mimi sina hoja kubwa kwa kumpenda Rais wetu majukumu mengi aliyokuwa nayo, wala mimi sina hoja mkikubali sawa, mkakipitisha sawa, wala sina hoja. Lakini Rais ana majukumu mengi. Leo hospitali tunamsubiri yeye, wala sina hoja mkikubali sawa, hamkukubali sawa huu umoja mimi sisimami tena.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mheshimiwa pamoja na maelezo ambayo ameyatoa Mhe. Jaku Hashim Ayoub ya majukumu mengi ambayo anayo Mhe. Rais na haya ni miongoni mwa majukumu yake ambayo anayo Mhe. Rais.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, katika eneo hilo kifungu cha 49(2) nilichangia kuwa hii adhabu ya shilingi laki tatu ni ndogo sana maana tunachokizungumza ni yale makosa ya mikusanyiko isiyo halali na tumeona nchi yetu ilikumbwa na mikusanyiko kama hiyo sana. Sasa leo unawakamata hao unakwenda kuwapeleka pale tu adhabu yake ni shilingi laki tatu ni kama tunacheza wakati kule kwengine tumeweka maisha. Lakini eneo hili ambalo ni athari katika nchi yetu tumeweka adhabu ya shilingi laki tatu, nikatoa mapendekezo angalau iwe ni shilingi milioni tatu nilikuwa nasubiri majibu ya serikali.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe Mwenyekiti, pendekezo la Mhe. Miraji Khamis Mussa la kuongeza faini kutoka shilingi laki tatu sio pendekezo baya. Lakini nadhani shilingi milioni tatu kenda mbali zaidi. Mimi nadhani kwa kosa lenyewe lilivyo *of course* yeye kasema faini lakini kawacha kifungo cha miezi mitatu kama kilivyo. Mimi nadhani shilingi milioni moja sio mbaya lakini isipindukie tena shilingi milioni tatu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Miraji Khamis Mussa.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana Mwanasheria Mkuu kwa kunielewa katika eneo hili. Lakini naomba akubaliane na mimi hizi jumuiya, maana hapa kikubwa tunazungumzia hizi jumuiya na ndio zinazoandaa haya na nchi yetu kuingia kwenye rehani kwa shilingi milioni moja

kama alivyozungumza yeye, naiafiki ile lakini katika utaratibu wa kupitisha sheria sikubaliani nao. Mimi naomba angalau ziwe shilingi milioni mbili kwa sababu hizi jumuiya tunazijua zinatuadhibu sana katika mambo yao haya, basi angalau hii adhabu iwe shilingi milioni mbili. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, kwenye kifungu hichi kuna adhabu mbili zilizotajwa, adhabu moja ni ya faini ya shilingi laki tatu au kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi mitatu ambayo kwa sasa hivi ipo. Maana yake haya sasa anayeamua ni yule hakimu ambaye anayesikiliza hiyo kesi ama yule mtu ampe adhabu ya faini ya shilingi laki tatu au ampeleke ndani kwa muda wa miezi mitatu. Sasa Mhe. Miraji Khamis Mussa kwenye kupeleka ndani miezi mitatu hana hoja hii anafurahia anaona safi hiyo miezi mitatu. Lakini hoja yake iko kwenye shilingi laki tatu na mimi nikasema kwa sababu na hiyo adhabu ya kifungo ni miezi mitatu, basi angalau hiyo faini itoke kutoka laki tatu iwe shilingi angalau milioni moja tusiende shilingi milioni tatu itakuwa tumekwenda zaidi hata hiyo adhabu ambayo anataka kupewa.

Kwa hivyo, adhabu ni faini ama aende ndani miezi mitatu. Mimi nilidhani hoja yake ingelikuwa aah! isiwe au iwe vyote viwili hiyo ingekuwa hoja sahihi. Lakini yeye yuko kwenye adhabu na mimi pendekezo langu ambalo naliomba Wajumbe walikubali ni iwe angalau basi shilingi milioni moja kuliko milioni tatu. Nashukuru.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na Mwanasheria Mkuu unapopandisha ile milioni moja mimi kifungu hiki chote kizima nilisema kiende mbele, lakini katika mazingira hayo hiyo milioni moja naikubali yake yeye lakini na hiyo adhabu

ya miezi mitatu iondoke iwe mwaka mmoja, angalau iwe hivyo nakubaliana na hivyo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mwanasheria Mkuu.
Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, adhabu ya faini kwa sababu alichangia kwenye hoja yake. Lakini hii kwa sababu tunapitisha vifungu huwezi tena ukaanzisha hoja mpya ya kusema pia na adhabu iwe ya miezi, hapana sio huo utaratibu wa kikanuni. Ile ya mwanzo kwa sababu alichangia na aka-*propose* na hiyo tumekubali kama angalau iwe shilingi milioni moja. Lakini huwezi sasa hivi tunapitisha vifungu ukasema aah! sasa nimetamkiwa pia na adhabu nayo pia iwe. Namuomba Mhe. Miraji atukubalie. Mheshimiwa nakushukuru. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Tumekuelewa Mwanashiria Mkuu, tunaendelea tumekubaliana hapa tutakuwa na adhabu ya shilingi milioni moja hayo ni marekebisho. Lakini suala la kifungo kisichozidi miezi mitatu kitabakia kuwa hivyo.

Kifungu 48-74 Pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Tisa

Makosa Yanayohusu Usimamizi wa Haki

Kifungu 75

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim Ayoub.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Narudia tena Mwanasheria Mkuu ni msomi, kifungu cha 84(3) mali ya thamani iliyotaifishwa itashughulikiwa kama ambavyo Rais anaweza kuelekeza bado tunaendelea tena wala sina kishindo tunamtwisha Mhe. Rais mzigo. Hizi sheria mkikaa mziangalie mzipime haya mengine sio

leo *TRA* tu wametaifisha mali, hebu angalieni haya mambo jamani mimi elimu yangu ndogo mpaka leo hii. Basi kila kitu kisingizio Mhe. Rais, kuna Mahakama, vile vile *TRA,* vile vile ina uwezo *ZRB* wanataifisha mafuta wanauza, sasa tafuteni hivyo vifungu vyengine huyo Rais mmoja tutamchosha, hata akilala kachoka kila kiapo kisingizio Mhe. Rais.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim Ayoub sema hoja yako.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Hoja yangu mimi namuonea huruma Mhe. Rais, nafikiri sote tunamuonea huruma Mhe. Rais humu juzi katununulia magari mawaziri na manaibu mawaziri magari mapya.

Mhe. Mwenyekiti: Sasa nini mapendekezo yako.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Atafutiwe kamishna mtu mwengine sio kila kitu Mhe. Rais.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwa kujali majukumu ambayo anayo Mhe. Rais nimpongeze sana kwa hilo. Lakini pia nimkumbushe Mhe. Jaku kama Mhe. Rais pia katika kutekeleza majukumu yake anatekeleza majukumu yake ambayo amepewa pia na sheria, hayo ndio majukumu ambayo anatakiwa Mhe. Rais ayatekeleze.

Kwa hivyo, miongoni mwa sheria ambazo anatakiwa Mhe. Rais atekeleze majukumu yake ni kifungu hiki ambacho nacho pia tunakipitisha. Kwa hivyo, asione tabu Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mhe Rais kamsikia na katambua kama anajali na anamuonea muhali lakini ndio kazi zenyewe zilivyo. Kwa hivyo, naomba

atukubalie kifungu hichi kipitishwe kwa sababu Mhe. Rais anasimamia majukumu yake kwa mujibu wa sheria na sheria zenyewe ndio hizi ambazo tunazipitisha Mheshimiwa. *(Makofi*)

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, mimi wala sitaki kujipendekeza kwa Mhe. Rais kama nataka uwaziri au naibu waziri, aaa siko huko kabisa, sitaki uwaziri wala unaibu waziri. Lakini Mwanasheria mengine haya uyapime sio kila kitu ndicho, sio kama swahaba hukosei kuna mengine mnateleza ndio maana tukawa *backbencher* kukuhojini huku. Mheshimiwa tuendelee.

Sehemu ya Tisa

Makosa Yanayohusu Usimamizi wa Haki

Kifungu 75-87 Pamoja na Marekebisho yake

Sehemu ya Kumi

Kuokoa, Kutoroka na Kuwazuia Watumishi wa Mahakama

Kifungu 88-93

Sehemu ya Kumi na Moja

Makosa Mchanganyiko dhidi ya Mamlaka ya Umma

Kifungu 94-99 Pamoja na Marekebisho yake

Sehemu ya Kumi na Mbili

Makosa Yanayohusiana na Dini

Kifungu 100-106 Pamoja na Marekebisho yake

Sehemu ya Kumi na Tatu

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, shughuli zinaanza sasa …

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku sijakupa ruhusa ya kuzungumza…

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Hili linatuhusu waislamu humu ndani kwa asilimia kubwa, sasa hapa tena kama patapigwa kura patatendeka hili, halihusu. Asilimia 99 humu tumo waislamu na hili hata Mwenyezi Mungu amelikataza na nikatumia hadithi *"Manraana min*…

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa kifungu gani unachokizungumzia

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kifungu cha 108(2)

Mhe. Mwenyekiti: Endelea.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mahakama mtu mwanamme anatenda kosa la kubaka ili ikiwa anamuingilia kingono mtu mwanamke katika mazingira yaliyopo pamoja na maelezo yafuatayo.

Ambaye si mke wake au mke ambaye ametenganishwa nae kisheria bila ya ridhaa yake wakati wa maingiliano ya kingono, hichi waislamu hakitufai. Mahakama kazi yake ni kupatanisha haiwezekani kugombana na mkeo halafu ukatenganishwa hakitufai kabisa ni dhambi kubwa hili mimi silikubali kabisa. Ikipigwa kura natoka natumia ile hadithi niliyosema mimi hili silikubali kabisa naisimamia dini yangu haya maisha ni ya muda mfupi, maisha ya kweli yako mbele safari hili mimi silikubali hata

kwa mikwaju. Hili kama kukipitisha kifungu mimi nitoke nje, kama mtahoji nitoke kabisa. Mwenyezi Mungu atakwenda kuniuliza "*kulukum rai wakulukum mas-ulu an raiyatih"* maana yake kila mmoja ni mchunga na kila mmoja ataulizwa kwa alichokichunga. Kwa hili mimi silikubali nataka maelezo ya serikali.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na namshukuru sana Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwa kutukumbusha pia kwa ku-*refer* hadithi, sasa sina hakika kama sahihi au dhaifu hiyo hadithi ambayo ameitoa. Lakini nimshukuru kama bado anajali na anajenga hoja yake vizuri. Lakini Mhe. Mwenyekiti, ukikisoma kifungu chenyewe kilivyo wala mimi sioni kama kina matatizo.

Kwa sababu kifungu kinasema mtu mwanamme anatenda kosa la kubaka ikiwa anamuingilia kingono mtoto wa kike au mwanamke katika mazingira yaliyopo katika moja ya maelezo yafuatayo.

(a) Ambayo ndio Mhe. Jaku Hashim Ayoub anajenga hoja yake inasema ambaye si mke wake. Kwa hivyo, kama sio mke wako wewe unatafuta nini kuingiliana nae kingono.

(b) Ikiwa mke wake ambaye ametenganishwa nae kisheria, kisheria umetenganishwa nae, kisheria sio mke wako tena bila ya ridhaa yake wakati wa maingiliano ya kingono, tena wametenganishwa kisheria na bila ya ridhaa ya huyo mwanamke. Mbona kifungu kipo vizuri wala hatutoingia motoni kwa kifungu hichi. Mhe. Mwenyekiti, nadhani sote tutaingia peponi kwa kuweka kifungu kizuri cha namna hii.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, mimi nilidhani Mwanasheria ni msomi wa kweli kweli kumbe hata elimu hii ndogo inamshinda. Mhe. Mwenyekiti, hapa naomba tuheshimiane kama mnapiga kura mimi nitoke nje siwezi kukubali baada ya maisha ya duniani kuna maisha ya kweli kweli huko tunakokwenda. Hii nilisema katika mchango wangu haya mambo yanahusu *separation* inayohusu *divorce* ya wakristo. Hili mimi silikubali mnataka kupiga kura mimi nitoke nje baada ya siasa kuna maisha nje, baada ya uhai kuna mauti, baada ya ujana kuna uzee. Haiwezekani wewe Mwanasheria sio swahaba humu ndani kama huwezi kukosea mnataka kupiga kura nitoke nje. Lakini hoja hii nitaisimamia mpaka dakika ya mwisho, haiwezekani kama yeye asikosee kwani yeye swahaba au Mtume.

Mhe. Mwenyekiti*:* Mhe. Jaku Hashim Ayoub kaa umeshaeleweka, tunaendelea. *(Makofi*)

Sehemu ya Kumi na Tatu

Makosa dhidi ya Madili

Kifungu 107-145 Pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Kumi na Nne

Makosa Yanayohusiana na Ndoa na Mahusiano ya Kifamilia

Kifungu 146

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Machano Othman Said

Utaratibu

Mhe. Machano Othman Said:Mhe. Mwenyekiti, hili ni Baraza la Kutunga Sheria lina taratibu zake. Hivi mtu ukisusa halafu unarudi tena ndani hivi hivi nafikiri sio utaratibu nzuri, kiti chako kichukue hatua.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Machano Othman Said sijakuelewa vizuri.

Mhe. Machano Othman Said: Nasemaje Mhe. Mwenyekiti, hapa tunatunga sheria wananchi wanatuona kama tutakuwa tunabishana na kiti halafu useme mimi natoka nje, utoke nje halafu urudi tena sasa tunakwenda vipi Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kanuni gani Mhe. Machano Othman Said inayosema hivyo. Mhe. Mwenyekiti, naomba.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa tuna taratibu zetu lakini jambo ambalo amelifanya Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwa kweli sio zuri na kutoka nje ku-*walk out* yeye mwenyewe kwa imani yake anaona hataki kuona imepitishwa. Lakini ajue kwamba yumo ndani ya Baraza la Wawakilishi.

Kwa hivyo, taratibu zetu tutazifuata vile vile mimi naamini kwamba kuna uongozi wa Baraza pamoja na kamati inayohusika na masuala kama hayo italifanyia kazi suala hili. Tunaendelea. (*Makofi)*

Sehemu ya Kumi na Nne

Makosa Yanayohusiana na Ndoa na Mahusiano ya Kifamilia

Kifungu 146-154 Pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Kumi na Tano

Maudhui na Makosa dhidi ya Afya na Utulivu

Kifungu 155-176 Pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Kumi na Sita

Kuua Bila ya Kukusudia na Kuua Mtoto Mchanga

Kifungu 177-187

Sehemu ya Kumi na Saba

Wajibu Kuhusiana na Hifadhi ya Maisha na Afya

Kifungu 188-192

Sehemu ya Kumi na Nane

Makosa Yanayohusiana na Kuua kwa Kusudia na Kujiuwa

Kifungu 193-201 Pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Kumi na Tisa

Makosa ya Kuhatarisha Maisha au Afya

Kifungu 202-215 Pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Ishirini

Makosa Yanayohusiana na Shughuli za Makundi

ya Kijamii

Kifungu 216-218 Pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Ishirini na Moja

Jinai kwa Kutojali na Kupuuza

Kifunga 219-228 Pamoja na marekibisho yake

Sehemu ya Ishirini na Mbili

Mashambulio

Kifungu 229-232 Pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Ishirini na Tatu

Makosa dhidi ya Uhuru wa Mtu

Kifungu 233-249 Pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Ishirini na Nne

Wizi

Kifungu 250-269 Pamoja na marekebisho yake.

Sehemu ya Ishirini na Tano

Makosa Yanayofanana na Wizi

Kifungu 270-278 Pamoja na marekebisho yake.

Sehemu ya Ishirini na Sita

Unyang'anyi na Kupora kwa Nguvu

Kifungu cha 279-289

Sehemu ya Ishirini na Saba

Uvunjaji wa Nyumba Usiku, Uvunjaji wa Nyumba Mchana na Makosa yanayofanana na hayo

Kifungu cha 290 - 297 Pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Ishirini na Nane

Udanganyifu

Kifungu cha 298 - 308 Pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Ishirini na Tisa

Kupokea Mali Iliyoibwa au Iliyopatikana Isivyo Halali na Makosa Yanayofanana na hayo

Kifungu cha 309 - 313 Pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Thelathini

Udanganyifu wa Wadhamini na Watu walio katika Nafasi za Dhamana na Hesabu za Uongo

Kifungu cha 314 - 318 Pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Thelathini na Moja

Makosa Yanayosababisha Uharibifu wa Mali

Kifungu cha 319 - 332

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia katika kifungu cha 319 juu ya uchomaji wa mali kwa makusudi, nilisema kwamba katika kifungu hiki, kwanza kifungu (c) ambacho kimetaja mrundikano wowote wa mazao ya mboga mboga. Halafu tukitazama na hiyo adhabu iliyowekwa ya kifungo cha maisha, kwa kweli hazina uwiano, kwamba mtu kachoma mrundikano wa mazao ya mboga mboga, halafu adhabu yake ni kifungo cha maisha. Hiyo haina uwiano, ilisema hivyo.

Vile vile katika kifungu cha (b) imesemwa chombo chochote kile kiwe kimekamilika au bado hakijakamilika, maana yake inawezekana hivyo chombo kinatengenezwa.

Kwa mfano, jahazi inatengenezwa pale Kinazini au mtumbwi mtu kenda kuuchoma halafu adhabu yake iwe ni kifungo cha maisha. Nilisema adhabu hiyo haina uwiano. Aidha, adhabu za aina hii za kuchoma zitazame ile thamani ya mali yenyewe, vyenginevyo hapa panahitaji mazingatio sana.

Vile vile tukitazama katika kifungu cha 321, kifungu hiki kimetaja kuchoma moto mazao ya mimea, kwa nini huu mrundikano wa mazao ya mboga mboga usije katika kifungu hiki cha 321. Mhe. Mwenyekiti, nafikiri umenifahamu nahitaji mazingatio kwa Mwanasheria Mkuu juu ya hili, tusije tukarudi tena, hii adhabu ni kubwa hakijakaa vyema hiki kifungu, ahsante.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, ukisoma kifungu cha 319 *of course* hii adhabu ambayo imewekwa, imewekwa kwa

vifungu vyote ambavyo vyenye (a), (b), (c) na (d), kama yeyote ambaye atafanya mambo haya basi adhabu yake itakuwa ni hii ambayo imetajwa. *Of course* hii adhabu ilitakiwa ije chini ili isomeke kama adhabu, hii itakuwa ni katika vifungu vyote hivyo ambavyo vimetajwa.

Lakini hoja ambayo anaizungumzia Mhe. Mjumbe kwenye kifungu cha (c) anasema mrundikano wowote wa mazao ya mboga mboga, madini au mafuta ya matunda. Kwa hivyo, kuna vitu vitatu ambavyo vimezungumzwa ndani ya hoja hii, lakini yeye amezungumzia hoja ya mboga mboga tu, akaona kwa adhabu hii ya mboga mboga mbona tumekwenda *extreme* na kuweka adhabu ya kifungo cha maisha.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani tunaweza kutenganisha hii adhabu ambayo iko hapa na kuwacha zile nyengine kuwa ni adhabu za kifungo cha maisha, hii nyengine kuiwekea utaratibu ambayo adhabu yake sasa labda itakuwa kifungo kisichopungua miaka 30 kwa sababu hili nalo ni kosa kubwa na ambalo linaweza pia likatia ukame katika nchi. Kwa hivyo, tunaweza hii peke yake ya matunda tukaiwekea adhabu ya kifungo kisichopungua miaka 30 na kuwa sio miongoni mwa adhabu ambayo itakuwa ya maisha.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa kuweza kuliona hilo na kama alivyopendekeza na mimi nakubaliana na yeye suala la mboga mboga liondoke lije katika 321 ambapo adhabu yake ni miaka 14. Lakini yaliyobaki tuendelee hivyo hivyo. Kwa kweli adhabu yake ni kubwa kwa sababu wengine wana vyombo vya mitumbwi hapa, sasa tulione hili ili tusije tukarejesha hii sheria mara kwa mara. Ahsante sana tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu cha 319 - 332 Pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Thelathini na Mbili

Kughushi Utengenezaji wa Sarafu, Utengenezaji wa Fedha Bandia na Makosa yanayofanana na hayo

Kifungu cha 333 - 353 Pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Thelathini na Tatu

Makosa Yanayohusiana na Sarafu na Noti

Kifungu cha 354 - 365

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, wakati na mimi nikichangia kwa maandishi nilimwandikia mheshimiwa kuhusiana na umuhimu wa sheria hii hasa kwa jamii na kutaka kauli yake kwamba, pale ambapo katika jamii yetu au sheria hii katika utekelezaji wake, kunatokea changamoto ambazo ni za msingi kwa ajili ya wananchi ambazo zinawakuta kila siku, basi Mhe. Waziri asisite kurudi nayo sheria hii ili tukaifanyia marekebisho. Sasa sikupata hiyo kauli yake, kwa hivyo naomba niisikie. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nakiri kaniletea mchango wake kwa maandishi. Lakini hilo suala analolieleza alilileta kwa ufupi sana kiasi ambacho mimi nilishindwa hata kutoa ufafanuzi, halafu kaniletea dakika ya mwisho kabisa tunataka tufanye majumuisho. Sasa masuala yetu haya wakati ule tunapotoa ufafanuzi na wao wanakuwa hawapo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nikiri kwamba aliniambia kweli lakini kwa utaratibu ambao kidogo haukuwa utaratibu wa kisheria wa

humu ndani kikanuni. Alinileta *very local* kwamba na yeye kachangia tu, kwa sababu huwezi kutuletea jina lako ukasema na mimi nachangia, lakini angalia mambo ya sheria. Hakuleta hoja kwamba tuijadili au tuitafutie ufafanuzi.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Simai Mohamed umemfahamu Mhe. Waziri.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu alipotumia neno *local*, sasa sijui alitarajia mimi, kwa sababu sina kompyuta ya ku-*type* hapa na kumpelekea na tunatumia kalamu, natakiwa nipeleke mchango wangu kwa maandishi. Sasa labda Mhe. Waziri atueleze sijui kama kuna mfumo mwingine wa kupeleka maoni au mchango kwake yeye tupate kuuelewa. Mimi najua mchango wowote unaopeleka, unapeleka kwa maandishi kwa kutumia kalamu, ahsante. Lakini Mhe. Mwenyekiti, naomba tuendelee.

Sehemu ya Thelathini na Tatu

Makosa Yanayohusiana na Sarafu na Noti

Kifungu cha 354 - 365

Sehemu ya Thelathini na Nne

Stempu Bandia

Kifungu cha 366 - 367

Sehemu ya Thelathini na Tano

Makosa yanayohusiana na Kompyuta

Kifungu cha 368 - 378 Pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Thelathini na Sita

Kughushi Alama za Biashara

Kifungu cha 379 - 380 Pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Thelathini na Saba

Kujifanya Mtu Mwengine

Kifungu cha 381 - 386

Sehemu ya Thelathini na Nane

Kujaribu

Kifungu cha 387 - 391 Pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Thelathini na Tisa

Kula Njama

Kifungu cha 392 - 393 Pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Arubaini

Washirika wa Uhalifu Baada ya Kutendeka Kosa

Kifungu cha 394 - 397 Pamoja na marekebisho yake

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, ilivyokuwa Kamati ya Kutunga Sheria imeupitia mswada wangu kifungu kwa kifungu na marekebisho yake. Sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, Mhe. Waziri ameshatoa hoja. Sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja hiyo wanyooshe mkono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Adhabu wa Mwaka 2018

(Kusomwa kwa mara ya tatu)

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja kuwa Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Adhabu na Kutunga Sheria Mpya ya Adhabu, Kuweka Masharti Bora Zaidi pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo kusomwa kwa mara ya tatu. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

(Mswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa mara ya tatu na kupitishwa)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, niwashukuru sana kwa michango yenu pamoja na utulivu wenu wakati tunapitisha vifungu pamoja na mashirikiano makubwa ambayo mmeonesha katika kuhakikisha sheria hii tumeipitisha. Sasa nichukue fursa hii kumkaribisha Mhe. Mwenyekiti wa Baraza bi Mwanaasha Khamis Juma aweze kuendelea tena na sheria nyengine ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora ataisoma. Tukiwahi atakuja pamoja na Mwenyekiti vile vile. Kwa hivyo, Mhe. Mwanaasha karibu.

(Hapa Mhe. Mwenyekiti alikalia kiti)

Muongozo

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, nilitaka kufahamu tu, nilitaka muongozo wako. Baada ya kutekeleza kazi zetu za kila siku, mfumo ambao tuliokuwa tukiufahamu wa kihistoria ambao tangu tumekuja wa kupeleka maoni yetu kwa viongozi au kwa mawaziri wakati ni wa kimaandishi. Lakini nataka nifahamu tu kama kuna utaratibu umebadilika kwa sababu nimepata mshtuko Mhe. Waziri aliposema kwamba nilipompelekea maandishi ya kwenye karatasi alisema ni *very local.*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe.

Mhe. Simai Mohamed Said: Naomba nimalizie Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Kabla hujamaliza. Nilikuwa nataka kujua muongozo wako ulioutaka ni kuhusiana na kitu gani au kanuni gani iliyovunjwa ya hili Baraza. *(Makofi)*

Mhe. Simai Mohamed Said: Mhe. Mwenyekiti, muongozo wa Spika, kwa utaratibu sidhani kama una kanuni.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Simai Mohamed Said kuhusu muongozo wako ulioulizа na mimi ndio nilitaka nijue ni kwa kanuni gani iliyovunjwa hukusema. Lakini nikupe tu taarifa kuwa unapotoa katika kanuni yetu hii, utakapotoa mchango wako wa maandishi unatoa *copy* unaupeleka kwa Katibu, moja inaletwa kwa Spika na *copy* nyengine atakuwa nayo Waziri. Naomba tuendelee Katibu. *(Makofi)*

Mswada wa Sheria ya Mwenendo wa Jinai ya mwaka 2018

(Kusomwa kwa mara ya pili)

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha pendekezo la kufuta Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai Nam. 7 ya Mwaka 2004 na Kutunga Sheria Mpya ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai ya Mwaka 2018 kwa lengo la kuondosha kasoro zilizojitokeza katika sheria hiyo. Kuingiza vifungu vipya vinavyohusiana na utaratibu wa makosa ya jinai ambavyo vilikosekana katika sheria ya awali ili kuifanya sheria hiyo iendane na wakati.

Mhe. Mwenyekiti, Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai ndio sheria kuu inayosimamia utaratibu mzima wa utawala wa sheria kwa makosa ya jinai hapa Zanzibar. Sheria hii kama zilivyo sheria nyingi za Zanzibar ilipokelewa kutoka nchini India na kuanza kutumika Zanzibar mnamo mwaka 1934, kabla ya kufanya mapitio mwaka 2004 ilijulikana kama *Criminal Procedure Decree*, c*hapter* 14.

Mhe. Mwenyekiti, sheria hii ilitumika katika uchunguzi wa uhalifu, kutambua watuhumiwa wa uhalifu na ukusanyaji wa ushahidi, utambuzi wa mtuhumiwa mwenye hatia au aliye na hatia na pia kutoa maamuzi ya adhabu kulingana na makosa husika.

Mhe. Mwenyekiti, sheria hii ilifanyiwa mapitio makubwa mwaka 2004, lakini mapitio hayo hayakuweza kuondosha kasoro zote zilizokuwemo na hivyo kupelekea kutokukidhi haja ya watumiaji, kwa vile bado ilibaki kuwa na vifungu vingi vya zamani visivyoendana na kasi ya kuibuka kwa makosa ya kijinai yanayochangiwa sana na maendeleo ya sayansi na teknolojia.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuzingatia upungufu huo wizara imeona kuna haja ya kufutwa na kutungwa upya sheria hii kuondoa upungufu uliokuwepo na hatimae kuwa na sheria inayokidhi mazingira ya sasa na kutatua changamoto zinazojitokeza katika usimamizi wa haki jinai.

Mhe. Mwenyekiti, kama tulivyoelewa, jamii yetu imekuwa ikishuhudia kuongezeka kwa matendo ya uhalifu ikiwemo udhalilishaji wa wanawake, watoto na watu wenye mahitaji maalum. Miongoni mwa sababu zinazotajwa kuchangia kwa makosa haya ni pamoja na sheria ya sasa kuruhusu dhamana na kutoa adhabu ndogo kwa wahusika wanaotiwa hatiani na mahakama kwa makosa hayo. Hivyo, sheria hii inayopendekezwa inalenga kutatua tatizo hilo kwa kuyaorodhesha makosa hayo kuwa ni miongoni mwa makosa yasiyo na dhamana. Aidha, kuwepo kwa sheria mpya ya ushahidi Nam. 9 ya mwaka 2016, inayotambua ushahidi wa kielektroniki kumepelekea pia baadhi ya sheria kufanyiwa mabadiliko ili ziendane na sheria hiyo hususan katika masuala yanayohusiana na ukusanyaji wa ushahidi. Miongoni mwa sheria hizo ni Sheria ya Makosa ya Jinai Nam. 7 ya mwaka 2004.

Mhe. Mwenyekiti, mapendekezo haya ya kufutwa na kutungwa upya kwa Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai ni sehemu ya utekelezaji wa program ya mageuzi katika Sekta ya Sheria kama ilivyobainishwa kwenye Mkakati wa Tatu wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Zanzibar (MKUZA III). Pia ni utekelezaji wa kifungu cha 7.0 cha Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2020 kuhusu Zanzibar kuimarisha utawala bora na utawala wa sheria.

Mhe. Mwenyekiti, mapendekezo ya sheria hii inatarajiwa kuleta faida tofauti zikiwemo:

1. Faida ya kuanza kuwepo kwa sheria ambayo taratibu zake ni rahisi kufahamika na kutekelezeka.

2. Kurahisishwa utekelezaji wa sheria ya ushahidi Nam. 9 ya mwaka 2016.

3. Kuzingatia baadhi ya haki za msingi za watuhumiwa na makosa ya jinai. Mfano, kukaguliwa na kuchukuliwa maelezo kwa mtuhumiwa mwanamke kufanywa na askari wa kike.

4. Kuweka mpangilio mzuri wa vifungu vya sheria nzima na kuzingatia kanuni za uandishi wa kisasa ili kurahisisha matumizi yake.

5. Kuondoshwa vifungu vilivyopitwa na wakati.

6. Kufanya sheria iendane na wakati.

Mhe. Mwenyekiti, sheria mpya inahusisha mapendekezo mbali mbali, baadhi ya mapendekezo hayo ni kama haya yafuatayo:

1. Jina la sheria kuwa ni Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai ya Mwaka 2018.

2. Kuondosha maneno yaliyopitwa na wakati na yenye maneno ya kikoloni.

3. Kuandika sheria katika lugha nyepesi ya kisheria na uandishi wa kisasa.

4. Maneno mbali mbali yamepewa tafsiri ikiwemo makosa yenye dhamana, makosa yasiyo na dhamana, lalamiko, usaili, mapatano na mtaalam wa afya, kutofautisha dhana ya makosa yenye dhamana na makosa yasiyo na dhamana.

5. Sheria kuandikwa sambamba na sheria nyenginezo zinazotumika pamoja katika utendaji. Mfano, utaratibu wa kuwasaili watoto katika sheria hii huenda kwenda sambamba na vifungu vilivyomo katika Sheria ya Mtoto Nam. 6 ya mwaka 2011.

6. Kuruhusu matumizi ya kumbukumbu ya kieletroniki katika sheria hii.

7. Kuwatambua Masheha katika ufikishaji wa wito wa Mahakama.

8. Kuiruhusu Mahakama kuweka mazingira maalum kwa mashahidi kwa makundi maalum na waathirika wa vitendo vya udhalilishaji.

9. Kuweka utaratibu wa Wazee wa Baraza *(Assessors)* kula kiapo mbele ya Jaji wa Mahakama Kuu

na kutumika katika kesi ambazo adhabu zake ni kifo au kifungo cha maisha.

10. Kuondoa marejeo ya vifungu vya sheria zilizofutwa mfano *Approved School Decree cap. 9* iliyofutwa na Sheria ya Mtoto Nam. 6 ya mwaka 2011.

11. Kuruhusu Mahakama kurekodi mwenendo wa kesi kwa kupitia mfumo wa kisasa wa kielektroniki.

12. Kufutwa Sheria ya sasa ya Mwenendo wa Jinai Nam. 7 ya Mwaka 2004.

Mhe. Mwenyekiti, Rasimu ya Sheria inayopendekezwa ina sehemu kumi na nane na jadweli saba.

Muundo wa sheria ni kama ifuatavyo:

Sehemu ya Kwanza: Masharti ya awali yanayojumuisha jina fupi la sheria kuanza kutumika na tafsiri ya maneno yaliyotumika katika mswada huo.

Sehemu ya Pili: Inahusu masharti yanayohusiana na uwezo wa Mahakama na mamlaka ya Mahakama hizo katika kutoa adhabu kama vile kifungo, faini na kuitumikia jamii.

Sehemu ya Tatu: Inahusu masharti ya jumla yanayohusiana na ukamataji, utorokaji na ukamataji tena. Sehemu hii inaeleza baadhi ya hatua kama vile ukamataji unaofanywa, ushughulikiaji wa mtu anayekamatwa, upekuzi wa mtu aliyekamatwa, ukamataji kwa hati au bila hati, ukamataji unaofanywa na mtu binafsi, kumuhoji mtu aliekamatwa, kurikodi mahojiano, uchukuaji wa maelezo ya mtuhumiwa, gwaride la utambuzi na uchunguzi wa kitabibu wa muathirika wa jinai wa mshtakiwa unaofanywa na daktari.

Sehemu ya Nne: Inahusu kuzuia utendaji wa makosa kwa njia ya kumtaka mtuhumiwa aweke dhamana ya kutunza amani na kuwa na tabia njema.

Sehemu ya Tano: Imeidhinisha masharti yanayohusu upelelezi wote wa jinai kama vile mahala pa uchunguzi na usikilizaji wa kesi na uhaulishaji wa kesi. Sehemu hii pia inaeleza masharti kuhusu udhibiti wa Mkurugenzi wa Mashtaka katika mwenendo wa jinai na uendeshaji wa mashtaka.

Sehemu ya Sita: Inahusu utaratibu wa ufunguaji wa mashtaka.

Sehemu ya Saba: Inahusu utaratibu wa kulazimisha mshtakiwa ahudhurie Mahakamani kwa njia ya wito au hati ya ukamataji. Sehemu hii pia inaelezea masharti mbali mbali kuhusu hati za upekuzi, dhamana, hati ya mashtaka na taarifa ya mashtaka. Kanuni za uandaaji wa hati ya mashtaka na uandaaji wa taarifa za mashtaka, pia inaelezea mambo yanayohusiana na kulazimisha mashahidi wahudhurie, kuwahoji mashahidi na kuagiza uchukuaji wa maelezo ya mashahidi.

Sehemu ya Nane: Imeweka masharti kuhusu namna ya kuchukua na kurikodi ushahidi katika uchunguzi wa usikilizaji wa kesi katika Mahakama za chini na Mahakama Kuu.

Sehemu ya Tisa: Inaelezea utaratibu wa usikilizaji wa kesi mbele ya Mahakama za chini hususan kuhusu usikilizaji wa kutoa uamuzi wa kesi za ukomo na dharura zinazohusiana na usikilizaji wa kesi mbele ya Mahakama za chini.

Sehemu ya Kumi: Ina masharti yanayohusu utaratibu wa usikilizaji wa kesi mbele ya Mahakama Kuu kama vile namna ya usikilizaji kesi, utayarishaji wa orodha ya Washauri wa Mahakama, uteuzi wa Washauri wa Mahakama, mahudhurio ya

Washauri wa Mahakama, usomwaji wa shitaka, usikilizaji wa kesi na utoaji wa adhabu.

Sehemu ya Kumi na Moja: Inahusu hatia na hukumu.

Sehemu ya Kumi na Mbili: Nimeweka wazi masharti ya adhabu na utekelezaji wake.

Sehemu ya Kumi na Tatu: Inahusu urudishaji wa mali iliyoibiwa hususan mali waliyokutwa nayo washtakiwa na urudishaji wa mali iliyoibiwa.

Sehemu ya Kumi na Nne: Ina masharti ya msingi kuhusu rufaa, mapitio na upelekaji wa kesi Mahakama Kuu.

Sehemu ya Kumi na Tano: Imeweka masharti kuhusu upelelezi wa vifo vya ghafla na uchunguzi wa vifo hivyo, sehemu hii imeweka wajibu wa mtu kutoa taarifa za kosa au ajali au kifo katika mazingira fulani, pia sehemu hii inaelezea kuhusu upelelezi juu ya kifo cha ghafla na uchunguzi.

Sehemu ya Kumi na Sita: Inahusu maelekezo ya Mahakama Kuu na amri nyengine za kipekee za Mahakama Kuu.

Sehemu ya Kumi na Saba: Inahusu mienendo ya kesi yenye kasoro kama vile mienendo iliyosikilizwa mahala ambapo sio sahihi, kukubaliwa ushahidi kimakosa au kukataliwa ushahidi kimakosa, kuacha kuapa na kuacha jambo au kukwepa makosa katika mienendo ya kesi.

Sehemu ya Kumi na Nane: Inaeleza masharti mengineyo yahayohusu mambo ya kumbukumbu ya kielektroniki, fomu zilizotumika, uwezo wa Jaji Mkuu kutunga kanuni, kufutwa kwa

Sheria ya Mwenendo wa Jinai Nam. 7 ya Mwaka 2004 na masharti yake.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, nachukua fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu waijadili rasimu hii ya sheria kwa kina huku wakizingatia sheria ya sasa haiendani na wakati na kusababisha matatizo katika jamii. Aidha, kilio kikubwa cha kupewa dhamana watuhumiwa wa makosa ya udhalilishaji hususan makosa ya kubaka yanatokana na mapungufu ya sheria hiyo ya sasa. Hivyo, kupitishwa kwa sheria hii mpya ya mwenendo wa makosa ya jinai kutasaidia kupambana na matatizo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa na imeungwa mkono. Sasa naomba nimwite Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum.

Mhe. Machano Othman Said (Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum): Mhe. Mwenyekiti, ifuatayo ni hotuba ya maoni ya Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum kuhusu Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Mwenendo wa Jinai Nam. 7 ya Mwaka 2004 na kuweka Utaratibu Bora wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai na Uendeshaji wa Kesi za Jinai na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehma kwa kutujaalia uhai na afya njema. Namuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu azidi kutubariki pamoja na kutupa neema zake ambazo kwa hakika sote ni wategemezi wa mahitaji yake.

Mhe. Mwenyekiti, pia natoa shukrani zangu za dhati kwako wewe binafsi pamoja na waendeshaji wote wa Baraza hili, wakiwemo Mhe. Spika, Naibu Spika na Mwenyekiti wa Baraza hili tukufu kwa namna mnavyoendesha kwa ushirikiano katika kuliongoza Baraza kwa umakini na umahiri mkubwa. Tunamuomba Mwenyezi Mungu akuzidishieni hekima na busara katika kutekeleza majukumu yenu ya kutuongoza ili tuweze kutekeleza vyema majukumu yetu katika chombo hiki muhimu kwa nchi yetu.

Aidha, kamati yangu inatoa pongezi za dhati kwa Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kuwasilisha mswada huu Barazani.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile natanguliza shukrani zangu kwa dhati kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushirikiano mkubwa waliouonesha pamoja na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mwendesha Mashtaka Mkuu *(DPP)* kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kutayarisha Mswada huu wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Mwenendo wa Jinai na Kuweka utaratibu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai na Usikilizaji wa Kesi za Jinai na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo ambayo utakapopitishwa kuwa sheria utarahisisha utekelezaji wake kuwa wenye kuleta ufanisi katika uendeshaji wa kesi za jinai.

Mhe. Mwenyekiti, madhumuni ya mswada huu ni kuweka utaratibu utakaofuata katika upelelezi wa makosa ya jinai na uendeshaji wa usikilizaji wa kesi za jinai na mambo mengine yanayohusiana na hayo na kufuta sheria ya mwenendo wa jinai namba 7 ya 2004.

Mhe. Mwenyekiti, mswada huu pia unaweka masharti yanayokwenda na wakati uliopo kuhusu utaratibu wa jinai unaondosha masharti yaliyofutwa na sheria nyingine pia

umetumia aina mpya ya uandishi wa sheria. Vile vile mswada huu unaainisha masharti ya sheria hii na masharti ya sheria mpya ya adhabu na unakusudia kuleta ufanisi katika usimamizi wa haki zinazohusiana na jinai ndani ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, pia napenda nitumie fursa hii kuwashukuru wadau mbali mbali ambao kamati yetu ilikutana nao na kutoa mashirikiano yao makubwa ambayo yalitupatia na kuweza kutoa maoni yao kwa lengo la kuboresha mswada huu. Kamati inachukua fursa hii kuwaomba wasichoke kutoa maoni yao pale ambapo tunawahitaji kwani sote tuna lengo la kuitetea jamii na kuikinga kuingia katika makosa ya kijinai ambayo hayakubaliki katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Sheria ya Utawala Bora na Idara Maalum, imeupitia mswada ukurasa kwa ukurasa toka mwanzo hadi mwisho na kuelewa zana nzima na mantiki ya mswada huu, ambapo marekebisho mbali mbali yamependekezwa kufanywa na kamati kwa kuzingatia umuhimu wa sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kubwa sasa naomba uwatambue wajumbe wa kamati hii ya sheria kama ifuatavyo:

1.	Mhe.Machano Othman Said	Mwenyekiti
2.	Mhe.Mwantatu Mbaraka Khamis	Makamu Mwenyekiti
3.	Mhe.Nadir Abdul-latif Yussuf	Mjumbe
4.	Mhe.Wanu Hafidh Ameir	Mjumbe
5.	Mhe.SaadaRamadhan Mwendwa	Mjumbe
6.	Mhe. Ali Khamis Bakari	Mjumbe
7.	Mhe. Suleiman Makame Ali	Mjumbe
8.	Nd. Ali Alawy Ali	Katibu, na
9.	Nd. Haji Jecha Salim	Katibu

Mhe. Mwenyekiti, naomba sasa uniruhusu nieleze baadhi ya marekebisho na mapendekezo mbali mbali ambayo kamati yetu imeyafanya na pia, naomba kuwatanabahisha Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu ya kwamba, hotuba hii inatoa ufafanuzi tu wa baadhi ya vifungu ambavyo vimependekezwa na kufanyiwa marekebisho na kamati. Hivyo, maelezo ya ziadi ya mapendekezo hayo yamo katika muhtasari wa marekebisho ambayo tayari Waheshimiwa Wajumbe mmeshapatiwa.

Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu cha 7 cha mswada huu kamati inapendekeza kurekebishwa kwa kufuta na kuandikwa upya maneno ya pembeni kama ifuatavyo:

“Adhabu ambazo Hakimu wa Mahakama ya Mkoa anaweza kutoa”.

Aidha, kamati inatoa mapendekezo hayo kutokana na lengo la kifungu hiki katika kuweka mipaka ya jukumu la kutoa adhabu kwa Hakimu wa Mahakama ya Mkoa.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile, kamati inapendekeza katika kifungu cha 29 kurekebishwa kwa kuweka maneno pembeni ambayo yamekosekana katika kifungu hiki. Hivyo, itaweza kusomeka kama ifuatavyo:

“Kuwashughulikia watu waliokamatwa na Afisa Polisi”.

Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu cha 34(2) kamati inashauri kufutwa na kuandikwa upya ili kwenda sambamba na dhana iliyokusudiwa katika mazingira ya kifungu hiki. Hivyo, baada ya marekebisho hayo kifungu hiki kitasomeka kama ifuatavyo:

“(2) Afisa wa polisi atamjulisha mtu aliyekamatwa kwamba ana haki ya kukaa kimya lakini iwapo ataamua kuzungumza, basi

chochote atakachokisema kinaweza kutumiwa dhidi yake Mahakamani".

Aidha, kwa mantiki ya kifungu hiki ni kwamba mtu ambaye amekamatwa kwa kosa lolote la jinai, anayo haki ya kukaa kimya bila ya kuongea chochote kutokana na sababu mbali mbali, lakini mtu huyo akiamua kuzungumza chochote mazungumzo hayo yatachukuliwa kama ushahidi wa kosa alilolitenda na utaweza kutumika Mahakamani.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inapendekeza katika kifungu cha 196 (4) kurekebishwa kwa kufuta maneno "Mrajis wa Mahakama Kuu" na badala yake kuweka maneno "Katibu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar" baina ya neno "kwa" na "kuhusu". Kamati inatoa ushauri huo kwa sababu Katibu Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ndiye mwenye dhamana ya watendaji wote wa Serikali. Hivyo, kwa umuhimu wa suala hili katika kutafuta haki ya jinai katika nchi basi ni vyema dhamira hii pia ikawa ni miongoni mwa majukumu yake.

Mhe. Mwenyekiti, aidha, kamati imeridhishwa na utaratibu unaoweka masharti kuhusiana na namna ya kuchukua ama kurikodi ushahidi katika uchunguzi na usikilizaji wa kesi katika Mahakama za chini kuwa sawa sawa na Mahakama Kuu. Hivyo, katika kifungu cha 205 Kamati inapendekeza kurekebishwa katika maneno ya pembeni, kwa kuongeza maneno "katika Mahakama Kuu" baada ya neno "ushahidi" ili kutoa maana iliyokusudiwa katika kifungu hicho.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile, katika masharti yanayohusu utaratibu wa usikilizaji wa kesi mbele ya Mahakama Kuu imefafanuliwa vizuri katika sehemu ya kumi ambapo Kamati imeridhishwa na maelezo yake. Hata hivyo, imeonekana kuwa kupitia kifungu cha 248 kuwepo kwa utata katika maana ya kifungu hiki. Aidha,

Kamati inashauri kurekebishwa kwa maneno ya pembeni ya kifungu cha 248, kwa kufuta neno “kukubali” na badala yake kuweka neno “kutokukubali” baina ya neno “ya” na “kosa” ili kuleta maana iliyokusudiwa katika kifungu hiki.

Hitimisho

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum inatoa shukrani zake za dhati kwa wahusika wote walioshiriki kuandaa mswada huu ambao ni muhimu na wenye maudhui mazito katika utekelezaji na usimamizi wa haki za jinai katika nchi yetu. Pia, kwa vile mswada huu ni muhimu sana katika uimarishaji wa utoaji haki kwa wananchi wa Zanzibar ni vyema, Wajumbe wako wa Baraza hili tukufu kuwa makini sana katika kuuchangia mswada huu. Vile vile mara tu baada ya kusainiwa kwa sheria hii ni vyema Serikali na Wajumbe wa Baraza hili kutoa elimu ya kutosha kwa wananchi ili waweze kuifahamu sheria hii ambayo ndio msingi mkuu wa mwenendo wa makosa ya jinai.

Mhe. Mwenyekiti, ni imani yangu kuwa Wajumbe wa Baraza hili Tukufu wamepata fursa ya kuupitia kwa kina Mswada huu, na kubaini maeneo kadhaa ya kuishauri Serikali kuhusu utekelezaji bora wa Sheria inayotarajiwa kutungwa amabayo itatoa fursa kwa kila mmoja miongoni mwetu na kupunguza ongezeko la makosa ya jinai katika mazingira ya nchi yetu, lakini pia na kuwadhibiti watoto wetu kutokana na matendo maovu wanayofanyika.

Mhe. Mwenyekiti, hivyo, ni matumaini ya kamati kwamba, Wajumbe wa Baraza hili tukufu, watauchangia, wataujadili ipasavyo na hatimae kuupitisha mswada huu na kuwa sheria ikiwa ni sehemu ya jukumu la Baraza, na hatimae kuipa fursa serikali kutekeleza sehemu ya jukumu lake la utekelezaji.

Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati yangu naomba kuchukua nafasi hii kuwashukuru sana wafanyakazi wa Kitengo cha Sheria cha Baraza la Wawakilishi kwa jinsi walivyoisaidia kamati yetu wakati wa kujadili mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, aidha, nachukua fursa hii kuwashukuru kwa dhati kabisa Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa umakini wao na usikivu wa hali ya juu waliouonesha wakati wa uwasilishaji wa hotuba hii. Kamati inawaomba waujadili kwa kina na hatimae kuupitisha kwa ajili ya kuwekewa misingi iliyo bora katika utekelezaji wake ndani ya jamii ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum. Waheshimiwa Wajumbe majadiliano yanaendelea na mpaka sasa nina jina la Mheshimiwa Ali Suleiman Ali.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuchangia Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Mwenendo wa Jinai Nam. 7 ya Mwaka 2004 na Kutunga Sheria Mpya ya Mwenendo wa Jinai na Kuweka Utaratibu Bora wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai na Usikilizaji wa Kesi za Jinai na Mambo Mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikupongeze kwa kunipa mtu wa kwanza baada ya kumaliza Mhe. Waziri na Mwenyekiti na mimi nikawa mtu ambaye nitaanza katika shughuli hii kuchangia mambo mbali mbali lakini kwa ufupi kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, nampongeza sana Mhe. Waziri, nampongeza Mhe. Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Mkurugenzi wa Mashtaka,

Mwanasheria Mkuu na wenzake wote kwa kuhakikisha kwamba umefika wakati wa kuweka sheria ambayo inakwenda na wakati unaofaa. Mhe. Mwenyekiti, mswada huu una mambo mengi lakini kubwa tunalozingatia kwamba una mambo ambayo yanafaa kuangaliwa kwa wakati tuliokuwa nao hivi sasa. Mimi nafikiri nitakuwa na vipengele vifupi vya adhabu kama ifuatavyo kutokana na makosa mbali mbali yaliyokuwemo ambayo Mahakama ya Hakimu wa Mkoa inaweza kutoa.

Mhe. Mwenyekiti, sehemu ya pili inazungumzia Uwezo wa Mahakama. Mara nyingi tumelalamika katika Baraza hili lakini pia wananchi wetu nje wanatutegemea sana kwa sababu sisi ndio tunaohusika na kuweka sheria hizi kwa ajili ya manufaa ya wananchi wetu kwa mambo mbali mbali ambayo yanawagusa. Tukubali tu kwamba adhabu nyingi zilikuwa zinapangwa huko nyuma lakini zilikuwa haziendani na wakati kwa sababu unakuta adhabu mfano sheria nyengine zimetungwa tokea mwaka 1917 zilizohusiana katika kurekebisha mambo haya, lakini bahati nzuri sasa hivi zimekuja katika mwaka 2018 zinafaa kuwekwa vizuri na kuhakikisha kwamba tunakwenda na wakati unaofaa.

Mhe. Mwenyekiti, katika sehemu ya pili kifungu cha 7 ukurasa wa 235 naomba ninukuu kama ilivyo. Mhe. Mwenyekiti, Mahakama ya Hakimu wa Mkoa katika kesi ambazo zinaruhusiwa na sheria inaweza kutoa adhabu zifuatazo:

(a) kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka 14;
(b) faini isiyozidi shilingi milioni 14;
(c) kutumikia jamii kwa kipindi kisichozidi miezi 12.

Kwa mujibu wa kanuni zilizotungwa na Jaji Mkuu. Hii Mhe. Mwenyekiti, niseme tu kwamba kidogo kutokana na adhabu ambazo Mahakama ya Mkoa imepewa zinaweza kutusaidia kidogo. Kwa sababu Mkoa ulikuwa umepewa adhabu baadhi ya

adhabu ambazo zimestahiki kwa wakati huo ilikuwa haitozidi miaka saba, lakini sasa hivi tunaanzia miaka 14 na faini isiyozidi shilingi milioni 10 kidogo wamepata uwezo. Lakini namuomba sana Mhe. Waziri, naomba Mahakama zetu zifanye kazi kadri ya uwezo wake pindi yanapotokea makosa ambayo yanastahiki na adhabu hizo yatimizwe hili liwe ni fundisho na kuondoa mambo ambayo hayastahiki katika adhabu mbali mbali zinazotokea.

Lakini kifungu cha 8 adhabu ambazo Hakimu wa Mahakama ya Wilaya anaweza kutoa. Mahakama ya Hakimu Wilaya katika kesi ambazo inaruhusiwa na sheria ni kutoa adhabu kama zifuatazo:

(a) Kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka saba;
(b) Faini isiyozidi shilingi milioni saba;
(c) Kutumikia jamii kwa kipindi kisichozidi miezi sita kwa mujibu wa kanuni zilizotungwa.

Mhe. Mwenyekiti, nasema tu kwamba hizi ni kesi za jinai na katika kesi hizi tulikuwa tunapiga kelele narudia tena kwamba adhabu ndogo, adhabu ndogo, lakini hizi adhabu zake zinastahili kutokana na mambo madogo madogo yanayotokea. Lakini hata hivyo, Mhe. Mwenyekiti, niseme tu kwamba kwenye Mkoa na Wilaya kuna mambo ambayo wakati mwengine hutokea na adhabu hizo tukazipigia kelele kidogo.

Kwa hivyo, nilikuwa naomba tu hapa pia wasiwekewe ndio mwisho itizamwe ule uzito wa kesi yenyewe, au lile tukio lenyewe lilivyotokea, au tatizo lenyewe kwa sababu ukitizama mwisho miaka 14 au miaka 7 lakini mengine hutokea jambo zito zaidi likatutisha katika mazingira yake. Kwa hivyo, ilikuwa iwekwe miaka 14 au vyenginevyo naweza kuendelea mbele zaidi. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, hali ya nchi yetu tunaelewa watu wetu wengi sasa hivi hawajifahamu baadhi yao, kwa hivyo

tukipata watu kama kumi, au ishirini, au watu watano sita, au nane wakipata fundisho la kufaa basi huenda ikapungua.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 9 adhabu ambazo Mahakama ya Mwanzo inaweza kutoa naomba ninukuu. "Mahakama ya mwanzo inaweza katika kesi ambazo adhabu zinaruhusiwa na Sheria ya kutoa adhabu zifuatazo".

1) Kifungo kwa kipindi kisichozidi mwaka mmoja;
2) Faini zisizozidi shilingi milioni moja;
3) Kutumikia jamii kwa kipindi cha miezi miwili kwa mujibu wa kanuni zilizowekwa.

Mhe. Mwenyekiti, Mahakama ya Mwanzo nayo kifungo kilichozidi nasema tu kwamba tuangalie matokeo yenyewe yanavyotokea, matokeo ya Mahakama ya Mkoa naweza kuja huko katika Mahakama ya mwanzo mimi naona kifungu hiki adhabu yake ndogo, adhabu yake ndogo tena ndogo. Kwa mfano Mhe. Mwenyekiti, tulikuwa tunalalamika sisi kesi za udhalilishaji Mahakama ya Wilaya au Mahakama ya Mkoa kapewa miaka si zaidi ya saba. Sasa hii Mheshimiwa siku nyengine kesi itaangukia Mahakama ya Mwanzo ikienda huko adhabu yake inaambiwa kifungo cha mwaka mmoja ni hatari.

Mimi ningeomba tu kwa kuwa huko mwanzo kuna miaka kumi na nne. kuna miaka saba na huyu basi angalau iwekwe miaka minne mawazo yangu au natoa rai, mwaka mmoja inaweza kutokea kesi wakati mwengine kaanzia Mahakama ya Mwanzo na Mahakama ya Mwanzo wameshapewa mpaka anaambiwa mwisho mwaka mmoja tu kidogo hatujafanya haki. Nasema tu Mheshimiwa hizi ni kesi za jinai hatutegemei zitokee lakini Mungu atuepushie zisitokee, lakini zikitokea kila mtu atakuangukia huyu kapelekwa Mahakama ya Mwanzo kapata mwaka mmoja anarudi baada ya miezi minane ilimradi hii kidogo. Mheshimiwa haileti msingi

bora, tuweke msingi kwamba kutoka miaka kumi na nne, miaka saba na hii ndio tunaipokea kama ilivyo, lakini baada ya miaka kumi na nne ije miaka kumi na huyu wa chini yake ndio aje miaka saba. Lakini kwa kuwa imewekwa kama ilivyowekwa basi angalau kutoka miaka saba katika Mahakama ya Wilaya huyu Mahakama ya Mwanzo apate miaka minne.

Mhe. Mwenyekiti, narudia sheria hii hakutungiwa fulani imetungwa kwa mtu yeyote mhalifu. Kwa hivyo, tuziangalie sana yanapotokezea matatizo yetu ili tuhakikishe kwamba wananchi wetu wanakuwa na imani na vyombo vyetu vya Mahakama. Mimi sisemi kwa ubaya lakini nasema hali halisi ilivyo wenzetu Mahakama wana kazi nyingi na mara nyingi wanapata shida kutokana na mazingara yanayojitokeza. Kwa hivyo, mimi wito wangu Mhe. Mwenyekiti, niombe sana mswada huu tunaouchangia na tuaoupitisha kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu lakini taaluma iwepo. Wananchi ndio wanaopata shida baada ya kutokea tokeo fulani kwa hivyo taaluma wapewe, elimu ya kutosha wapatiwe ili tuhakikishe kwamba linapotokea kosa ushahidi unapatikana na kuondoa usumbufu wa nenda rudi. Mhe. Mwenyekiti, ikiwa kesi zetu zitakwenda kwa mapema zaidi na zitakwenda kwa haraka kama zinavyotakiwa tunahakikisha Mheshimiwa mambo mengi yataondoka katika nchi yetu na itakuwa tunabakiwa na historia katika maisha ya kila siku.

Mhe. Mwenyekiti, kuna mambo mengine katika ukurasa wa 237 sehemu ya tatu naomba ninukuu "Masharti ya jumla kuhusu kukamata, kutoroka na kukamata tena". Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha kumi na mbili (12) kinasema kama ifuatavyo:

Kifungu cha 12:

> "(1) Katika Mahakama Afisa wa Polisi au mtu mwengine anayefanya ukamataji atamshika kikamilifu au

atauzuia mwili wa mtu anayetaka kukamatwa isipokuwa kama atajisalimisha mwenyewe kwa maneno au vitendo.

(2) Ikiwa mtu huyo atakaidi kwa nguvu juhudi za kumkamata au atajaribu kukwepa kukamatwa Afisa huyo wa Polisi au mtu mwengine anaweza kutumia njia zote za lazima kufanikisha ukamataji."

Mhe. Mwenyekiti, nafikiri hili ni suala la msingi kabisa kwa sababu mtu anapofanya kosa hutakiwa aridhie yale makosa yake ili afikishwe pahala panapohusika kwa usalama zaidi, lakini mara nyingi tunashuhudia kwamba mhalifu huwa anafanya mambo yake kwa kuhakikisha kwamba asifike pale panapohusika kwa kutoa ushahidi au kupata maelezo yanayohusika. Kwa hivyo, hapa tumeambiwa tu kwamba polisi au mtu mwengine yeyote kutumia njia zozote. Sasa hizi njia zozote zingefafanuliwa. Kwa sababu njia zozote Mhe. Mwenyekiti, inaweza kuwa ukatumia mabavu ukampiga magumi au ukamfanya nini ndio njia zozote. Ni vyema katika sheria tufafanue kitu ambacho kitatusaidia.

Mhe. Mwenyekiti ningeshauri "au kwa njia yoyote", njia yoyote ni msingi lakini iwe na ufafanuzi unaofaa. Tunasema tu kwamba pamoja na uhalifu lakini nchi yetu na serikali yetu imo katika ulimwengu wa haki za binaadam, haki za binaadam ni jambo la msingi na tunalililia ndio maana tuna Wizara ya Katiba, Sheria, Utawala Bora na Utumishi wa Umma hiyo ni heshima ya nchi yetu. Bahati nzuri Mhe. Mwenyekiti, Wizara hii ni muhimu sana na haki za binaadam ni suala zuri, hata Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi bahati nzuri alipoteuliwa mara baada ya kifo cha Marehemu Dkt. Omar Ali Juma alikuwa wizara yake hii. Kwa hivyo, wizara hii ina historia kubwa. Haki za binaadam ni misingi bora kwa hivyo katika ukamataji Mheshimiwa tusitoe fursa moja kwa moja tu vyovyote itakavyokuwa, tutafute changanuo ambalo litatoa

maelezo mazuri. Tunajua katika kukamata kuna wengine wababe wanaokamatwa, kuna kitu gani lakini tutumie njia nzuri za ustaarabu ambazo zitastahiki mtu yule kupatikana na hatia ambayo inafaa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa jumla niseme tu kwamba suala letu zuri la mswada huu ni kuhakikisha kuweka mambo mazuri kwa walengwa ambao watapatikana na hatia mbali mbali, lakini pia kuwapa nafuu watendaji wetu katika sehemu zao za kazi ili wajifahamu na wajielewe katika shughuli zao wanazofanya kila siku. Naamini kwamba hivi sasa kesi za jinai zipo nyingi na zinatokea kwa wingi, mimi ningeomba sana kwamba wananchi wetu narudia tena wapewe taaluma ya kutosha na waelewe wapi pa kukimbilia pindi linapotokea tatizo linalowahusu.

Mhe. Mwenyekiti, nakuja katika ukurasa wa 312 sehemu ya kumi na moja "Hatia na Hukumu - Kutiwa hatiani kwa makosa ambayo sio yaliyoshtakiwa nayo mshtakiwa". Kifungu cha 275(1) "Kutiwa hatiani kwa makosa ambayo sio yaliyoshtakiwa nayo mshtakiwa iwapo kosa limethibitishwa linajumuishwa na kosa linaloshtakiwa.

Kifungu cha 275(1):

“Pale mtu anashtakiwa kwa kosa linalokusanya maelezo tofauti, mkusanyiko wa baadhi ya maelezo hayo tu yanaweza kutengeneza kosa dogo lililokamilika, na mkusanyiko huo unathibitishwa lakini maelezo yaliyobakia hayakuthibitishwa, anaweza kutiwa hatiani kwa kosa dogo ingawa mtu huyo hakushtakiwa kwa kosa hilo.”

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba sana wanasheria wanajua sheria, hakimu atakuwa anajua sheria, lakini mwananchi ukimzonga hapa haielewi. Ndiyo nikasema pamoja na jitihada hizi lakini taaluma zitolewe kweli kweli kipindi hichi kiwepo maalum cha kusoma

vifungu hivi na kuwaelimisha wananchi wetu wasije kufanya makosa ambayo hawayaelewi.

Kifungu cha 275(2):

> "Pale mtu anashtakiwa kwa kosa na maelezo yanathibitika ambayo yanalishusha kuwa kosa dogo, anaweza kutiwa hatiani kwa kosa dogo ingawa mtu huyo hakushtakiwa kwa kosa hilo."

Mhe. Mwenyekiti, hichi kizungu naomba sana tutulie kweli kweli, Waheshimiwa Wajumbe wenzangu niwaambie hii ni sheria na sheria ina mambo mengi, mimi nilitoa mfano hapa na leo nitautoa tena.

Wakati tunaingia Barazani mwaka 1995 katika Baraza hili nakumbuka katika mwaka 1997 ilitungwa Sheria ya Mali ya Asili kwamba mtu yeyote atakayesafirisha mchanga au maliasili inayohusika bila ya kibali mali hiyo itataifishwa na itakuwa ni mali ya serikali. Bahati nzuri wakati ule ndio kwanza tunaingia katika Baraza hatuelewi nini kinachoendelea. Bahati nzuri Mwakilishi mwenzetu wakati huo Mhe. Ame Mati Wadi wa Matemwe, namtaja ili anisikie na yeye huko lilimtokea janga analo gari lake lilichukua mchanga wakati kibali alikuwa hana. Lilipokamatwa akaambiwa Mheshimiwa gari linataifishwa au ulipe shilingi milioni mbili. Akasema sheria hiyo imepita mwaka gani.

Mhe. Marehemu Mwanasheria wetu Mzee Iddi Pandu Hassan akaenda akamuonesha sheria hii hapa mliitunga nyinyi wenyewe na Mhe. Haji Omar Kheri yumo humu tulikuwa wote. Bahati nzuri Mheshimiwa tumekaa pale papatu papatu kweli ikabidi sheria msumeno alipe fedha ili atoe gari yake na alifanya hivyo. Kwa hivyo, nawaomba Waheshimiwa wenzangu Mhe.

Mwenyekiti, tuangalie sana sheria hizi na tuangalie vifungu kweli kweli. Si vibaya kusema hichi sijakifahamu ili tueleze kwa manufaa ya wananchi wetu. Wananchi wetu wapo nje wanatutegemea sisi kwa hivyo tutakalolipitisha huku tujue kwamba tuna jukumu la kuwalinda na kuwasaidia kwa hali na mali. Bila ya sisi Mheshimiwa watakuwa hawana kinachoendelea kwa kutokujifahamu.

Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 316 Sehemu ya Kumi na Mbili, Adhabu na Utekelezaji wake na aina tofauti za adhabu. Kifungu cha 292 kinasema adhabu zifuatazo zinaweza kutolewa na mahakama. Niruhusu niseme tu kwamba kuna aina nyingi za adhabu nazo ni:

(a) kifo;
(b) kifungo;
(c) kutumikia jamii;
(d) faini;
(e) kutaifisha;
(f) malipo ya gharama;
(g) malipo ya fidia;
(h) kuweka dhamana kwa ajili ya kutunza amani na kuwa na tabia njema, au kufika mahakamani kwa ajili ya hukumu;
(i) uangalizi;
(j) kufuta au kusimamisha leseni ya udereva chini ya Sheria ya Usafiri Barabarani;
(k) kuachiwa kwa masharti chini ya Sheria ya Uangalizi wa Wahalifu;
(l) amri kuhusu skuli zilizoidhinishwa chini ya Sheria ya Watoto;
(m) adhabu nyengine yoyote inayotolewa na Sheria ya Adhabu au sheria nyengine yoyote.

Mhe. Mwenyekiti, hili ni darasa kila tafsiri ina mambo yake. Mimi nataka kuthibitisha mpaka hii leo kuna kutumikia jamii, mimi naelewa lakini kuna wengine hawaelewi nini kutumikia jamii. Chombo cha mahakama ilikuwa ni haki yake kuwaelimisha wananchi wetu. Niseme tu kwamba kutumikia jamii ni moja katika mashtaka aliyoshtakiwa mtu kwa kosa alilolifanya lakini adhabu yake akaambiwa kuwa utatumikia jamii, kasafishe hospitali, wewe katengeneze bustani mahali fulani, kafyagie mahali fulani. Kuna wengine hawaelewi kwa hivyo mimi naona tafsiri hiyo iendelee.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 293 ukurasa huo huo Adhabu ya Kifo:

Kifungu cha 293:

> (1) Endapo mtu yeyote anahukumiwa adhabu ya kifo, adhabu hiyo itaelekeza kwamba mtu huyo atanyongwa shingoni mpaka afe.
>
> (2) Adhabu ya kifo haitotamkwa au kurekodiwa dhidi ya: *Sentence of death shall not be pronounced on or recorded against:"*

Hichi Kiingereza hakifai bwana hapa, tuwekewe lugha ambayo wananchi wetu wanaielewa. Tunakuja katika adhabu hii ya kifo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sipingi adhabu ya kifo, lakini sina imani sana na kifungu hichi. Tokea mwaka 1964 nchi yetu hii yametokea mengi, mpaka wamemuuwa Rais wetu wa kwanza, Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema Mzee Abeid Amani Karume. Tumeumia na nasema tu kama Mwenyezi Mungu angemjaalia angekuwa hai Zanzibar ingekuwa kuliko Ulaya au Dubai na kwengineko, lakini ndiyo Mwenyezi Mungu

alivyomjalia miaka yake minane, historia iliyowekwa Unguja na Pemba ndio hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, niseme tu kwamba mimi nashauri adhabu ya kifo sio mbaya, tukisema kwamba mtu alifanya kosa la ujambazi au kosa gani akauwa na yeye anafaa auliwe lakini kwa hapa kwetu haijatokea. Jambo kubwa lililotokea katika nchi yetu ni kuuliwa Kiongozi wa Nchi. Mimi naomba au nashauri adhabu hii ifutwe.

Watu wengi unakuta Mahakamani wamehukumiwa adhabu ya kifo, tumekwenda kutembea Vyuo vya Mafunzo sehemu mbali mbali unawakuta watu wanakwambia mimi nangojea adhabu ya kifo ana miaka 40 au 30 ni bora tukatafuta ushauri wakaambiwa kifungo cha maisha au mengineyo. Lakini hili neno la adhabu ya kifo na hata dunia sasa hivi inasema kwamba imepitwa na wakati, haifai kwa sababu naweza kusema tu kwamba imani za viongozi wetu, maraisi wetu wote waliotangulia mpaka aliyekuwepo wana imani nzito kusema huyu kafanya hivi ni mnyonge, Mwenyezi Mungu ndiye anayemlipa mtu.

Mhe. Mwenyekiti, hata Mhe. Rais wetu Magufuli katika kutembelea wafungwa alitamka akasema adhabu ya kifo ipo lakini tutakwenda na ushauri mwengine. Hakuipinga ipo, mimi nashauri kwa Zanzibar imefika wakati tuiondoe kabisa ili tuweke masharti mengine mazuri kama kifungo cha maisha kitawasaidia wananchi wetu na adhabu zitakwenda vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo kwa heshima na taadhima nasema tu kwamba mswada huu ni mzuri na nimeupokea na nasema tu kwa kuwa mimi na wananchi wangu wa jimbo langu la Kijitoupele nitawapa taaluma juu ya athari za kesi za jinai zinapotokea wasishiriki katika mambo mabaya wasije kupata hatia.

Baada ya hayo naushukuru mswada huu kwa asilimia mia moja. Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti: Nakushukuru Mhe. Ali Suleiman Ali sasa naomba nimwite Mhe. Simai Mohamed Said na Mhe. Suleiman ajiandae.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nianze kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu na nichukue nafasi hii pia kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na Mwenyekiti wa Kamati kwa kazi nzuri ambayo wameifanya ya kutoa mapendekezo yao ili tuweze kuishauri serikali.

Nikiri tu kwamba mswada huu ni mzito kama ule ambao tuliouzungumza mapema tulioujadili na leo tumeupitisha. Moja katika jambo ambalo litakuwa linawagusa wananchi wetu kila siku ni sheria ambazo tunazozipitisha kama hivi pamoja na hii ya leo, *inshaallah* Mwenyezi Mungu akitujaalia naamini tutapitisha pamoja na masahihisho, marekebisho na mapendekezo yote. Nichukue nafasi hii kuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Tunguu kwa kuniwezesha wao mimi leo kuwepo hapa na niweze kutoa mchango wangu.

Mhe. Mwenyekiti, leo asubuhi nilitoa mchango wangu kwa njia ya maandishi, lakini sasa hivi natoa mchango wangu uliokuwa rasmi wa kuzungumza na ninaamini huu ndio utakuwa mchango ambao unaozungumziwa na labda Mhe. Waziri anaupenda zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitakwenda kwenye kifungu cha 42 juu ya Kumbukumbu za Mahojiano. Kifungu hiki kinasema:

Kifungu cha 42(1):

"Afisa yeyote wa polisi ambaye anamuhoji mtu kwa madhumuni ya kujua kama mtu huyo ametenda kosa atawezesha mahojiano hayo kurekodiwa".

Mhe. Mwenyekiti, suala la Uhamiaji, Polisi ni jambo la Muungano, sasa tunapozungumzia kuweka rekodi na kumbukumbu panahitajika pia kuwepo kwa nyenzo na vitendea kazi. Tunasimamia sheria hii kwa kushirikiana pia na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika maeneo pengine ya uchunguzi pamoja na pia kumkamata mtu na kumtia hatiani. Leo ukiangalia maeneo mengi ya polisi zetu pale ambapo panahitajika vifaa, gari, mafuta au uthibitisho unakuta kuna changamoto za vifaa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kule jimboni kwetu Tunguu ukenda kwenye kisiwa cha Uzi unakuta wakati mwengine kituo cha polisi kimefungwa. Ukenda maeneo mengine unakuta vifaa na vitendea kazi hawana. Sasa naomba sana katika kuteleleza sheria hii na hasa eneo la kumwezesha hayo mahojiano na kuweka rekodi, ikiwa ni rekodi ya maandishi au rekodi ya kurekodiwa sauti, maana kuna watu wengine wana ulemavu. Unapotaka kuweka rekodi ni lazima na hao askari au wanaosimamia kazi hiyo wawe wameweza kupata vitendea kazi vizuri. Serikali nayo iangalie vizuri sana katika mfumo mzima wa sheria hii ili waweze kuhakikisha kwamba mambo yote yanakuwa.

Mhe. Mwenyekiti, pia suala la elimu, wananchi wetu leo ukimwambia tu mtu nakupeleka mahakamani pengine hana kosa lolote na pengine yeye angeshinda hiyo kesi, basi anapata khofu na hata kuanguka na kuzimia unapomtajia kwamba nitakupeleka mahakamani. Yote haya yanatokana na kutokufahamu haki yake.

Mhe. Mwenyekiti, umuhimu wa sheria hii ili kuweza kuifikisha kwa wananchi sisi kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi inawezekana tukafanya. Nimpongeze sana Mhe. Ali Suleiman Ali

(Shihata) yeye ni mtaalam ameongea vizuri na amebeba jukumu hilo pia kwa niaba ya wananchi wake na mimi nitalibeba.

Lakini katika kutekeleza kazi hii hatuwezi tukawafikia wananchi wote tukawafahamisha kwamba tunapokwenda majimboni kwetu tuna mengi ya kuzungumza, kuna siasa, kuna mambo ya michango ya kuwasaidia wananchi wetu, kuna mambo ya kushirikisha jamii katika kazi za kila siku na kuna mambo ya kusikiliza matatizo yao ambayo waliyokuwa nayo. Haya ambayo ni jukumu la serikali tushirikiane kwa pamoja na elimu itakayokwenda kuwafikia isiwe elimu kali kama alivyosema Mhe. Ali Suleiman Ali, ile lugha ya Kiingereza. Elimu itakayokwenda iwe katika mashule ya sekondari pamoja na vyuo, iwe ni elimu inapitishwa katika njia watakayoweza kuifahamu. Katika haya makosa yanayofanywa unakuta makosa mengine yapo zaidi kwa vijana, watu wenye umri wa kati kati. Kuna makosa mengine yanafanywa katika jamii na watu wote. Ule mfumo wa elimu katika kuipeleka tusitumie mawazo baada ya saa 8:30 au taarifa ya habari ya saa 9:00, tujue nyakati ambazo vijana, wazee, utakuwa unawafikia ule ujumbe.

Lakini pia katika kupeleka hizi sheria tunaweza tukafungua mitandao ambayo ya kisasa kama *face book* vijana wengi wanatumia kila siku, ukatoa mada moja ya sheria kifungu kimoja ili kiweze kujadiliwa na watu ikaweza kuwafikia ile elimu. Hili ndilo litaweza kuwasaidia wananchi ule ufahamu wao kuwajengea. Lengo hapa ni kuhakikisha mwananchi sio kwamba anapewa adhabu lakini moja ni kuhakikisha kwamba yule mtu hafanyi lile kosa.

Mhe. Mwenyekiti, katika sheria hii jambo kubwa sana ni elimu kuweza kuwafikia wananchi wetu. Sheria ni nzuri kabisa na hata tukipingana katika mfumo je, tuweke suala la mtu kwamba anyongwe, adhabu ya kifo iwepo au isiwepo. Mimi huko napata

mashaka kwa sababu hata na mimi mwenyewe pia sijawahi kukutwa na jambo ambalo nikasema huyu mtu fulani madhali kanifanyia makosa haya basi na yeye anyongwe. Lakini ukienda kwa mtu ambaye mtoto wake ameharibiwa, mtu ambaye mama yake amepigwa kisu amekufa, basi na yeye atakwambia kwa uchungu basi na yeye huyo anastahiki kufa, anastahiki kunyongwa. Masuala haya yana pande mbili za shilingi kwa hivyo kama mjadala utahitajika mrefu wa kitaifa katika kuzungumza suala zima juu ya adhabu ya kifo ili kupatikane muafaka.

Mhe. Mwenyekiti, tunajua imani za viongozi wetu, tunafahamu historia ambazo viongozi wetu walipotoka nayo. Mambo haya ambayo yamo humu mengine yanahitaji mazungumzo. Ndio maana leo nikasema sheria hizi tunazozipitisha hapa pale ambapo tutaona kuna kasoro naomba sana Mhe. Waziri asione tabu kurudi kwa haraka ili tuweze kufanya marekebisho. Marekebisho haya tunapoyafanya ndivyo tunavyoweza kuwafikia wananchi wetu, ndio tunawasaidia wananchi wetu na ndio msingi wa Chama chetu cha Mapinduzi kuelekea mwaka 2020.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niongelee kwenye kifungu cha 44 “Uwezo wa kuchukua alama za vidole na picha za watuhumiwa”. Unaweza ukaenda katika maeneo mengine ule wino ukaambiwa umefungiwa kwenye *draw* askari hayupo, inaweza ikatokezea kwa sababu vifaa walivyokuwa navyo ni vichache. Tunawalamu askari wetu, tutawalaumu maeneo tofauti lakini tunapokuja kwenye bajeti hapa, fedha ambazo tunazotakiwa ziende katika vituo vya polisi ni suala la Jamhuri ya Muungano sio SMZ. Kwa hivyo, vitendea kazi katika maeneo tofauti tuhakikishe kwamba nako tunashirikiana vizuri katika kuboresha maeneo hayo.

Maana yake kifungu cha 44 anasema:

Kifungu cha 44:

"Mkuu wa kituo cha polisi au afisa yeyote wa polisi anayepeleleza kosa anaweza kuchukua au kuwezesha kuchukuliwa vipimo au alama za mikono, vidole, nyayo, au vidole vya miguu, au rekodi za sauti au, picha ya, au sampuli za maandishi ya mkono ya mtu ambaye anashtakiwa kwa kosa...".

Mhe. Mwenyekiti, mimi maishani mwangu nikienda katika kituo cha polisi labda kitu ambacho nitakachokiona kinatumia umeme ni feni, taa na ukibahatika kuna TV. Namuona kule Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto anapeleka kichwa chake inaelekea kwamba ananiunga mkono mawazo yangu, kwa sababu najua yeye pia katika kutekeleza sheria zake na kuwalinda watoto na akina mama zetu anapata mitihani mikubwa sana pale wanapofika katika vituo hivi. Kwa hivyo, mimi naomba sana katika suala la vitendea kazi, masuala haya yapo ndani ya jamhuri. Leo tunapitisha sheria hapa ikiwa kituo cha polisi hana wino tunafanyaje. Maana yake bajeti hiyo ipo ndani ya Jamhuri. Tunapitisha sheria hapa lakini yule ambaye anatakiwa atekeleze jukumu lake anayesimamia ni jamhuri. Sasa hapa tunawaunganisha vipi katika kuona tunatekeleza majukumu yetu kuona tunakwenda vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ninachoomba katika masuala ya vitendea kazi ushirikiano uwe mzuri pamoja na jamhuri ili haya yote ninastahiki kusema kwa undani lakini nakumbuka huko nyuma *OCD* anapewa sijui lita nne au tano labda pengine viongozi na serikali inawaongezea bajeti katika suala zima. Lakini humu ukenda katika vituo vya polisi vyote hata ukiingia katika hizo selo zenyewe mazingira yaliyokuwemo humo ndani na mazingira ya polisi, hata yule mtu kumpa *confidence* kwenda kupeleka kuripoti jambo ambalo tukio limemkuta anakuwa hana uhakika nalo pale wakati mwengine unakuta kuna mabishano. Sasa mimi niombe sana katika suala la vitendea kazi itakuwa ndio

katika sehemu moja pia kubwa sana kuhakikisha utekelezaji wa sheria hii hasa hata watu ambao inawagusa kila siku.

Lakini pia Mhe. Mwenyekiti, hapa tunaongelea kuhusu sheria hii ambapo watu wamewahi kufanya makosa. Mimi nataka nifahamishwe na Mhe. Waziri naomba utakapokuja uje unipe ufafanuzi mzuri sana kuhusu utumiaji wa silaha za moto, ni suala ya Jamhuri ya Muungano, ni sheria ambayo Zanzibar inasema hairuhusiwi. Lakini silaha za moto kutumia bastola na bunduki yale ambayo Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf alikuwa anayazungumza sana mwaka jana haya yote hayaruhusiwi Zanzibar. Sasa ikiwa hayaruhusiwi Zanzibar mtu akikutwa nayo ni sheria ipi itamtia hatiani na adhabu ipi ambayo inamkuta humu ndani, aidha akiwa ametumia kwa maovu kwa kumtisha mtu ni kwa eneo lipi. Sasa naomba sana Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri atakapokuja atueleze suala zima la mfumo huo.

Lakini pia tukienda kwenye kifungu cha 151 kinasema Uwezo wa jumla wa kutoa dhamana. Kinazungumzia masharti kuhusu dhamana kinasema hivi:

Kifungu cha 151:

"(1) Pale mtu yeyote, asiyekuwa mtu anayeshtakiwa kwa kuua kwa kukusudia, uhaini, unyang'anyi wa kutumia silaha, kukutwa na silaha, kusafirisha dawa za kulevya, kosa linalohusu kiwango kikubwa cha dawa za kulevya, kubaka, kuingilia kinyume na maumbile, kunajisi mtoto wa kiume, kubaka…"

Nasema kwamba mwisho kinamalizia hivi:

"Na yupo tayari wakati wowote wakati yupo kwenye hifadhi ya afisa huyo katika hatua yoyote ya mwenendo wa

shauri mbele ya mahakama hiyo kuweka dhamana, mtu huyo anaweza kupewa dhamana."

(2) Mkuu huyo wa kituo cha polisi au mahakama, badala ya kuchukua dhamana kutoka kwa mtu huyo inaweza, kumuachia mtu huyo atakapotekeleza ahadi ya dhamana bila ya wadhamini kwa ajili ya kuhudhuria kwake kama itakavyoelezwa baadae".

Mimi naomba kidogo Mhe. Mwenyekiti, wakati Mhe. Waziri atakapokuja au Mwanasheria Mkuu atufafanue zaidi hapa kuhusu dhamana kwa sababu hili ni suala la elimu. Ukiangalia hapa napata kidogo sintofahamu kwamba tunakusudia nini hasa kwenye dhamana hii na hapa nataka nizungumze suala la dhamana.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye suala la dhamana lazima wananchi wetu wafahamishwe unaambiwa mtu anapopewa dhamana anatakiwa awe mtulivu, awe msikivu, awe mfano mzuri katika jamii, lakini watu wanapewa dhamana nchi hii wakitoka huko nje wanafanya makosa. Masheha wanawatambua lakini pia hakuna kiunganishi wa kuweza kuwa *monitor* na kufahamu mwenendo wao mzima kubwa unaloambiwa wakati mwengine aripoti saa 1:30 polisi au aripoti saa 8:00. Sasa kuja polisi saa 8:00 kuripoti au kuja saa 1:30 haimaanishi kwamba yule mtu katika jamii ni mfano mzuri bado na hafanyi makosa yoyote, anapokuja kuripoti katika kituo anathibitisha kwamba yeye bado yupo hapa katika Visiwa vya Zanzibar.

Sasa lazima nataka nifahamu ni njia ipi tunahakikisha kwamba katika sheria hii wale ambao wanapewa dhamana wanakuwa ni mfano mzuri katika jamii na ili wanaendelea kufanya kazi au shughuli zao za kila siku bila ya kuharibu na kufanya mambo mengine.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nataka nichangie kifungu cha 269, 270, 271 na 272. Kifungu cha 269 kinazungumzia utoaji wa adhabu kinasema hivi:

Kifungu cha 269:

"Ikiwa Jaji anamtia hatiani mshtakiwa anakiri kosa, itakuwa ni wajibu wa mahkama kumuuliza mshtakiwa kama ana chochote cha kusema kwa nini adhabu isitolewe kwake yeye kwa mujibu wa sheria, lakini kuacha kumuuliza mshtakiwa hakutakuwa na athari katika uhalali wa mwenendo wa kesi."

Mhe. Mwenyekiti, wakati mwengine mtu ambaye pengine hana kosa au alifanya kosa sio la makusudi anapopelekwa katika mahkama zetu hizi unakuta wakati anakosa nafasi ya kumpata mwanasheria kuweza kumsaidia. Unawakuta wafanyakazi au watu ambao katika maeneo pale pale katika mazingira ambayo alikuwemo anaambiwa mtu akubali kosa, anakubali kosa wakati alikuwa hana kosa anaambiwa akiri kosa ili jaji amsamehe. Inaweza kuwa alikuwa anaendesha gari akaua aidha mtoto bila kukusudia akafika pale mbele akaambiwa au akashauriwa na watendaji ndani ya mahkama kwasababu tayari ameshachanganyikiwa yeye ametiwa ndani ya *lockup* anapelekwa mahkamani anakubali kukikri kosa kwa kosa ambalo yeye hajafanya kwa makusudi.

Mhe. Mwenyekiti, namalizia nishaona taa yako. Lakini hapo hapo yeye anakubali lile kosa badala yake kinachomkuta anatiwa hatiani anashtakiwa na anafungwa kifungo kuliko ambacho yeye angeweza kujitetea mwenyewe.

Ninaomba sana katika suala zima la utoaji wa adhabu, suala zima la kusimamia sheria hii wafanyakazi wetu ndani ya mahkama

miingiliano yao pamoja na watu ambao aidha wao wana makosa au hawana makosa basi wawe wamekaa mistari miwili kama *parallel lines.* Yaani wasiwe kila wakati wao wanaingilia ili kujenga mahusiano ambayo yalikuwa hayapo na wao kujigeuza ni ma-*legal counsel wao* au washauri wa kisheria kwa ajili ya hao watu.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie katika kifungu cha 286 juu ya suala zima la kuhujumu uchumi. Naomba sana Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri atakapokuja atutolee maelezo ya kina hiki kifungu ili wananchi wetu huko nje waelewe vizuri. Sio tena baadae mambo yanakuja kutokezea ambayo yalikuwa sipo yapo tuambiwe sasa mtu yeyote akifanya hili ataonekena yeye ni mbaya nchi yetu inaendesha masuala ya kibiashara, wengine bado ufahamu wao kwao ni mdogo ni vizuri wakafahamishwa.

Baada ya hapo Mhe. Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kukushukuru wewe kwa nafasi uliyonipa, niwashukuru Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa kunisikiliza nasema ahsanteni sana. Naunga mkono hoja mia juu ya mia, ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Simai kwa mchango wako sasa naomba nimwite Mhe. Suleiman Makame Ali na kama muda utaruhusu basi Mhe. Shehe Hamad Mattar ajiandae.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Mhe. Mwenyekiti, kwanza kwa ruhusa yako nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Wizara hii, nimpongeze Mkurugenzi wa Mashtaka kwa kazi kubwa waliyoifanya ili kuhakikisha kwamba wanatuletea sheria hizi ambazo ilikuwa vilio kwa jamii yetu ya Zanzibar ambayo siku nyingi wananchi wanalalamika lakini nadhani sasa dawa imepatikana.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sitosema sana kwa sababu ni Mjumbe wa Kamati hii iliyowasilisha hapo Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum masuala yote tumeyapitia.

Mhe. Mwenyekiti, kusema la ukweli mswada huu ni mzuri, mkubwa na sisi kamati tulikaa kama muda wa siku sita tukijadili na kushauriana ili kuhakikisha pale penye kasoro tunapaweka sawa.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, kwa faida ya wananchi pamoja na Baraza hili kwenye kifungu cha 376 kidogo nikitaka ufafanuzi tu hapa Mahkama Kuu inaweza katika utekelezaji wa mamlaka yake ya jinai kutoa amri yoyote ambao inaweza kutolewa Mahkama za Uingereza. Mhe. Mwenyekiti, hapa kidogo nilikuwa nataka ufafanuzi kwa sababu nikiwa kama mjumbe wa kamati yawezekana ikawa hili sikuliona.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende kifungu cha 337 kinasema kurejesha mali iliyoibiwa. Mhe. Mwenyekiti, mara nyingi hapa huwa na huku kuna matatizo kwamba zile mali zinazoibiwa ama iwe majambazi au watu wa kawaida kwa vile ni wizi kuwa zile mali baadhi ya nyengine hazipatikani. Sasa Mhe. Mwenyekiti, hapa mimi nataka hili suala nikupe mfano. Mhe. Mwenyekiti, kuna siku moja walitokea wavuvi kule Tanga wakavua samaki wakakamatwa kufika mahkamani samaki wale wakatakiwa kama ushahidi ikawa wameshapikwa wameshaliwa hawapo tena kwa hivyo ile kesi ikawa haipo.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, siku nyengine wale wezi wanaiba zile mali wanakamatwa kuna mambo yanafanyika wale waliokwenda kudai zile mali zao huwa wanazikosa. Kwa hiyo Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba hili lichukuliwe zaidi na lifanyiwe kazi ili kuhakikisha kwamba vitendo hivi vinazuiwa.

Mhe. Mwenyekiti, zaidi niseme sina cha ziada isipokuwa ni hayo na hoja yangu ilikuwa ni hiyo. Mhe. Mwenyekiti, mimi naunga mkono asilimia mia kwa mia ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Nakushukuru sana Mhe. Suleiman Makame Ali sasa naomba nimwite Mhe. Shehe Hamad Mattar.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kuchangia machache katika mswada huu kwa jioni hii. Namuomba Mwenyezi Mungu aniwezeshe nichangie kwa utulivu na amani kabisa na ueleweke.

Mhe. Mwenyekiti, katika mswada wetu wa leo kwanza nitangulize shukrani zangu za dhati kwa kamati ambayo imeupitia mswada huu pamoja na wale wote ambao wameuandaa hadi kutuletea mbele yetu na leo tukapata fursa ya kuujadili. Pia wale wote ambao hawajachangia niwaombe wachangie na mimi naanza kuukubali mia juu ya mia pamoja na marekebisho yake.

Mhe. Mwenyekiti, mchango wangu mimi naanza katika sehemu ya kwanza palipoanza kutoa maneno tafsiri hapa nimeona kuna mambo sijaona tafsiri yake wakati tunatumia sheria hii.

Tafsiri ya neno katiba hapa halikutafsiriwa na humu ndani limetumika. Naomba iangaliwe sana katiba ipi iliyokusudiwa kuitumia matumuzi ya katiba humu kwenye mswada huu. Lakini pia tafsiri ya silaha haikutolewa katika tafsiri zilizopo hapa hazipo na huko ndani tumezitumia hizi neno silaha, ningeomba itafutwe silaha ya aina gani hapa.

Lakini niende tena katika ukurasa wa 233 kifungu kilichosema tafisiri ya neno "afisa wa utabibu" naomba ninukuu.

"Maana yake ni daktari yeyote aliyeajiriwa na Serikali aliyesajiliwa chini ya masharti ya Sheria ya Madaktari na Madaktari wa Meno kifungu cha 12 (1)".

Hapa naona kwanza kama walivyopendekeza hawa kamati na mimi nasema hichi kifungu kiondolewe ili maneno matatu hapa yaandikwe, maneno ya mwisho kifungu cha 12 (1) napendekeza nayo yaondolewe kwasababu hayaleti maana hapa.

Lakini sasa swali langu hapa linasema kwamba Afisa wa Utabibu ni yule ambaye aliajiriwa na serikali. Sasa je, wale maafisa matabibu ambao wamo katika hospitali binafsi wasieleweke hawamo katika tafsiri hii watakapofanya mambo haya. Naomba sana atakapokuja waziri anieleze zaidi madaktari binafsi je, wenye leseni za serikali wasitambuliwe.

Niende katika sehemu nyengine ukurasa wa 235 kifungu ch 5 (1) naomba nikinukuu kwa haraka sana.

Kifungu cha 5 (1):

"Kosa lolote chini ya sheria yoyote isiyokuwa Sheria ya Adhabu, pale ambapo mahakama yoyote imetajwa kwa ajili hiyo katika sheria hiyo, litasikilizwa na mahakama hiyo".

Hiyo hiyo imekuwa imejieleza sana naomba sana patiwe neno mahakama ipi ielezwe kama Mahkama ya Mkoa, Wilaya au ya Rufaa ielezwe hivyo baada ya kuacha mahkama hiyo hiyo. Lakini kifungu cha 5 (2) kinasema.

Kifungu cha 5 (2):

"Pale ambapo hakuna mahkama iliyotajwa, linaweza,…".

Hapa kuna neno linahitajika naona kama hivi shauri kuna neno linahitajika kuingizwa kwasababu linaweza tu, hatujajua kitu gani kinazungumzwa hapa napendekeza sana litiwe neno shauri linaweza, kwa kuzingatia masharti mengine ya sheria hii,… iendelee hivi isomeke hivyo Mhe. Mwenyekiti.

Lakini tuendelee tena katika sehemu ya tatu Masharti ya Jumla kuhusu Kukamata, Kutoroka na Kukamata Tena kifungu cha 12 (1) naomba kisomeke hivi:

Kifungu cha 12 (1):

"Katika kukamata afisa wa polisi au mtu mwengine anayefanya ukamataji kwa mujibu wa sheria…"

Liingizwe neno hapo kwa mujibu wa sheria halafu iendelee "…atamshika kikamilifu au atauzuia mwili wa mtu anayetaka kukamatwa…".

Lakini mwisho wa neno vitendo liongezwe neno hili kabla ya kukamatwa ataarifiwa tuhuma ya kosa lake yule ambaye anakwenda kukamatwa asiwe tu anaambiwa tunakukamata. Aarifiwe unakamtwa kwasababu fulani na haya hata ndani ya mapolisi huwa tunasikia hivyo, lakini hawatekelezi unakwenda unakamatwa unaambiwa utajua polisi au utajua unapokwenda hiyo sio haki aelezwe na mtuhumiwa yule pale wakati ule hajajulikana kosa lake aweze kujua kwamba ninakwenda kujibu nini akifika huko atakapoulizwa. Sio kama anakwenda anachukuliwa tu kwamba anatiwa pingu twende, kosa langu nini jamani, utakwenda kujua huko. Vyombo vyetu vinafanya mambo kama haya naomba sana iweke wazi kitu hichi.

Lakini kifungu cha 2 pale inapozungumza "Ikiwa mtu huyo atakaidi kwa nguvu juhudi za kumkamata, au atajaribu kukwepa

kukamatwa, afisa huyo wa polisi au mtu mwengine anaweza kutumia njia zote za lazima…". Hili neno njia zote za lazima hapa tunatoa uhuru mkubwa kufanikisha ukamataji huo, hebu tunaona bora tuzitaje njia za lazima ni kama zipi hapa tusiseme tu huyu akaja kusimamia akajaribu kutengeneza mazingira akasema mimi natumia njia za lazima zipi zioneshwe hapa. Hii inawezekana pengine akampiga au akamtia madawa ya sumu pale yeye ndio anaweza, nadhani zingetajwa hizi njia ambazo zinahitaji kuchukuliwa za lazima.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika ukurasa wa 240 kifungu cha 21(1)(e) naomba ninukuu.

Kifungu cha 21 (1)(e):

"mtu yeyote aliyetiwa hatiani na kuachiwa anatenda kosa la kuvunja sharti lolote lililoainishwa katika kifungu cha 328 cha sheria hii au kanuni yoyote iliyotengenezwa chini yake".

Mhe. Mwenyekiti, tatizo la baadhi ya miswada yetu inayoletwa hapa kama nilivyozungumza mwanzo kwanza iangaliwe tena upya kabla haijawasilishwa hapa. Tunavitaja vifungu hapa kuvitumia halafu tunapitisha lakini ukienda kifungu chenyewe sivyo kinavyoeleza. Tukiangalia hiki kifungu cha 328 cha sheria hii, ndivyo kinavyoeleza hivi masuala haya ni tofauti kabisa na ilivyo na kitu kama hiki. Mhe. Mwenyekiti, naomba niepuke kidogo kimetuathiri hata baadhi ya sheria zetu zinazopitishwa katika Baraza hili tukufu ambalo tayari limeshapitishwa naona, ilipopitishwa Sheria ya Michezo, Mabaraza ya Michezo ya Wilaya utaikuta kesi hiyo kama ipo mpaka leo Baraza hili sheria ile ina makosa na inachukuliwa ni sahihi.

Kwa hivyo, mtu ambaye ataabidhiwa na kupewa adhabu kwa mujibu wa sheria ile mfano hicho ni kifungu cha 24 cha Baraza la

Michezo la Wilaya yake kilikosewa tokea mwaka huo na mpaka leo kinaendelea hivyo hivyo kwamba badala ya kuandikwa mwaka naomba nikiseme vile kifungu kilivyokuwa sheria hiyo ya michezo na leo isije ikatokezea hapa. *Zanzibar Sports Council* Nam. 8 ya mwaka 1998 ndivyo ilivyoandikwa lakini kumbe ilikusudiwa ya mwaka 1984.

Kuondoka ile nne tu tayari hapa limeshakuwa ni kosa mwanasheria akija hapa wakili atakuja kumuangalia jamani huyu mtu mnamhukumu kwa kosa gani, kwa sheria ipi, akija akitizama ile sheria mpaka leo haijafutwa ya michezo.

Kwa hivyo, hii leo natahadharisha sana mambo ya vifungu hivi kwamba tuviangalie vizuri sana kwasababu katika utaalam wetu sisi tunaweza tukawa hatuvioni, lakini nyinyi mnaotayarisha miswada hii mviangalie sana natoa tahadhari sana katika hilo.

Lakini niendelee kuchangia katika ukurasa 244 kifungu cha 31 kinachosema kuwashughulikia watu waliokamatwa na watu binafsi hapa pametajwa naomba ninukuu.

Kifungu cha 31:

"Mtu yeyote binafsi anayemkamata mtu mwengine yeyote bila ya hati atalazimika, bila ya kuchelewa, kumkabidhi mtu huyo aliyekamatwa kwa afisa wa polisi,… na kuendelea"

Lakini hapa sasa suala la kukamata sio polisi peke yake kuna vyombo vyengine ambavyo vina mamlaka kama hiyo mfano *ZAECA*, Maliasili ziko sheria wakikamata mali ambayo sio wanayo haki ya kukamata, *ZRB* wanayo haki ya kukamata. Kwa hivyo, hapa nadhani ni vyema na hivi vyombo vyengine tukavihusisha kwa sababu hizo kesi baadae zitakwenda mahkamani. Lakini mtu anaweza kujitetea akasema sheria haipo

hivyo imesema mtu polisi tu kwa hivyo tuvitambue hivyo vyombo vyengine ambavyo haviko mbali ya polisi.

Jambo jengine Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako niende katika kifungu cha 151 ukurasa 276 Masharti kuhusu Dhamana. Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu ni kifungu cha 151 (4) kinachosema hivi:

Kifungu cha 151(4):

"Bila ya kujali chochote kilichomo katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Jaji Mkuu anaweza katika kesi yoyote kuelekeza kwamba mtu yeyote apewe dhamana."

Hata Mhe. Simai Mohammed Said (Mpakabasi) alikizungumzia kifungu hiki. Mhe. Mwenyekiti, hapa nashauri sana majukumu haya asiachiwe Jaji Mkuu peke yake, majukumu haya wapewe hata majaji wengine, wale ni majaji ambao wameteuliwa na Mhe. Rais wa Zanzibar kwa kuwaamini. Kwa hivyo, leo tunampa dhamana hii Jaji Mkuu peke yake na jaji huyu ambaye yeye akiwa katika kuhukumu kesi anaweza akafanya hivyo na akihukumu kesi pale ni sawa sawa na majaji wengine. Sasa vipi leo mtu huyo ataweza kutoa hukumu abadilishe hukumu yake ile aliyosema asipewe dhamana. Tuwape fursa na majaji wengine ambao ni majaji walioteuliwa na Rais kuweza kutengeneza majukumu haya kama vile alivyopewa Jaji Mkuu. Hayo ni maoni yangu.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine ni katika ukurasa wa 316 sehemu ya kumi na mbili Adhabu na Utekelezaji wake. Aina tofauti za adhabu.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa naomba umalizie.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, naomba nimalizie kidogo katika vifungu namba 292 vimetajwa vifungu

vyote hivi hapa lakini naomba kiongezwe kifungu kimoja (n) tukimaliza (m) pamoja na hii kufilisi. Katika vifungu vilivyotajwa hivi hapa vitajwe na kufilisi pia iwemo miongoni mwa adhabu yatakapotokezea mambo hayo yanayostahiki adhabu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo, niombe sana na nikushukuru sana kwa muda na mimi naunga mkono hoja hii mia juu ya mia pamoja na marekebisho yake. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe na mimi niwashukuru sana kwa michango yenu na naomba niakhirishe Baraza hili mpaka kesho tarehe 13/02/2018 saa 3:00 asubuhi.

(Saa 1:41 usiku Baraza liliakhirishwa mpaka tarehe 13/02/2018 saa 3:00 asubuhi)